BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KIDATO CHA SITA, 2016

## 121 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# RIPOTI YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) 2017

# 121 KISWAHILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624, Dar es Salaam
Tanzania

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2017**

Haki zote zimehifadhiwa

# YALIYOMO


YALIYOMO ... iii
DIBAJI ... iv
1.0 UTANGULIZI ... 1
2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA ... 2
2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ... 2
2.2 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO ... 2
2.2.1 Swali la 1: Ufahamu ... 2
2.2.2 Swali la 2: Ufupisho ... 8
2.3 SEHEMU B: MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA ... 11
2.3.1 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi ... 11
2.3.2 Swala la 4: Matumizi ya Sarufi ... 15
2.3.3 Swali la 5: Matumizi ya Lugha ... 20
2.3.4 Swali la 6: Matumizi ya Sarufi ... 26
2.4 SEHEMU C: UTUNGAJI ... 30
2.4.1 Swali la 7: Uandishi wa Kadi za Mialiko ... 30
2.5 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI ... 36
2.5.1 Swali la 8: Kuenea kwa Kiswahili wakati wa Ukoloni ... 36
2.5.2 Swali la 9: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili ... 42
2.6 SEHEMU E: TAFSIRI ... 49
2.6.1 Swali la 10: Nadharia ya Tafsiri ... 49
3.0 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI ... 57
3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ... 57
3.2 SEHEMU A: FASIHI KWA UJUMLA ... 57
3.2.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla ... 57
3.2.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla ... 63
3.3 SEHEMU B: USHAIRI ... 69
3.3.1 Swali la 3: Uhakiki waUshairi ... 69
3.3.2 Swali la 4: Uhakiki wa Ushairi ... 79
3.4 SEHEMU C: RIWAYA ... 85
3.4.1 Swali la 5: Uhakiki wa Riwaya ... 85
3.4.2 Swali la 6: Uhakiki wa Riwaya ... 94
3.5 SEHEMU D: TAMTHILIYA ... 101
3.5.1 Swali la 7: Uhakiki wa Tamthiliya ... 101
3.5.2 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya ... 108
3.6 SEHEMU E: USANIFU WA MAANDISHI. ... 117
3.6.1 Swali la 9: Usanifu wa Maandishi ... 117
4.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA ... 124
5.0 HITIMISHO ... 125
6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ... 126
Kiambatisho A ... 127
Kiambatisho B ... 128

**DIBAJI**

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa ripoti kuhusu kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika Mtihani wa kuhitimu Kidato cha Sita kwa somo la Kiswahili mwaka 2017. Ripoti hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa kufaulu au kutofaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi, walimu, wazazi na wadau wa elimu kwa ujumla.

Ripoti hii ni tathmini ya mwisho inayoonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa maarifa ambayo waliyapata au walishindwa kuyapata walipokuwa katika elimu ya juu ya Sekondari kwa miaka miwili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika ripoti hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri, wastani au vibaya katika mtihani huu. Ripoti inaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya watahiniwa kupata alama za juu kama vile kuelewa maelekezo na mahitaji ya swali, kuwa na maarifa na ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha na kuwa na uelewa wa mada mbalimbali zilizotahiniwa. Pia ripoti imebainisha sababu za watahiniwa kupata alama za wastani hususani kwa kutoa majibu yasiyojitosheleza. Aidha, ripoti hii imeonesha sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kufanya vibaya kwa baadhi ya maswali ikiwa ni pamoja na kutoelewa matakwa ya swali ama kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana mbalimbali za somo la Kiswahili.

Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mitihani inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania litapenda kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia kuboresha taarifa zinazoandaliwa ili kuwasaidia watahiniwa wanaotegemea kuwa wataalam wa lugha ya Kiswahili kwa siku zijazo.

Mwisho Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Walimu na wadau wengine wa elimu waliohusika katika kutayarisha ripoti hii. Aidha, shukrani ziwafikie wafanyakazi wa Idara ya TEHAMA walioshiriki katika uchambuzi wa takwimu zilizotumika katika taarifa hii.

Dr. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Ripoti hii ni uchambuzi wa kufaulu au kutokufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2017 kwa somo la **121 Kiswahili**. Mtihani wa somo la Kiswahili kwa watahiniwa wa Kidato cha Sita ulifanyika Mei, 2017 na ulizingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili kwa Kidato cha V hadi cha VI. Mtihani huu ulikuwa na karatasi mbili (2) yaani 121/1 Kiswahili 1 na 121/2 Kiswahili 2.

Mtihani wa **121/1 Kiswahili 1** uligawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za *Ufahamu*, *Utumizi wa Lugha*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utungaji*, *Maendeleo ya Kiswahili* na *Tafsiri* ambapo kila sehemu ilikuwa na alama ishirini (20). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali saba (7) kati ya maswali kumi (10). Sehemu A na B maswali mawili (2) kwa kila sehemu na sehemu C, D na E, swali moja kwa kila sehemu.

Mtihani wa **121/2 Kiswahili 2** uligawanywa katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za Fasihi kwa *Ujumla*, *Ushairi*, *Riwaya*, *Tamthiliya na Usanifu wa Maandishi* ambapo kila sehemu ilikuwa na alama ishirini (20). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matano (5) kwa kuchagua swali moja kwa kila sehemu. Aidha, swali la tisa (9) lilikuwa ni la lazima.

Mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2017 ulifanywa na watahiniwa 14,629. Kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2017 ulikuwa mzuri ambapo asilimia 99.88 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata wastani wa alama 35 na zaidi. Ufaulu huu umejikita katika pande kuu tatu za ufaulu, ambazo ni ‘‘vizuri,’’ ‘‘wastani’’ na ‘‘hafifu.’’

Ripoti hii inaonesha uchambuzi wa maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu ili kukuza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Uchambuzi huu unalenga kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kilichofanywa na watahiniwa. Aidha, ripoti hii inaonesha sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutopata alama za juu katika majibu ya maswali kwa baadhi ya mada. Hivyo, uchambuzi huu umeweka mpango mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa mada ambazo hazikufanywa vizuri ili kuboresha kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mitihani yote inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

# 2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

## 2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inafafanua uchambuzi wa kina wa kila swali na majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyofanywa vizuri, wastani na yale yaliyofanywa vibaya. Aidha, sababu za kufaulu kwa kiwango cha juu, wastani au cha chini kwa watahiniwa zimeelezwa bayana kwa kila swali. Chati za kufaulu na sampuli za majibu ya watahiniwa kwa kila swali zimeambatanishwa ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huu.

Viwango vya kufaulu vimegawanyika katika sehemu kuu tatu kwa kuzingatia asilimia ya watahiniwa waliopata alama 35 au zaidi katika kila swali. Kiwango hafifu cha kufaulu ni asilimia 0 hadi 34 na kiliwakilishwa kwa rangi nyekundu; kiwango cha wastani cha kufaulu ni asilimia 35 hadi 59 na kiliwakilishwa kwa rangi ya njano; ambapo kiwango kizuri cha kufaulu ni asilimia 60 hadi 100 na kiliwakilishwa kwa rangi ya kijani.

## 2.2 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO

### 2.2.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali hili lilihusu mada ya *Ufahamu na Ufupisho* na lililenga kupima ufahamu. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyotokana na habari hiyo. Maswali hayo yaligawanyika katika vipengele (a) hadi (f) na vilikuwa na jumla ya alama 10.

Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari kisichozidi maneno matano na kilikuwa na alama 1.

Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kueleza mawazo makuu ya mwandishi kutokana na habari na kilikuwa na alama 2.


Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya maneno aliyopewa kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Maneno hayo ni (i) *Hazina* (ii) *Kitambo* (iii) *Hutakasa* (iv) *Peponi*. Kipengele hiki kilikuwa na jumla ya alama 4.

Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kuthibitisha usemi, ‘‘nyumba nzuri si mlango fungua uingie ndani’’ na kilikuwa na alama 1.

Kipengele (e) kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya usemi “Ukitaka kumficha mjinga mpe kitabu” na kilikuwa na alama 1.

kipengele (f) kilimtaka mtahiniwa kueleza ushauri wa mwandishi kuhusu vitabu vipya na kilikuwa na alama 1.

Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la lazima. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na idadi kubwa ya watahiniwa. Asilimia 96.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani na zaidi kutokana na kujibu vipengele vingi vya swali hili kwa usahihi. Chati Namba 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 1**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Watahiniwa wengi (72.0%) walifanya vizuri na kupata alama 6 hadi 10 kwa kuwa waliweza kuandika kichwa cha habari, kuelezea mawazo makuu ya mwandishi na kutoa maana za maneno kama yalivyotumika katika habari kwa usahihi. Aidha, waliweza pia kueleza maana ya usemi “ukitaka kumficha mjinga mpe kitabu” na wengine waliweza kung’amua ushauri wa mwandishi kuhusu vitabu vipya. Kielelezo 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vipengele vyote vya swali kwa usahihi.

**Kielelezo 1.1**

1 a) UMUHIMU WA KUSOMA VITABU

(b) (i) Kujiwekea tamaduni za kujisomea vitabu mara kwa mara ili kupata maarifa, busara akili na kuongeza werevu

(ii) Kuchagua vitabu vya kusoma kwasababu si kila kitabu kina mafundisho mema vingine vina ambukiza maovu, hivyo katika wakati huu uliojaa vitabu vingi vizuri na vibaya, ni vyema kufanya uchaguzi wa kitabu kabla ya kununua. Ndio maana mwandishi anasema "Nyumba nzuri si mlango, fungua ndani uingie" akimaanisha usichague kitabu kwasababu ya jalada zuri bali tazama yaliyomo / yaliyoandikwa ndani ya kitabu.

C (i) Hazina - thamani


(ii) Kitambo - zamani / vilivyopita na wakati.

iii) Hutakasa - husafisha.

iv) Peponi - mahali patakatifu

d)

Mwandishi anaposema "Nyumba nzuri si mlango, fungua uingie ndani" anamaanisha kitabu kizuri cha kusoma si kile chenye jina zuri na jalada la kupendeza tu bali kile kilichoandikwa ndani ya kitabu ambacho ndicho muhimu zaidi kwa msomaji. Kitabu kinaweza kuwa na jina zuri na jalada la kupendeza lakini kilichoandikwa ndani ya kitabu kinaweza kuwa ni cha kupotosha, kisichona maadili au chenye maovu hivyo wanunuzi wa vitabu ni busara kununua kitabu kwa kutazama pia kilichoandikwa ndani ya kitabu badala ya kununua kitabu kwasababu ya kupendezewa na jina au jalada la kitabu.




e) Maana ya usemi "ukitaka kumficha mjinga mpe kitabu" kinamaanisha ukitaka kumsaidia mtu iwe kwa hekima, busara, akili au muongozo mpe kitabu, kwasababu ya watu wengi (wajinga) kutokupenda kusoma vitabu na kutokuwa na utaratibu wa kujisomea kitabu mtu huyu (mjinga) hataweza kusoma kitabu na kutokujua kilichomo ndani ya kitabu na atabaki na ujinga wange.wake

f) Ili tuweza kupata maarifa mwandishi anatushauri tusome vitabu vipya kabisa, pia tunaweza kusoma vitabu vya zamani kabisa ila kwa jicho la hekima ili kuongeza maarifa zaidi.

Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahinwa aliyeweza kufuata matakwa ya swali kwenye vipengele (a), (b), (c), (d), (e) na (f) kwa usahihi na kupata alama zote.

Asilimia 24.6 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango cha wastani. Watahiniwa hao walipata alama za wastani yaani 3.5 hadi 5.5 kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele ambapo vipengele vingine vilikuwa na majibu yasiyojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu vizuri vipengele (b), (c) ii, iii na (f) lakini katika vipengele 1(a), (c) (i),(iv),(d),(e) alitoa majibu ambayo si sahihi. Kielelezo 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu baadhi ya vipengele na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 1.2**


1 a) VITABU NI HAZINA BORA.

b) - vitabu ni rafiki.

- vitabu ni hazina.

c i. Hazina - hakiba ya baadaye.

ii. kitambo - ~~vya~~ muda mrefu uliopita.

iii. Hutakasa - husafisha au upendezesha.

iv. Peponi - mahali penye amani.

d. Anamaanisha sio kila kionekacho kizuri kwa macho kinapendeza.


e. Anamaanisha ukitaka kumuelimisha mjinga ache ujinga na kuwa mueleuu mpe kitabu hajifunze.

f. mwandishi anashauri husome vitabu vizuri ili kustawisha akili, kujenga tabia nzuri.

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu baadhi ya vipengele kwa usahihi na kushindwa kujibu vipengele vingine vya ufahamu. Pia mtahiniwa anaonesha kuwa na makosa ya kitahajia katika kipengele (e) ambapo aliandika "hajifunze" badala ya "ajifunze."

Watahiniwa wachache, asilimia 3.4 pekee, ndio walioshindwa kujibu swali hili kutokana na kukosa uelewa na maarifa ya kutosha kuhusu ufahamu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) aliandika kichwa cha habari kwa herufi ndogo badala ya herufi kubwa, na katika vipengele (b), (c) (iii), (iv) alitoa maana ambazo sio sahihi kulingana na kifungu cha habari. Aidha, mtahiniwa mwingine aliweza kujibu kwa usahihi kipengele c(i), na c(ii) lakini katika kipengele (d), (e) na (f) mtahiniwa alitoa majibu ambayo sio sahihi. Kielelezo 1.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vipengele kwa usahihi na kupata alama za chini.

**Kielelezo 1.3**



1.

~~a) Elimu~~

a Uongozi Mzuri una Faida.

b) i) Mwandishi anasema kuwa ili kufanya jamii iwe vizuri ni kuzima kusoma vitabu ambavyo vimesomwa na watu wakitafunga kwa kupata maadili zaidi.

ii) Uongozi mbaya na kuzima upeyuwe vita. kwa sababu wakuu na uongozi mbaya huku viziwi na viziwi kuwa na uongozi mbaya usiokuwa na maendeleo.

c i) Hazina ya Akiba

ya Akiba: kwa sababu mwandishi anasema vitabu ni hazina kwa.

ii) Zamani


Jicini ni vitu vya zamani vilivyopita.

iii) Huelimisha.

kusini anasoma vitabu vizuri hu-kuza na kuenga kubwa nzuri.

iv) Sehem nzuri

kwa sababu mwandishi anasema kitabu kizuri ni rafiki kweli pekee.




Kielelezo 1.3 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vipengele vingi kutokana na kukosa uelewa na maarifa ya ufahamu.

### 2.2.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilihusu mada ndogo ya *Ufupisho* na lililenga kupima matumizi ambapo mtahiniwa alitakiwa kutumia ufahamu ili kufupisha habari aliyoisoma. Swali lilikuwa na alama 10 na lilimtaka mtahiniwa kufupisha habari kwa maneno yasiyozidi mia moja na ishirini (120).

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa la lazima. Asilimia 95.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walijibu vizuri na kupata alama za wastani na zaidi na kulifanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi. Chati Namba 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 2**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Watahiniwa wengi, asilimia 68.3 walifanya vizuri na kupata alama za juu 6 hadi 10. Kiwango kizuri cha kufaulu kwa watahiniwa kilitokana na kuzingatia mpangilio wa mawazo wenye mantiki, matumizi ya alama na vituo, kutumia maneno mengine tofauti na yale yaliyotumika katika habari bila kupotosha kiini cha habari ya awali, kuzingatia idadi ya maneno na matumizi ya lugha sanifu. Kielelezo 2.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika ufupisho unaokidhi kanuni na taratibu za ufupisho.

**Kielelezo 2.1.**

2. Vitabu ni rafiki bora wa wanadamu kwani bila ukurasa wa kitabu unamanufaa makubwa kwa msomaji na ni akiba maishani. Vitabu vizuri ni rafiki kwa binadamu kwani vimebeba ujuzi, maarifa na maadili mazuri yafaayo maishani. Binadamu wa sasa ni tofauti na wa zamani kwani sasa vitabu vipo karibu nasi tofauti na wazee wa zamani walitumia muda mwingi kutafuta maneno ya wenye hekima.


Ni vizuri kusoma vitabu ili inapaswa kuwe na uchaguzi mzuri wa vitabu vitakavyoweza kumjenga mtu katika maadili mema. Na pia inapaswa mtu kujue maudhui ya kitabu bila kuangalia uzuri wa jalada na asome kwa umakini na uelewa mkubwa.

Vitabu vibaya huharibu akili na vitabu vizuri hujenga akili. Inapaswa Tusome vitabu vizuri ili kunufaisha akili na kupata ujuzi na maarifa ya kutumia katika maisha yetu ya kila siku.

Kielelezo 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyezingatia kanuni za uandishi wa ufupisho na kupata alama za juu.

Asilimia 27.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 3.5 hadi 5.5 kutokana na kushindwa kuzingatia baadhi ya kanuni za ufupisho kikamilifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kutumia maneno yake mwenyewe na kutozingatia matumizi ya alama za uandishi kwa usahihi. Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefupisha habari bila utoshelevu.

**Kielelezo 2.2**




2 Vitabu ni sehemu muhimu katika maisha ya binadamu kwa sababu hutuongezea maarifa kwenye stadi mbalimbali za maisha, kama vile dini, elimu na biashara. Kutokana na kusoma kwa vitabu vingi sisi tunashauriwa kusoma vitabu vitakavyo tuongezea maarifi. Ni muhimu kuangalia kilicho andikwa ndani sio kuangalia jarada la kitabu ambayo kwa nje mengi ni mazuri na yanapendeza kama hatutaangalia matini kwenye uchaguzi wa vitabu tunaweza kupotea, kwani vitabu hivyo vinaupotoshaji mkubwa. Si vibaya watu kusoma vitabu vya kuburudisha wakati wa kupumzika bali tuangalie ni maudhui gani yaliyo ndani yake. Kwa kuwa kuna vitabu vingi vilivyoandikwa hapo kale ni vizuri pia kupenda kusoma vitabu vilivyo-andikwa hivi karibuni ili kujua mambo yanayo-endelea Duniani. Hivyo ni vyema watu kujua kusoma na kuandika, maana hata wakipewa vitabu hawawezi kusoma.

Kielelezo 2.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kutumia baadhi ya kanuni za kufupisha habari na kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache, asilimia 4.4 walipata alama hafifu yaani 0 hadi 3. Kati yao, asilimia 0.7 walipata alama 0 kutokana na kutozingatia taratibu za uandishi na kanuni za ufupisho kama vile; *kuwa na mpangilio wa maneno usio na mantiki, matumizi yasiyo sahihi ya alama na vituo, kupotosha kiini cha habari ya awali, kutozingatia idadi ya maneno* pia *matumizi ya lugha isiyo sanifu*. Kielelezo 2.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa

aliyeshindwa kabisa kufupisha habari aliyopewa na badala yake akatunga habari yenye kichwa cha habari “UTANDAWAZI” ambayo haina uhusiano wowote na habari aliyopewa.

**Kielelezo 2.3**


2: UTANDAWAZI

Utandawazi katika jamii yetu ni jambo zuri kwani huleta maendeleo katika jamii yetu zaidi mwetu. Katika utandawazi kuna mambo mbali mbali ya kujifunza ambayo ni uzeme katika maisha yetu kama vile kujua mambo ya kibiashara, sayansi, na teknolojia. Kupitia kwa utandawazi katika jamii kwa sasa umeanza kuleta mawasiliano kulinganisha na nyakati za nyuma ambapo watu walikuwa ngaiko katika kupata mawasiliano. Katika jamii yetu ya sasa vijana wengi hushindwa kuweza kuchagua mambo yaliyo mema badala yake hufuata mambo mabaya kwa kuona kwamba wanaonda na wakati hali ambayo huweza kuwapelekea kupata matatizo kama vile na kuweza kupoteza maisha yao basi hawana budi kufanya mambo mazuri ili kupata maendeleo.


Kielelezo 2.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufupisha habari aliyopewa kwa kutunga habari isiyokuwa na uhusiano nayo.

## 2.3 SEHEMU B: MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

### 2.3.1 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi

Swali lilihusu mada ya *Matumizi ya Sarufi* na lilimtaka mtahiniwa (a) kueleza maana ya viambishi vya O-rejeshi na (b) kuunganisha sentensi kwa kutumia O-rejeshi. Swali lililenga kupima matumizi na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali lilijibiwa na asilimia 65.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa waliochagua swali hili kilikuwa kizuri sana ambapo asilimia 98.4 walifaulu kwa kiwango cha juu na wastani. Chati Namba 3 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 3**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 94.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 6 hadi 10. Kiwango hiki cha juu kinadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya viambishi vya O – rejeshi. Watahiniwa waliweza kutoa maana ya viambishi vya O – rejeshi na kisha kuunganisha sentensi kwa usahihi kwa kutumia O – rejeshi katika sentensi walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuelezea viambishi vya O – rejeshi kuwa ni *aina ya viambishi ambavyo hurejelea mtenda au mtendwa wa jambo katika sentensi*. Aidha, aliweza kuunganisha sentensi kwa kutumia viambishi vya O – rejeshi. Kielelezo 3.1 kinadhihirisha jibu la mtahiniwa aliyefanya vizuri kwa kufuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 3.1.**

3. (a) Viambishi vya O-rejeshi ni aina ya viambishi ambavyo hurejelea Mtenda au Mtendwa wa jambo katika sentensi. Mfano, Mtoto aliyekamatwa ni mwanangu. Katika sentensi kiambishi cha O-rejeshi ni "aliye"

3 (b) (i) Kanu ameleta mpira wa miguu uliokuwa [illegible]

(ii) Rukia anatafuta vitabu vilivyokwisha.

(iii) Gazeti lililochapwa, limekwisha.


(iv) Mtoto aliyetekwa nyara amepatikana.

(v) Yule msichana aliyesimama pale ni dada yangu.

Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa maana ya viambishi vya O – rejeshi. Hata hivyo, mfano wa kiambishi cha O-rejeshi "*aliye*" alioutoa haukuwa sahihi kwani ulitakiwa kuwa "ye" peke yake.

Aidha, asilimia 4.1 ya watahiniwa walipata alama za wastani yaani 3.5 hadi 5.5 kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza viambishi kuwa *hutumika kukamilisha sentensi ili ilete maana iliyokusudiwa* badala ya kueleza kuwa hutumika katika kumrejelea mtenda/mtendwa wa jambo kama ilivyotakiwa. Hata hivyo, mtahiniwa huyo alimudu kuunganisha sentensi (b) (iii), (iv) na (v) pekee na kupata alama za wastani.


**Kielelezo 3.2**




Kielelezo 3.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeunganisha sentensi kwa usahihi lakini akashindwa kubainisha viambishi vya o – rejeshi kwa kuandika silabi *je* katika kipengele b (i) na (ii) visivyokuwa na uhusiano na viambishi vya O-rejeshi na hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache sana, asilimia 1.6 pekee ndio waliojibu vibaya swali hili na kuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama 0 hadi 3. Watahiniwa hao walishindwa kufafanua dhana ya viambishi vya O – rejeshi na kuunganisha sentensi kwa kutumia O – rejeshi. Katika majibu yao, baadhi ya watahiniwa walichanganya dhana ya O – rejeshi na dhana ya viunganishi ambazo ni aina za maneno. Kielelezo 3.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetumia viunganishi (aina za maneno) ili kuunganisha sentensi alizopewa isivyo badala ya kutumia viambishi vya O - rejeshi.

**Kielelezo 3.3**


3 b (i) Kanu ameleta mpira wa miguu kwani ulikuwa unahitajika mpira.

(ii) Rukia anatafuta vitabu na vitabu vimekwisha.

(iii) Gazeti lilichapwa lakini gazeti limekwisha.

(iv) Mtoto anetikwa nyara ila mtoto amepatikana.


(v) Yule msichana [illegible] pale kumbe yule msichana ni dada yangu.

Kielelezo 3.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kabisa kufafanua dhana ya viambishi vya O – rejeshi na kisha kutumia viunganishi (aina za maneno) kuunganisha sentensi alizopewa kinyume na mahitaji ya swali.

### 2.3.2 Swala la 4: Matumizi ya Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* na lilimtaka mtahiniwa kufafanua kazi mbili za mnyumbuliko na kazi tatu za uambishaji katika lugha ya Kiswahili. Swali lililenga kupima maarifa na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 76.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa ni swali la kuchagua. Asilimia 89.7 ya watahiniwa hao walijibu vizuri na kufaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 4 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 4**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 70.6 walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu 6 hadi 10. Watahiniwa hao waliweza kufafanua kazi mbili za mnyumbuliko katika lugha ya Kiswahili kama vile *kuunda neno jipya na kupanua maana ya neno*. Aidha, walimudu kufafanua pia kazi tatu za uambishaji katika lugha ya Kiswahili kama vile *kuonesha nafsi*, *njeo*, *hali*, *kauli mbalimbali* na nyinginezo kwa usahihi. Kielelezo 4.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua kazi mbalimbali za mnyumbuliko na uambishaji katika lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo 4.1**

4. Mnyumbuliko ni kitendo cha kurefusha neno. Uambishaji ni upachikaji wa viambishi katika mzizi wa neno. Uambishaji unaweza kuhusisha kuweka viambishi awali au tamati. Mnyumbuliko na uambishaji huwa na kazi tofauti katika kiswahili.

Kazi za mnyumbuliko ni pamoja na;

Kuonyesha hali ya kutenda, kutendeana, kutendesha.

Mfano; Piga (Tenda)
Pigania (Kutendea)
Piganiana (Kutendeana).

Kubainisha au kupata aina ya neno au maneno mapya.

Mfano; Mchezo – Mchezaji, hivyo pamoja na mambo mengine hufanya kazi kubwa ya kurefusha maneno.

Kwa upande wa uambishaji, huwa na kazi zifuatazo;

Kuonisha njeo.

Mfano; Watakuja

Wa-ta-kuj-a, "-ta-" ni kiambishi cha njeo, kuonesha wakati ujao.

Kuonesha nafsi.

Mfano; Aliyesema.

A-li-ye-sem-a, "a" ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu umoja.

Kuonesha au kukamilisha maana.

Mfano; Someana

Som-ean-a "a" ni kiambishi tamati maana.


Hivyo, husaidia katika lugha ya kiswahili.

Kielelezo 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kufafanua kazi mbili za mnyumbuliko na kazi tatu za uambishaji katika lugha ya Kiswahili kama ilivyotakiwa.

Asilimia 19.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao walitoa hoja zisizojitosheleza hususan kwa kutoa hoja chache au zisizofafanua vyema dhana husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kazi moja tu ya mnyumbuliko na katika uambishaji hakutoa mifano madhubuti inayodhihirisha kazi za uambishaji. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa

kutoa hoja zisizojitosheleza na kutokutoa mifano madhubuti katika kufafanua kazi mbili za mnyumbuliko na kazi tatu za uambishaji katika lugha ya Kiswahili.


**Kielelezo 4.2**


04. Mnyumbuliko ni kile kitendo cha kuzalisha maneno mengi
kutokana na neno moja Mfano Taifa linakuwa Taifani,
Taifisha, Taifishana au Taifishwa. Vilevile Uambishi
ni kitendo cha kuongeza Mofimu kabla au baada ya mzi
zi wa neno. Kwa mfano Lima inakuwa analima, analimi
wa, Watalimiana, hivyo ndivyo uambisha unaweza kutokea
katika sentensi au neno. Na zifuatazo ni kazi za mnyambuli
ko katika lugha ya Kiswahili nazo ni kama vile:-
Mnyumbuliko hukuza lugha kwa kuongeza idadi ya mi
samiati katika lugha ya Kiswahili. Mfano neno piga linawe
za kunyumbuliwa na kwa na msamiati zaidi ya mmoja kama
vile pigia, pigiana, pigishwa, pigishiwa au pigika ambapo
ndipo msamiati mingi huzaliana na kukuza lugha.
Mnyumbuliko pia hupamba lugha kwa kuongeza msamiati
yenye mvuto katika lugha ya Kiswahili ambayo huwavutia
hata watumiaji wa lugha ya Kiswahili Mfano. neno gonga
linaweza kunyumbuliwa na kuleta maana kama vile gonge
a, gongesha, gongana hata gongeshewa ambapo maneno
kama haya huweza kutumia na vijana ili kupamba
mazungumzo yao. Vilevile zifuatazo ni kazi za Viambishi
katika lugha ya Kiswahili nazo ni kama vile:-
Viambishi au Uambishi huonyesha wingi na umoja
katika lugha ya Kiswahili. Mfano neno Lima linaonyesha
kauli ya kutenda umoja ila linapowekewa viambishi
awali na tamati linaweza kuonyesha wingi kama vile
Wanalima kauli ya kutenda wingi.
Uambishi huonyesha urejeshi wa mtenda, kwa kuong
eza Mofimu kabla ya mzizi wa neno au baada ya mzizi
wa neno urejeshi wa mtenda huonekana kwa Mfano
neno piga linapowekewa Mofimu kati kuonyesha
urejeshi wa mtenda linaweza kuwa pigwa ambapo ni
kauli ya kutendwa.

Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu baadhi ya kazi za mnyumbuliko na uambishaji.

Aidha, asilimia 10.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 3 kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya mnyumbuliko na uambishaji na hivyo kushindwa kufafanua kazi za mnyumbuliko kama *kuunda neno jipya na kupanua maana ya neno*. Pia alifafanua kazi za uambishaji kama *kuonesha nafsi*, *njeo*, *hali*, *kauli mbalimbali* na nyinginezo kama ilivyotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kazi mbili za mnyumbuliko kama vile *kuonesha wakati* na *kuonesha mtendwa* na katika uambishaji akataja kazi kama vile ; *kuonesha kielezi na kupata maana zaidi ya moja* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alishindwa kufafanua kazi mbili za mnyumbuliko na kazi tatu za uambiashaji kama ilivyotakiwa.

**Kielelezo 4.3**


04 Zifuatazo ni kazi za mnyumbuliko kama vile:
Kuonyesha wakati, Hii ni kuwa unaweza kujua ni wakati gani neno limetumika ni lazima kuangalia ni namna linaweza kutumika mfano
Lima, Limiwa hii inaonyesha kuwa ni wakati ulipo
Kuonyesha Mtendwa wa jambo, Pia mnyumbuliko katika maneno huweza kuonyesha namna mtendwa wa jambo linavyofanyika
Mfano Lima, Lomwa, Lomiwa kwa kuwa hii inaonyesha namna mtu anavyofanyiwa
Lakini pia kuna kazi tatu za uambisha katika lugha navyo ni kama ifuatavyo.
Kuonyesha Kielezi, maneno yanapo pachikwa katika kiizizi wa neno yanaonyesha namna au mahali, Sehemu fulani mfano shuleni, kanisani, kwa namna hiyo ni imeweza kuonyesha Sehemu fulani.
Kupata maana zaidi ya moja, maneno au mofimu zinapopachikwa huweza kufanya neno moja kuwa na maana zaidi ya moja
mfano - Lima ni kitendo
- Limao ni nomino


Kielelezo 4.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kabisa kufafanua kazi mbili za mnyumbuliko na

kazi tatu za uambishaji katika lugha ya Kiswahili kama ilivyotakiwa.

### 2.3.3 Swali la 5: Matumizi ya Lugha

Swali lilihusu mada ya *Matumizi ya Lugha* na lilimtaka mtahiniwa kufafanua changamoto anazokabiliana nazo mtumiaji wa lugha ya Kiswahili ambaye ni mahiri wa lugha zingine. Swali lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali lilijibiwa na asilimia 64.9 kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 75.5 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 5 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika swali hili kiasilimia.





**Chati Namba 5**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 64.1 ya watahiniwa walijibu vizuri swali hili na kupata alama za juu 6 hadi 10. Kiwango hiki cha kufaulu kinadhihirisha kuwa mada ndogo ya umahiri katika lugha ilieleweka vizuri kwa watahiniwa. Watahiniwa hao waliweza kutaja na kufafanua vizuri changamoto anazokabiliana nazo mtumiaji wa lugha ya Kiswahili ambaye ni mahiri wa lugha zingine kama vile *msamiati*, *matamshi*, *maana na sarufi* ya lugha ya Kiswahili na lugha zingine anazotumia. Kielelezo 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua changamoto nne anazokabiliana nazo mtumiaji wa lugha ya Kiswahili ambaye ni mahiri wa lugha zaidi ya moja ijapokuwa alitoa mfano wa msamiati ‘bunge’ na

‘ikulu’ isivyo sahihi kwani maneno hayo hayana athari yoyote kwa mtu mahiri wa lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo 5.1**



5 Umahiri wa Lugha; Ni ujuzi wa hali ya
juu wa Lugha katika stadi zake zote nne
yaani, Kusoma, Kuandika, Usikivu na Kuongea.
Ili mtu aweze kuwa mahiri wa Lugha fulani
Lazima ajifunze lugha hiyo, afanye mazoezi
ya kuzungumza Lugha hiyo katika maongezi
yake ya kila siku na vilevile akae karibu na
wajuzi wa Lugha hiyo ili aweze kukosolewa
au kurekebishwa pale anapokosea kutamka lugha
ya Kiswahili ina wamatumiaji wengi Lakini watu
miaji hao wanakumbwa na changamoto nyingi kwa
sababu pia ni wamahiri wa Lugha nyingine
hasa za kibantu na zakigeni kama vile

ya Kiingereza. Zifuatazo ni changamoto kuu nne zinazowakabili watumiaji wa Kiswahili. Kutokana na umahiri walionao wa Lugha nyingine.

Kimatamshi: Hii ni changamoto inayowakumba watumiaji wa Kiswahili ambaye ni mmahiri wa Lugha nyingine hasa za Kibantu kwani kutokana na athari za Lugha hizo hujikuta akichanganya Matamshi ya maneno mbalimbali. Mfano. Wakurya hutumia r badala ya l katika Lugha ya Kiswahili kama vile rara, Angaria, wanyakyusa hutumia ~~v~~ fya bdala ya vy- kama fyakula badala ya viafu.

Kimsamiati: Pia watumiaji wa Lugha ya Kiswahili ambaye ni mahiri wa Lugha nyingine hujikuta wakichanganya misamiati ambayo ipo katika Lugha zao na pia kwenye Kiswahili bila kujua kama inatofautiana kimaana. Mfano wa misamiati hiyo ni Bunge ambao katika Lugha ya Kisambaa ina maana ya kikao, Ikulu katika Kisukuma na Kigogo.

Kimaana: Pia hii ni changamoto nyingine inayomkumba mtumiaji wa Kiswahili ambaye ni mahiri wa Lugha nyingine kwani kuna baadhi ya misamiati inayotumika katika Kiswahili na Lugha nyingine hasa za Kibantu Lakini ina Maana tofauti Mfano neno "Jana" katika Lugha ya Kiswahili Lina maana ya siku moja iliyopita lakini kwa wasukuma Lina maana ya siku inayofuata ~~v~~ yaani "Kesho" Mfano Baba mtakuja Jana hivyo kutokana na maneno kama hayo watu hao hujikuta wakiyaelewa na kuyatumia maneno yao katika Lugha ya Kiswahili kama yanavyo maanisha katika Lugha ~~zao~~. yao.


05 Kisanifi; Pia Mtumiaji wa kiswahili
ambaye ni mahiri wa Lugha nyingine anakumbwa
na changamoto za Kisanifi kwani Kila Lugha in
a kanuni na taratibu zake hivyo mtu akiwa
mmahiri wa Lugha zaidi ya moja huchanganya
sanifi za Lugha hizo. Mfano katika Lugha za
Kibantu kama vile ~~Kikuu~~ ya Kifipa sanifiyake huru
mia umbo la wingi ili kuonyesha heshima kwa
wakubwa ~~Mfano~~. ~~Baba~~ mt: hivyo kutokana na hali
hiyo mfipa anapotumia Kiswahihi hu ~~w~~katena umbo
la wingi kitu ambacho huathiri ~~mto~~ sanifi ya Kiswahi
li. Mfano wababa mtakuja lini?.badala ya Baba
utakuja lini?.
Hivyo basi ili kuepuka changamoto hizo
mtumiaji hana budi kujifunza na kuwa makin
i na kanuni na taratibu za Lugha zote na
pia alewe Msamiati mbalimbali na aweze kuta
fautisha maana zaka katika Kila Lugha.

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetaja changamoto nne muhimu ambazo humkabili mtumiaji wa lugha ya Kiswahili ambaye ni mahiri katika kutumia lugha zingine, japokuwa jibu lake lina dosari za kiundishi ambapo katika aya ya tatu alindika *kibant-* badala ya kibantu na *kiswahihi* (aya ya 5) badala ya Kiswahili.

Watahiniwa wachache, asilimia 13.4 walijibu swali hili na kupata alama za wastani yaani 3.5 hadi 5.5 kwa kuwa walitoa hoja zisizotosheleza matakwa ya swali. Wengine walitaja changamoto chache zilizo sahihi na zingine zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja changamoto mojawapo kuwa ni '*kurudia maneno*' hoja ambayo sio sahihi. Kielelezo 5.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja pungufu na nyingine zisizo sahihi.

**Kielelezo 5.2**

5 Mahili wa lugha ni mtu yeyote, mwenye ujuzi wa hali ya juu wa lugha katika stadi nne ambazo kusoma, kuandika, kuzungumza na kusikiliza. Mtu ambaye ni mahili wa lugha mbili au zaidi anakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Tatizo katika matamshi. Mtu aliye mahili wa lugha mbili au zaidi mwisho wake huweza kuchanganya matamshi ya lugha moja na nyingine mfano

| Kiswahili | Kikutya |
|---|---|
| lala | rara |
| Neno | Matamshi |
| lala | rara |
| viatu | fyiatu |

Kutokana na hali hii mtu aliye mahili wa kikuria hili na kilugha mfano wakurya "l" hutamka "r" na wanyakyusa "v" wanatamka "fy".

Tatizo la msamiati. Mtu aliye mahili wa lugha zaidi ya moja anaweza kuchanganya msamiati. Kwa mfano mahili wa lugha ya kiswahili na kiingereza huweza kuchanganya msamiati wa kiingereza na kiswahili kwa mfano

"Nitakuinform nikifika school"

"Anatakiwa kupewa demotion"

Badala ya "Nitakujulisha nikifika shuleni"

"Anatakiwa kushushwa cheo"

Tatizo la kurudia maneno. Mtu aliye mahili wa kiingereza na kiswahili anaweza kuchanganya kwa kurudia maneno yaleyale katika uongeaji wake kwa mfano

"Nimefika barabara ya Nyerere road"

Kielelezo 5.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika "kurudia maneno" kama changamoto inayomkabili mmahiri wa lugha, hoja isiyo sahihi na kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 22.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walipata alama hafifu 0 hadi 3 kwa kuwa walikosa maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu mmahiri wa lugha zaidi ya moja ikiwemo lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja baadhi ya changamoto kuwa ni '*kutotumia lugha hiyo kwa mazingira ya kila siku, kutosoma lugha hiyo kwa kiwango cha juu, kutokuwa*

*karibu na wajuzi wa lugha hiyo na ukasumba*.’ Kielelezo 5.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kabisa kubainisha changamoto zinazomkabili mahiri wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine.

**Kielelezo 5.3**

05 Umahiri ~~ki~~ Ni kile kitendo cha mtu-kujua au kuwa na ujuzi mpana katika stadi zote nne za lugha. Mfano, kusoma, kusikiliza, kuandika na kuzungumza. Mtu anapokuwa mahiri wa lugha huwa anakabiliwa na - changamoto nyingi pale anapokuwa anatoa - kazi yake.


Yafuatayo ni changamoto za umahiri wa zinazomkabili mahiri wa lugha anapofanya kazi yake ya umahiri

Kutotumia lugha hiyo kwa Mazingira ya kila siku; Mtu anapokuwa mahiri wa - lugha moja au nyingi anashindwa pale ambapo anaweza kuitumia lugha hiyo ni pale tu pa-kufanyia kazi, lakini anapokuwa sehemu - nyingine anakuwa anatumia lugha nyingine - hiyo inamfanya mtu huyo kuwa mahiri mzuri katika lugha.

Kutosoma lugha hiyo kwa kiwango cha ~~juu~~ juu; Mtu anapokuwa mahiri wa lugha fulani ni lazima awe amesoma lugha hiyo kwa kiwango cha juu. Endapo hajasoma - Lugha hiyo kwa kiwango cha juu itampelekea kushindwa kufanya kazi yake ya umahiri vizuri.

Kutokuwa karibu na wajuzi wa lugha hiyo; Endapo mahiri asipokuwa karibu na wajuzi wa lugha hiyo, ita kuwa ni vigumu mtu huyo kutoa au kufanya kazi yake vizuri kwa kuwa karibu na wajuzi itam-fanya kuwa vizuri katika suala la umahiri.

Kutokuwa karibu na wajuzi wa lugha, ni-changamoto inayomfanya mahiri, kushindwa




kufanya kazi vizuri kwa anakuwa anajifunza
lugha mbili kwa wakati mmoja, hivyo kushi-
ndwa kufanya vizuri.
Ukasumba; Mahiri anapokuwa -
anajua lugha zaidi ya mbili inakuwa ni -
shida kwani anakuwa anachanganya maneno
ata mfano: kiswahili na kiingereza hivyo basi
anapokuwa kuchanganya kwa maneno -
kumpelekea kushindwa kufanya kazi yake
kwa ya umahiri vizuri.
Hivyo basi, kutokana na changamoto
hizi, Mahiri wa lugha inampasa kusoma -
lugha hiyo kwa kiwango cha juu, na kuwa -
karibu na wazawa wa lugha husika.

Kielelezo 5.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye alifafanua hoja zisizo sahihi kuhusu changamoto zinazomkabili mmahiri wa lugha ya Kiswahili na lugha nyingine kinyume na matakwa ya swali.

### 2.3.4 Swali la 6: Matumizi ya Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* na lilimtaka mtahiniwa kubainisha matumizi ya mofimu ‘ki’ iliyopigiwa mstari katika sentensi alizopewa. Swali lililenga kupima matumizi na lilikuwa na jumla ya alama 10.


Swali hili lilijibiwa na asilimia 45.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani na kulifanya kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wachache. Asilimia 68.8 ya watahiniwa hao walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Namba 6 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 6**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 32.7 ya watahiniwa hao walijibu swali vizuri na kupata alama za juu yaani 6 hadi 10, kwa kuwa walimudu kubainisha matumizi ya mofimu ‘ki’ kwa usahihi kama ilivyotumika katika sentensi walizopewa. Aidha, watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya mofimu kwa jumla. Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyebainisha matumizi ya mofimu ‘‘ki’’ kwa baadhi ya sentensi kwa usahihi.

**Kielelezo 6.1**



6 i) kuonyesha Upatanisho wa kisarufi, Ngeli ya KI-VI
ii) kuonyesha Masharti
iii) kuonyesha Upatanisho wa kisarufi, Ngeli ya ki-vi
iv) kuonyesha kitenzi kishirikishi (ushirikishi)
v) kuonyesha Urejeshi wa kitendwa
vi) kuonyesha wakati (wakati Uliopo).
vii) Huwakilisha Mtendi
viii) kuonyesha Udogoshi
ix) kuonyesha namna au jinsi
x) kuonyesha namna au jinsi

Kielelezo 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye alibainisha matumizi ya maofimu ‘ki’ kwa baadhi ya sentensi zilizoorodheshwa kwa usahihi.

Baadhi ya watahiniwa, asilimia 36.1 walipata alama za wastani 3.5 hadi 5.5 kwa kuwa walimudu kubaini matumizi ya ‘ki’ kwa

baadhi ya vipengele na kushindwa kuyabaini katika vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu kipengele cha 6 (ix) *Aliruka juu <u>ki</u>huni*, mtahiniwa huyo alibainisha ‘ki’ kama *kihusishi* badala ya kielezi ambalo ndilo jibu sahihi. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kupata alama za wastani.


**Kielelezo 6.2**

06
i). Kiti kidogo
⇒ Ina Maanisha (bainisha) udogo wa kitu au udogodishaji wa kiti.
⇒ Inabainisha upatanisho wa kisarufi.
ii). Akija apewe mzigo wake.
⇒ Inabainisha hali ya Masharti.
iii) Kitabu kimechanika
⇒ Inabainisha ngeli ya KI-VI ambayo ni ngeli ya tatu
iv). Kiti ki kidogo
⇒ Inabainisha ushirikishi au hali ya ushirikishi.
v). Wanakisubiria. au kauli
⇒ Inabainisha hali, ya kitendea
vi) Analima akiimba
⇒ Inabainisha uhusishaji (kihusishi).
vii) Ataruma alichokipanda
⇒ Inabainisha utendaji
viii) Kitoto kiki sikinenzi.
⇒ Inabainisha udogo ambapo inaonesha hali ya kudharau.
ix) Aliruka juu kihuni
⇒ Inabainisha kihusishi
06 x) Anachezea kidoto
⇒ Inabainisha hali ya kudunishwa kwa Mtu au kuonyesha badhi..

Kielelezo 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele (v),(vi),(vii),(ix) na (x) na kubainisha matumizi ya mofimu ‘ki’ kwa usahihi katika vipengele vingine.

Watahiniwa wengine, asilimia 31.2 walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi na kupata alama hafifu yaani 0 hadi 3. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 1.8 walipata alama 0 kutokana na kubainisha matumizi ya ‘ki’ yasiyo sahihi. Watahiniwa hawa walionesha kukosa uelewa wa dhana ya mofimu kwa ujumla na hivyo kushindwa kabisa kubaini mofimu ‘ki’ kama zilivyotumika katika sentensi husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika matumizi ya ‘ki’ kama (i) Kiti kidogo akaandika ‘kudogosha’ badala ya ‘*kiambishi cha umoja/upatanisho wa kisarufi* (ii) Akija apewe mzigo wake akaandika ‘*kutoa taarifa ya mtu fulani*’ badala ya *masharti/njeo* majibu ambayo hayakuwa sahihi. Kielelezo 6.3 kinadhihirisha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubaini matumizi ya mofimu ‘ki’ kama ilivyotumika katika sentensi alizopewa.

**Kielelezo 6.3**


6 (i) Ki- Imetumika kuonyesha udogo wa kitu (kudogosha)
(ii) Ki- Imetumika kutoa taarifa ya Mtu fulani kutendewa jambo fulani
(iii) Ki- Imetumika kutoa taarifa ya kitu kilichofanyiwa kitu kilichotendeka
(iv) Ki- Kuonyesha hali ya kitu
(v) Ki- Kuonyesha hali ya watu kungojea kitu
(vi) Ki- Kuonyesha jambo linalotendwa Au kutoa taarifa ya jambo kutendeka.
6. (vii) Ki- Kuonyesha hali ya jambo linalongojewa kutendeka
(viii) Ki- Imetumika kuonyesha udogo wa kitu kudogosha
(ix) Ki- Kuonyesha jambo lililofanywa na mtenda


Kielelezo 6.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye alishindwa kueleza matumizi ya mofimu ‘ki’ kama ilivyotumika katika sentensi badala yake alitoa majibu anuwai yasiyokidhi matakwa ya swali kwa vipengele vingi.

## 2.4 SEHEMU C: UTUNGAJI

### 2.4.1 Swali la 7: Uandishi wa Kadi za Mialiko

Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji* na mada ndogo ya Uandishi wa Kadi za Mialiko. Swali lilimtaka mtahiniwa (a) kutaja na kueleza mambo saba ya kuzingatia wakati wa kuandika kadi ya mwaliko na (b) kuandika kadi ya mwaliko kwa kuzingatia taratibu za uandishi. Swali lililenga kupima uundaji na na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali lilijibiwa na asilimia 99.9 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa ni swali la lazima. Swali hili lilijibiwa vizuri zaidi na watahiniwa wengi ikilinganishwa na maswali mengine katika mtihani huu ambapo asilimia 98.9 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 7 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika swali hili kiasilimia.




**Chati Namba 7**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia


Swali hili ndilo lililojibiwa vizuri zaidi ya maswali yote katika karatasi ya mtihani huu. Asilimia 87.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu ambazo ni 12 hadi 20. Watahiniwa hao waliweza kutaja na kueleza mambo saba ya kuzingatia wakati wa kuandika kadi za mwaliko kama vile, *jina la mwandishi* na *anuani yake*, *jina la mwandikiwa*, *lengo la mwaliko*, *tarehe ya mwaliko*, *mahali pa mwaliko/eneo/sehemu*, *muda wa tukio* na *taarifa ama mawasiliano*.

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutaja na kuelezea mambo stahiki katika uandishi wa kadi ya mwaliko na kuandika kadi iliyokidhi vigezo vyote vya uandishi wa kadi za mwaliko.

**Kielelezo 7.1**

7a Kadi ya mwaliko ni taarifa ama ujumbe unaotolewa na mtu ili kumwalika ama kuwaalika ndugu, jamaa na marafiki katika sherehe ama tafrija fulani. Yafuatayo ni mambo muhimu saba ya kuzingatia katika uandishi wa kadi ya mwaliko.

Jambo la kwanza ni jina la mwandishi na anwani yake kama ipo. Mwandishi anatakiwa kuandika jina lake ili kumtambulisha ama kuwatambulisha wale anaowaalika katika tafrija ama sherehe yake ili wajue mwaliko umetoka kwa nani.



7(a) Pili ni jina la mwandikiwa. Mwandishi wa kadi ya mwaliko lazima aandike mtu ama jina la mtu anayemwandikia ili iwe rahisi kumfikia huyo mtu.


Lengo la mwaliko. Mwandishi wa kadi ya mwaliko lazima aandike lengo la kualika mfano: kualikwa katika sherehe ya kumpongeza mtoto ama siku ya kuzaliwa. Hii itamsaidia mualikwa kujua lengo la mwaliko.

Tarehe ya mwaliko. Mwalikaji anatakiwa kuandika tarehe ya mwaliko, hii humsaidia mwalikwa kujua tarehe tukio litakapofanyika na kufanya maandalizi ya kutosha.

Mahali pa mwaliko/eneo/sehemu. Mwandishi/mwalikaji anatakiwa aeleze wazi eneo ambapo tukio litafanyika ili kurahisisha kazi. Hii humsaidia mualikwa kujua sehemu ama mahali sherehe zitakakofanyika.

Muda wa kufika, mwalikaji lazima ataje muda wa kufika katika mwaliko. Hii husaidia waalikwa kufika kwa wakati katika eneo la tukio.

Taarifa ama mawasiliano kwa waliaalikwa. Kadi ya mwaliko inatakiwa kuwa na mawasiliano ama taarifa kwa



7 b) Familia ya SIKUTEGEMEA KIZITO
Inayofuraha kubwa kukualika / Kuwaalika
Bw/Bi/Mb/Pr/Mwl/Dkt/Shk/
NDUGU, JAMAA NA MARAFIKI
Katika sherehe ya kumpongeza kijana wao mpendwa
SIKUJUA KIZITO
Kwa kuhitimu kidato cha sita itakayofanyika tar: 7/6/2017
nyumbani kwake mtaa wa Majengo saa 9:00 alasiri.
Kufika kwako ndio mafanikio ya sherehe.
Mawasiliano: 0714 - 378 368
MZEE KIZITO.

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetaja na kueleza kwa usahihi mambo ya kuzingatia katika

kuandika kadi ya mwaliko na kisha kuandika kadi ya mwaliko iliyozingatia vigezo na taratibu za uandishi kama ilivyotakiwa.

Watahiniwa wachache asilimia 11.9 waliojibu swali hili walipata alama za wastani 7 hadi 11.5. Watahiniwa hao walikuwa na mapungufu katika majibu yao kama vile kuorodhesha baadhi tu ya mambo ya kuzingatia katika uandishi wa kadi ya mwaliko na wengine kushindwa kuelezea kwa usahihi vigezo hivyo vya uandishi wa kadi husika. Aidha, watahiniwa wengine waliweza kuandika kadi ya mwaliko kwa kuzingatia baadhi ya vigezo sahihi vya uandishi wa kadi ya mwaliko kama vile *jina la mwalikwa, tarehe, mtu wa kurudishiwa majibu, muda wa mahafali bila kufafanua lengo la mwaliko na kuacha baadhi ya vigezo vingine muhimu na* hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 7.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hakuorodhesha baadhi ya mambo muhimu katika uandishi wa kadi ya mwaliko na kuandika kadi ya mwaliko isiyojitosheleza.

**Kielelezo 7.2**

7.b Familia ya Bwana na bibi Sikutegemea Iya
kizito wa Dar-es-salaam (Tabata)
wanayo furaha kukualika / kumualika
Ndugu, Bi & Bw, Miss, Mrs, Mch
Abbas Mkwetu
katika tafrija fupi ya kubatizwa
kwa mtoto wao mpendwa
Sikutegemea kizito
Itakayofanyika tarehe 07/06/2017 katika ukumbi
wa Mt. Agness mwenge Dar-es-salaam
kuanzia saa 12:30 jioni
Kufika kwako ndio mafanikio
ya sherehe hii
Tafadhari fika na kadi hii
kwa mawasiliano zaidi
0714671123 - Baba sikutegemea
0688111141 - Mama sikutegemea


· Utangulizi / utambulisho
7.a Salamu za mwaliko; kwa familia au mtu anayetoa mwaliko anaonesha hisia zake kwa yule anaowaalika kwa kujitambulisha.
Jina / cheo cha mwalikwa
hapa kunaoneshwa jina la mwalikwa kwa kuonesha cheo alichonacho kwa mfano, Ndugu, Bwana na bibi, Mchungaji
Aina ya sherehe
Pia kadi inatakiwa kutaja ni aina gani ya sherehe itakayotokea mfano. harusi

Jina la mhusika
yaani anatajwa mhusika anayefanyiwa sherehe au tafrija hiyo. kwa mfano ya mtoto wao mpendwa Agness kimaunya
Mahali au sehemu tukio
hilo litakapofanyika kama ni ukumbini nyumbani na ni maeneo gani kadi inatakiwa kueleza
7a Muda na tarehe
Yaani tukio hilo litafanyika wakati gani, ili mgeni mwalikwa aweze kujua atafika muda gani kwa mfano
"Shughuli itafanyika kuanzia saa 12:30 jioni" na tarehe ngapi
Mawasiliano
kwa kuweka namba za simu, anuani E-mail ili kuweza kupata maelezo zaidi juu ya mwaliko huo.

Kielelezo 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya kipengele (a) cha swali na kushindwa kukidhi matakwa ya kipengele (b) yaani kuandika kadi ya mwaliko.

Aidha, asilimia ndogo sana, asilimia 1.1 ya watahiniwa ndio waliofaulu kwa kiwango hafifu cha ufaulu yaani alama 0 hadi 6.5. Watahiniwa hao hawakuweza kujibu swali hili kama ilivyotakiwa kutokana na kukosa maarifa ya kutosha katika uandishi wa kadi za mwaliko. Watahiniwa hao walishindwa pia kutaja na kuelezea mambo saba ya kuzingatia katika uandishi wa kadi za mwaliko kama vile jina la mwandishi, mwandikiwa, lengo, tarehe na mengineyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika barua ya kikazi badala ya kuandika kadi ya mwaliko. Kielelezo 7.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuandika vigezo saba vya kuzingatia katika uandishi wa kadi ya mwaliko, badala yake aliandika barua rasmi ya mwaliko kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 7.3**


7b.

Sikutegemea Kizidu.
P.O BOX 507,
Shaurimoyo.
Zanzibar.

4/5/2017.

NDUGU, JAMAA NA MARAFIKI.
P.O BOX 503,
Bagamoyo,
Tanzania

Ndugu,

KUH: SHEREHE YA KUMPONGEZA MTOTO WANGU ANAYEHITIMU KIDATO CHA SITA 2017.

Kwa uwingi wa heshima

Tafadhali husika na mada iliyopo hapo juu.

Mimi Bi Sikutegemea Kizidu ninaifuraha kubwa ya kukualika

Ndugu, marafiki na jamaa wote katika sherehe ya mtoto wangu kipenzi

Sikuyua Kizidu.

Katika sherehe yake ya kuhitimu kidato cha sita katika shule ya Kikukotoni Sekondari Skuli mwaka 2017. Ambapo sherehe hiyo itafanyika mnamo tarehe 7/6/2017 katika ukumbi wa Buawani saa 10.00 jioni. Kufika kwako ndio kufanikisha sherehe ya mtoto wangu. Watoto tunawapenda lakini wakae nyumbani.

Ahsante.

Wako mzazi mpenzi


Kielelezo 7.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika barua rasmi ya mwaliko badala ya kadi ya mwaliko kama ilivyotakiwa.

## 2.5 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI

### 2.5.1 Swali la 8: Kuenea kwa Kiswahili wakati wa Ukoloni

Swali lilihusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* katika mada ndogo ya *Kuenea na Kukua kwa Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni.* Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza namna Waingereza na Waarabu walivyodumaza maendeleo ya Kiswahili wakati wa ukoloni nchini Tanzania. Swali lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 63.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi. Miongoni mwao, asilimia 90.2 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kutokana na majibu yao kukidhi haja ya swali kwa kiasi kikubwa. Chati Namba 8 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.





**Chati Namba 8**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 53.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha juu na kupata alama 12 hadi 20. Miongoni mwao, asilimia 13.0 walijibu swali hili vizuri zaidi na kupata alama 15 hadi 20. Watahiniwa hao waliweza kueleza namna Waingereza na Waarabu walivyodumaza maendeleo ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua jinsi Waingereza walivyodumaza Kiswahili kama vile ‘‘*kusanifisha Kiswahili bila kuwashirikisha wazawa, Kiswahili kutokutumika katika ngazi za*

*juu za utawala*'' na kwa upande wa Waarabu alielezea ''*shughuli za kidini zilivyotumia lugha ya Kiarabu pekee*, *vitabu vya kidini kutokutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili* na *kutotumia Kiswahili katika biashara au kukitumia Kiswahili kwa kiasi kidogo sana ikilinganishwa na kiarabu''* hoja ambazo ni sahihi. Kielelezo 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefafanua kwa usahihi jinsi Waingereza na Waarabu walivyodumaza Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni.

**Kielelezo 8.1**

8 Maendeleo ya Kiswahili enzi za ukoloni nchini
Tanzania yalidumazwa na mambo mengi ambayo
Waingereza na Waarabu wanamna yao walivyo
changia katika kudumaza lugha ya Kiswahili
Kipindi cha utawala wao.
Waingereza walichangia kudumaza Kiswahili
enzi za utawala wao kama ifuatavyo
Walisanifisha Kiswahili kwa bila kushirikisha
Wazawa. hivyo ikapelekea kusanifishe Kiswahili
kwa kutumia Sarufi ya Kiingereza. kutoshirikishwa
kwa wazawo kwenye usanifishaji wa Kiswahili
kulidumaza Kiswahili ambapo Kiswahili kilitumia
kanuni za sarufi ya Kiingereza
Vilevile Kiswahili hakikutumika katika
ngazi za juu za utawala. Waingereza walitumia
Kiswahili kwenye ngazi ndogo za utawala lakini
hawakukitumia kwenye ngazi za juu za utawala.
hivyo ilipelekea Kiswahili kuonekana ni lugha ya
watu wa chini
Pia katika elimu Kiswahili hakikutumika
katika ngazi za juu za elimu ambapo ngazi za
chini za elimu Kiswahili ndio kilitumika hivyo
ilipelekea kudumaa kwa Kiswahili kipindi
cha ukoloni.
Walikidharau Kiswahili na kutokutilia
Maanani lugha ya Kiswahili ambapo walikiona
Kiswahili kama ni lugha ya watu wa chini
hivyo walichangia kwa kiasi kikubwa kudumazaa
Kiswahili
Pia Waarabu walichangia katika
kudumaza Kiswahili kama ifuatavyo
Shughuli za kidini zilitumia lugha ya –



8. Kiarabu hivyo kupelekea kudumaa kwa lugha ya Kiswahili. waarabu katika shughuli zao ~~za~~ kueneza dini walitumia Kiaarabu hivyo kupelekea kudumaa kwa lugha ya Kiswahili
Pia Waarabu hawakufanya mbinu zozote katika kusanifisha lugha ya Kiswahili Waarabu hawakuchukua mbinu ~~za~~ zozote katika kusanifisha lugha ya Kiswahili hivyo walikidumaza kwa namna moja ama nyingine .
Vitabu vya kidini havikutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Vitabu vya kidini walivyotumia waarabu vilandikwa kwa lugha ya kiarabu pia hawakuweza kuvitafsiri kwenda katika lugha ya Kiswahili hivyo ilipelekea kudumaa kwa lugha ya Kiswahili .
Pio kwenye biashara; ~~Kisw~~ Kiswahili kilitumika kidogo sana ukilinganisha na Kiarabu hivyo ilipelekea kudumaa kwa lugha ya Kiswahili enzi zo ukoloni. pia Matumizi ya Kiswahili yalikuwa machache sana hivyo kupelekea kudimaa kwake.
Waarabu na waingereza pamoja na kuambo wamechangia kwa namna moja ama nyingine katika kudumaza kiswahili vilevile wamesaidia sana katika kukikuza kiswahili nchini Tanzania. ambapo Waingereza walisaidia katika kukisanifisha Kiswahili

Kielelezo 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeelezea jinsi Waingereza na Waarabu walivyodumaza maendeleo ya Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni.

Watahiniwa wengine, asilimia 36.5 walipata alama za wastani 7 hadi 11.5 kutokana na kuelezea hoja zinazopwaya katika kueleza jinsi Waingereza na Waarabu walivyodumaza maendeleo ya Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni. Watahiniwa hao katika majibu yao walitoa hoja na kushindwa kuzifafanua kikamilifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja hoja kama *uhaba wa fedha*, hoja ambayo si sahihi. Aidha, mtahiniwa huyo alikuwa na tatizo la kitahajia na matumizi yasiyo sahihi ya alama za uandishi. Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye hoja zake nyingi hazikujitosheleza na kutotumia alama za uandishi na tahajia ipasavyo.

**Kielelezo 8.2**

$ Maendeleo ya kiswahili nchini Tanzania, ni kukua na kuongezeka kwa msamiati na kuenea au kuongezeka ~~w~~ kwa watumiaji. katika utawala wa waingereza na waarabu waliweza kuchangia katika maendeleo ya kiswahili Tanzania kwa kutumia njia mbalimbali kama vile biashara, elimu, utawala, dini na hata kuimarisha pia waliweza kukidumaza kiswahili nchini Tanzania. Zifuatazo ni hoja au njia ambazo walizitumia wa ingereza katika kudumaza maendeleo ya

$ ya kiswahili nchini Tanzania.

Waingereza walisanifisha kiunguja kuwa lugha ya kiswahili bila kuwashirikisha wenyeji, hii ni moja ya sababu ambayo waingereza iliwapeleka kudumaza maendeleo ya kiswahili nchini Tanzania kwa sababu waingereza hawakuangalia mtindo wa lugha ya kibantu. Hivyo ikapelekea watu kudharau lugha ya kiswahili.

Waingereza walitumia ~~nausun~~ mtindo wa lugha ya Kiingereza katika lugha ya usanifishaji, pia katika harakati za kusanifisha lugha waingereza walitumia kwa kiasi kikubwa mtindo wa lugha ya Kiingereza katika lugha ya kiunguja hii ikapelekea baadhi ya maneno kutokutamkika vizuri. kwa maana jinsi yanavyotamkwa na kuandikwa ni tofauti mfano inzi, ng'e na mbwa. Hii ikapelekea kudumaa kwa lugha.

Waingereza walipuuza matumizi ya lugha ya kiingereza zaidi kuliko Kiswahili katika elimu na utawala, pia katika utawala wa kiingereza waliweza kuruhusu ~~kiswahili~~ kiingereza kitumike zaidi katika elimu hasa ya sekondari kwa sababu katika masomo ya sekondari yote hutumia lugha ya kiingereza. hii ikapelekea kudumaa kwa lugha ya kiswahili nchini Tanzania.

Uhaba wa fedha, pia waingereza wali kuwa na tatizo la fedha ambalo lilipeleke

8 kuhindwa kuchapisha machapisho mbali mbali yaliyoandikwa kwa lugha ya kiswahili hivyo watu wakashindwa kuijua lugha ya kiswahili. Ifuatayo ni namna Waarabu walivyodumaza maendeleo ya lugha ya kiswahili nchini Tanzania.

Waarabu waliingiza msamiati wao katika lugha ya kiswahili, pia hii ni njia ambayo waarabu walitumia kudumaza kiswahili kwa sababu kunabaadhi ya msamiati ya kiarabu ipo katika lugha ya kiswahili, jambo lililopelekea watu kushindwa kutamka maneno haya mfano shekh khatibu. hii ikapelekea kudumaza lugha ya kiswahili.

Waarabu walikihusisha kiswahili na dini, pia hii ilipelekea kudumaza maendeleo ya kiswahili nchini Tanzania kwa sababu kuna wengi ambao hawakuipenda dini ya kiislamu ambayo ililetwa na waarabu. hivyo watu wengi hawakutaka kutumia lugha ya kiswahili wakijua ni lugha ya kiislamu. Hivyo hii ikapelekea kudumaza kiswahili nchini Tanzania.

Waarabu walitumia lugha ya kiarabu katika shule za madrasa, pia katika kufundisha elimu ya madrasa waarabu walitumia sana lugha ya kiarabu kuliko kiswahili hii ikapelekea watu wengi hasa watoto kujua sana kiarabu kuliko lugha ya ya kiswahili. Hivyo hii ikapelekea kudumaa kwa kiswahili nchini Tanzania.

Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa lisilojitosheza na lenye matumizi ya misamiati isiyo sahihi kwa kiwango kikubwa; kwa mfano, ‘*ikapelekea*’ badala ya ‘*ikasababisha*’ na hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa wachache, asilimia 9.8 pekee, ndio waliopata alama hafifu yaani 0 hadi 6.5 kutokana na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali. Baadhi ya watahiniwa hao walieleza mambo yaliyosaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili wakati wa Waingereza kama vile ‘*shughuli za manamba, shughuli za kielimu na usanifishaji*.’ Kwa upande wa Waarabu walitaja : shughuli za *kueneza dini, shughuli za kibiashara, ndoa* na

*utawala* zilivyochangia katika kukuza Kiswahili badala ya kueleza ni jinsi gani Waingereza na Waarabu walivyojihusisha na shughuli hizo katika kudumaza maendeleo ya Kiswahili wakati wa ukoloni nchini Tanzania. Kielelezo 8.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu tofauti na matakwa ya swali kwa kufafanua jinsi Waingereza na Waarabu walivyojishughulisha na na ukuzaji wa Kiswahili nchini Tanzania badala ya kuelezea ni jinsi gani walivyodumaza lugha ya Kiswahili wakati wa ukoloni.

**Kielelezo 8.3**

8 Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na ~~tu~~ watu wanaoishi kusini mwa jangwa la sahara na lugha zao hufanana sana kimsamiati matamshi, maumbo na miundo ya sentensi. Ni lugha ambayo inatumiwa sana nchini Tanzania si kweli kuwa Waingereza na Waarabu walidumaza kiswahili wakati wa ukoloni nchini Tanzania kwani walichangia katika kukikuza na kukiendeleza.

Ufuatao ni mchango wa Waingereza katika maendeleo ya kiswahili

Shughuli za Utawala; katika shughuli za kiutawala waingereza walihimiza kila mtu anayetaka kufanya kazi katika serikali ya mwingereza lazima awe anajua vizuri kiswahili hivyo ikapelekea watu kujifunza kiswahili ili waweze kuajiriwa katika serikali ya mwingereza.

Shughuli za manamba; katika shughuli za manamba waingereza walihimiza kila Akida ajifunze kiswahili ili aweze kuwasiliana vyema na wenzake.

Shughuli za elimu; katika kutolea elimu walisisitiza sana matumizi ya kiswahili ikiwa ni pamoja na kuanzisha shule mbalimbali kama vile Tabora boys na Mpwapwa ili waweze kuimarisha utawala wao. Hivyo walijikuta wakikuza na kuendeleza kiswahili.

Usanifishaji; mwingereza ndiye aliyefanya kazi ya kusanifisha lugha ya kiswahili nchini na kukifanya kizidi kukua.

8 Ufuatao ni mchango wa Waarabu katika kukuza na kuendeleza lugha ya kiswahili.

Shughuli za kueneza dini; katika kufundishia dini ya kiislamu waarabu walitumia lugha ya kiswahili. Hata mahubiri yalitolewa kwa lugha ya kiswahili hivyo wali jikuta wakikuza na kuendeleza kiswahili.

Shughuli za biashara; waarabu walipofika Afrika mashariki walianza kufanya biashara na wenyeji wa Afrika na katika biashara zao walitumia lugha ya kiswahili hivyo kiswahili kilikuwa na kuenea.

Ndoa; waarabu walipoingia Afrika walijikuta wakioa mabinti wa kiafrika kwani walikaa kwa muda mrefu. Walitumia kiswahili kama lugha yao ya mawasiliano hivyo kupelekea kiswahili kukua na kuenea.

Utawala; katika utawala wa waarabu walitumia lugha ya kiswahili katika shughuli zao zote za kutawala, hivyo kupelekea kiswahili kukua na kuenea.

Pamoja na kwamba Waingereza na Waarabu walijitahidi sana katika kukuza na kueneza lugha ya kiswahili lakini bado inakumbwa na changamoto nyingi kama vile uhaba wa wataalamu, uhaba wa fedha kwa ajili ya kuandaa machapisho mbalimbali pamoja na upinzani kutoka katika lugha za kigeni.


Kielelezo 8.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza mambo yaliyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi ya Waingereza na Waarabu kinyume na matakwa ya swali.

### 2.5.2 Swali la 9: Kukua na Kuenea kwa Kiswahili

Swali lilihusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* katika mada ndogo ya *Kukua na Kuenea kwa Kiswahili kabla na baada ya Uhuru*. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kazi tatu za BAKITA na kazi tatu za UKUTA katika kukuza na kueneza Kiswahili.

Swali lililenga kupima uchambuzi na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 36.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 74.9 walijibu swali hili vizuri na kufaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 9 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia




**Chati Namba 9**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 29.3 ya watahiniwa hao waliweza kueleza kwa usahihi kuhusu kazi za BAKITA na UKUTA katika juhudi za kukuza na kueneza Kiswahili na hivyo kupata alama 12 hadi 19. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza kwa usahihi kazi za BAKITA na UKUTA na kutoa hoja tatu kwa kila asasi kama vile ; BAKITA (*kuthibiti ufasaha wa lugha katika vitabu vya kiada, kushirikiana na vyombo vingine vya kukuza Kiswahili, kuandaa jarida la Kiswahili ili kuelezea mada mbalimbali za Kiswahili*. Kwa upande wa UKUTA, mtahiniwa huyo alitoa hoja kama *kuamsha ari ya wanaopenda kuandika vitabu*, *Kulinda utamaduni wa taifa*, *kuhimiza na kuhamasisha matumizi fasaha ya Kiswahili* hoja ambazo ni sahihi. Kielelezo 9.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza kazi za BAKITA na UKUTA kwa kutoa hoja tatu kwa kila upande ambazo ni toshelevu. Hata hivyo, watahiniwa wengi walikabiliwa na tatizo la kuchanganya kazi zinazofanywa na

asasi hizi, na hivyo hakuna mtahiniwa aliyemudu kupata alama zote katika swali hili.

Kielelezo 9.1


9 ya kutumika mashuleni, kwa kupitia hivo
matumizi ya Kiswahili fasaha yameongeze
kanchini na kuchangia kukuza na kueneza
lugha ya kiswahili.

Kuandaa jarida ambalo hueleza
maada mbalimbali za kiswahili na sanu
fiyake, Lengo la kuandaa jarida hilo ni
kuhakikisha kuwa watanzania wanazijua
kanuni mbalimbali zinazotawala katika
lugha ya kiswahili. Kupitia jarida hilo kisw
ahili kinapata nafasi ya kukua zaidi nchini
Tanzania na sehemu zingine Afrika mashari
ki, mfano Kenya na uganda ambako majari
da haya yana wafikia.

Pia ~~BAKITA~~ UKUTA Taasisi iliyoanzishwa
1959 na Mathias mnyampara ilichangia kwa
kiasi kikubwa katika uanzishwaji wake, taasi
si hiyo ina kazi zifuatazo katika kukuza na
kueneza lugha ya kiswahili,

Kuamsha ari kwa watu wanaotaka
kuandika vitabu mbalimbali vya kiswahili
na vile vya ushairi, Hutoa ushauri kwa
watu wenye nia ya kuandika vitabu mba
limbali na vile vya ushairi. Pia huwasaidi
a katika kuhakikisha wanachapisha vita
bu vyao na kusaidia kupata chapa yenye
ithibati ya kukithibitisha kuanza kutumi
ka. Kupitia hivo vitabu mbalimbali vya us
hairi vimepatwa kuandikwa na vinatumika
mashuleni, Hivyo kupelekea kukuza na kuen
eza kiswahili

Kukuza na kulinda utamaduni


9 wa Taifa katika nyanja zote, shughuli hi-
hizi hufanywa kwa kushirikiana na wi-
zara ya michezo na utamaduni. Matumi-
zi ya Kiswahili yanahimizwa kutumika, na
pia ushairi na michezo mbalimbali yana-
yoendana na utamaduni wa Kiswahili ua-
himizwa kutumika kote nchini. Mfano nga-
ma mbalimbali na nyimbo zenye kubeba
utamaduni wetu huhamasishwa kutumika.
Kuhimiza na kuhamasisha matumi-
zi ya Kiswahili fasaha na ushairi wake,
UKUTA inasimamia matumizi ya Kiswahili
fasaha nchini Tanzania, kwa kushirikiana
na taasisi nyingine ambazo huandaa kamu-
si yenye Kiswahili sanifu. Pia katika kukuza
ushairi wenye kutumia lugha ya Kiswahili
UKUTA hupitia vitabu mbalimbali vyaushai-
ri ili kuangalia ufasaha wa maneno yaliyo-
tumika na kupitisha. Kupitia hivi husaid-
ia kukuza na kueneza Kiswahili.
Pamoja na kuwa na umuhimu
mkubwa taasisi hizi zote mbili hukumbw-
a na changamoto mbalimbali kama vile
uhaba wa fedha za kuendeshea semina
mbalimbali, uhaba wa vitabu, uhaba
wa wataalamu wenye ujuzi wa kutosha ili
kuendesha taasisi hizo na pia serikali kuto-
toa ushirikiano mkubwa kwa changamoto
kubwa katika kufanikisha shughuli zao.

Kielelezo 9.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeleza kazi za BAKITA na UKUTA kwa usahihi na kupata alama za juu kati ya 12 na 19.

Hata hivyo asilimia 45.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani alama 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika baadhi ya hoja zake aliandika, *kuandaa wataalamu, kuandaa kamusi* (BAKITA) na kwa upande wa UKUTA aliandika, '*kuandaa sera zenye kuhimiza matumizi ya Kiswahili*' hoja ambazo hazikuwa sahihi kwa kuwa hamasa kuhusu

matumizi sahihi ya Kiswahili haikuwa kazi mojawapo ya UKUTA bali ya BAKITA. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyebainisha kazi za BAKITA na UKUTA kwa kuchanganya dhima hizo kwa baadhi ya hoja zake.

**Kielelezo 9.2**

9. Lugha ni sauti za nasibu zenye mpangilio maalumu wenye maana uliokubalika na jamii fulani kutumika kama chombo cha mawasiliano baina yao. Kiswahili ni lugha ya kibantu yenye asili ya mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki. Kama ilivyo lugha nyingine Kiswahili kina sifa ya kukua na kuenea, kuathiri na kuathiriwa na lugha nyingine, kukopa misamiati kutoka lugha nyingine na kuwa na hali ya ubora. Kipindi cha ukoloni Kiswahili kilikuwa na kuenea kwa sababu ya kutumika katika dini, utawala, elimu, biashara na shughuli zo kilimo. Baada ya uhuru Kiswahili kiliteuliwa kuwa lugha ya Taifa la Tanzania Vilianzishwa vyombo mbalimbali vya kukuza na kueneza Kiswahili. BAKITA ni Baraza la Kiswahili Tanzania ambalo lilianzishwa kwa lengo la kukuza na kueneza kiswahili. UKUTA ni Ukuzaji wa Kiswahili na Ushairi Tanzania chombo hiki pia kilianzishwa kukuza kiswahili.

Zifuatazo ni kazi za Baraza la Kiswahili Tanzania katika kukuza na kueneza Kiswahili.

Kuandaa wataalamu wa lugha ya Kiswahili ili waweze kufundisha katika shule za msingi hadi vyuoni. Kazi ya BAKITA ni kuandaa wataalam au walimu wa Kiswahili nchini ili wafundishe masomo ya Kiswahili kwa ufasaha katika shule mbalimbali na vyuo mbalimbali ili Kiswahili kiweze kukua na kuenea nchini.

Kuandaa kamusi ya Kiswahili na kuiboresha kuendana na wakati pamoja na ukuaji wa Kiswahili. Pia Baraza la Kiswahili Tanzania lina kazi ya kuandaa kamusi mbalimbali za lugha ya kiswahili ili ziweze kutumika mashuleni. Pia misamiati inapoongezeka ni kazi ya BAKITA kuandika kamusi nyingine kwa ajili ya matumizi ya Kiswahili shuleni hadi vyuoni.

9. Kubaliki kazi za Kiswahili ili ziweze kutumika katika elimu. Baraza la Kiswahili Tanzania lina kazi ya kuratibu na kubaliki kazi zinazoandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili ziweze kutumika katika ufundishaji wa Kiswahili bila kukidumaza na kuharibu Kiswahili.

Zifuatazo ni kazi za Ukuzaji wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA).

Kuandaa vitabu vya mashairi mbalimbali. Ukuzaji wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) una kazi ya kuandaa vitabu vya mashairi ili viweze kutumika katika shule na vyuo nchini. Hivyo mashairi yanapotungwa ni lazima UKUTA ihusike ili kupitisa wasomaji.

Kubaliki kazi za washairi mbalimbali kabla hazijaanza kutumika. UKUTA una kazi ya kubaliki kazi mbalimbali za ushairi zinazotungwa na washairi nchini ili kujua ubora na udhaifu wake ili ziweze kutumika katika medani za taaluma.

Kuandaa sera mbalimbali zitakazohimiza matumizi ya Kiswahili na utunzi wa ushairi. Pia UKUTA una kazi ya kuandaa sera mbalimbali zitakazosaidia Kiswahili kuzidi kukua na kuenea nchini Tanzania. Pia kuwasisitiza watunzi mbalimbali wa mashairi kutunga mashairi ya Kiswahili.


Hivyo basi, kutokana na kazi za vyombo hivi Kiswahili kinazidi kukua na kuenea nchini Tanzania na nje ya Tanzania. Sababu nyingine zinazowezesha kukua na kuenea kwa Kiswahili ni vyombo vya habari, shughuli za michezo, siasa, wasanii wa Tanzania, utawala, dini na elimu. Hali hii inafanya Kiswahili kupata hadhi ya kuwa lugha ya kimataifa kwani inatumika zaidi ya nchi moja ulimwenguni.


Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeelezea kazi za BAKITA na UKUTA kwa usahihi kwa baadhi ya hoja na nyingine kutojitosheleza na hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 25.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu yaani 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu kazi zinazofanywa na asasi za BAKITA na UKUTA katika jitihada za kueneza na kukuza Kiswahili. Baadhi yao, walielezea kazi za asasi hizo zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea kazi za BAKITA kama vile ;

‘*Kusanifisha lugha ya Kiswahili, kuchapisha mitihani mbalimbali, kuchapisha vitabu na kueneza elimu ya watu wazima*; na kwa upande wa UKUTA akataja hoja kama *kuchapisha kamusi, kusanifisha lugha ya Kiswahili*, majibu ambayo si sahihi kama kielelezo 9.3 kinavyodhihirisha hayo.

**Kielelezo 9.3**


4. BAKITA, Baraza la Kiswahili Taifa. BAKITA
na UKUTA ni taasisi za Kiswahili ambazo zilizundu
kwa lengo la kukuza na kueneza Kiswahili
Zifuatazo ni kazi za BAKITA na UKUTA katika
kukuza na kueneza Kiswahili. Kwa kuanza na
BAKITA;
Kusanifisha Lugha ya Kiswahili, Kazi ya kwanza
ya BAKITA ni kusanifisha lugha ya Kiswahili. B
araza la Kiswahili Taifa katika kukuza na kueneza
Kiswahili limesaidia katika kusanifisha Lugha ya
Kiswahili na kupanga kuwa lugha sanifu. Kwahiyo
Baraza la Kiswahili limesaidia kusanifisha lugha ya
Kiswahili
Kuchapisha mitihani mbalimbali, Kazi nyingine
ya Baraza la Kiswahili Taifa ni kuchapisha mitihani
mbalimbali ya Kiswahili kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi
Baraza Kiswahili Taifa limejihusisha na uchapishaji wa
mitihani ya wanafunzi mbalimbali kwa lengo la kuwasaidia
hii. Kwa hiyo kazi nyingine ni kuchapisha mitihani
mbalimbali kwa lengo la kuwasaidia wahitimu mbalimbali
Kupitia mitihani mbalimbali limesaidia kukuza na
kueneza Lugha ya Kiswahili
Kuchapisha/Walichapisha vitabu mbalimbali
ya Kiswahili, pia Baraza la Kiswahili la Taifa
limesaidia katika kuchapisha vitabu mbalimbali na vitabu
hivyo vilichapishwa kwa lugha ya Kiswahili. Kupitia
kuchapisha vitabu mbalimbali kulizhangia katika
kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo
Kazi nyingine ya BAKITA katika kukuza na
kueneza lugha ya Kiswahili ni kuchapisha vitabu
mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili
Kwa kufuatia na UKUTA, Zifuatazo ni kazi za ukuta


9: Kuanzia elimu kwa watu wazima, kazi ya kwa ya UKUTA ilikuwa ni kuanzia elimu kwa watu wazima, kupitia kuanzia elimu kwa watu wazima pia ikapelekea kukua na kuenea kwa Kiswahili. Kazi ya kuanzia ni kuanzia elimu kwa watu wazima.
Kusanifisha lugha pia kazi ya pili ya UKUTA katika kukuza na kuenea lugha ilikuwa ni kusanifisha lugha ya Kiswahili. Pia UKUTA katika kukuza na kuenea Kiswahili ilifanya kazi ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Kupitia kusanifisha lugha ya Kiswahili vilevile ikapelekea Kiswahili kukua na kuenea. Kwa hiyo kazi nyingine ya UKUTA ni kusanifisha lugha ya Kiswahili.
Walichapisha kamusi mbalimbali za lugha ya Kiswahili, vilevile kazi nyingine ya UKUTA katika kukuza na kuenea Kiswahili ilikuwa ni kuchapisha kamusi mbalimbali. Kupitia kuchapisha kamusi mbalimbali za Kiswahili / kwa lugha ya Kiswahili vilevile ikapelekea kukua na kuenea lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo kuchapisha kamusi pia ni kazi moja wapo kati ya kazi za UKUTA katika kukuza na kuenea Kiswahili.
Hitimisho, vyombo vyote hivyo vitoa kazi mbalimbali na bado vina umuhimu mkubwa katika suala zima la kukuza na kuenea Kiswahili nchi Tanzania. Hivyo basi kuna haja ya vyombo hivyo kuendelea kuwepo.


Kielelezo 9.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza hoja mbalimbali za asasi za BAKITA na UKUTA badala yake akaeleza hoja zisizohusiana na asasi hizo kinyume na matakwa ya swali.

## 2.6 SEHEMU E: TAFSIRI

### 2.6.1 Swali la 10: Nadharia ya Tafsiri

Swali lilitoka mada ya *Tafsiri na Ukalimani* na lilimtaka mtahiniwa kufafanua mambo muhimu sita ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri. Swali hilo lililenga kupima Uchambuzi na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wengi (asilimia 99.7) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la lazima. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango kidogo cha kufaulu. Asilimia 42.2 pekee ndio walioweza kujibu swali hili na kupata alama za juu na za wastani. Chati Namba 10 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 10**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Idadi kubwa ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 6.5 kwa kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri.

Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 21.2 walipata alama za chini zaidi yaani 0 hadi 1 kwa kuwa walishindwa kutoa utangulizi unaofaa na kufafanua mambo sita ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri isivyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika majibu yake alitoa hoja hizi; ‘*kuwa mjuzi au mahiri, kujua mazingira ya lugha chanzi*, *kuwa na kamusi husika, kuwa karibu na wajuzi, kutumia maneno ya karibu au maana sawa*’ kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri.


**Kielelezo 10.1**

10. Kutafsiri ni hali ya uhaulishaji wa ujumbe au maana kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine au kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Ni kweli kuwa kazi ya kutafsiri ina taratibu mahsusi. Zifuatazo ni taratibu mahsusi wakati wa kutafsiri au ufasiri.

Kuwa mjuzi au mahiri wa lugha zote mbili. Mfasiri anatakiwa kuwa mahiri wa lugha zote mbili yaani lugha chansi na lugha lengwa ili kuwawezesha kufasiri maana kamili ya ujumbe kutoka lugha chansi kwenda lugha lengwa.

Pia vile vile ni muhimu kujua mazingira ya lugha chansi yalipotokea. Ni muhimu kabla ya kutafsiri, mfasiri lazima ajue mahali au mazingira ya lugha chansi ilipotokea iwe ya kanisani, mtaani, shuleni na kwingineko ili kutoweza kuharibu maana ya lugha chansi kwenda lugha lengwa.

Pia ni muhimu kuwa na kamusi wakati wa ufasiri ili kurahisisha na uwiano



10 wa misamiati migumu. Mfasiri ni kweli lazima awe mahiri wa lugha zote mbili pia ni lazima awe na kamusi kwa maana kuna baadhi ya maneno yana maana zaidi ya moja mfano katika kiswahili neno kama! Mbuzi, kanga, meza na mengine. Hii humuwezesha mfasiri kujua neno lililoyotumika.

Pia kutafsiri kunatakiwa mtu awe karibu na wajuzi au mazingira ya lugha zote mbili. Hii hunipa urahisi wakati wa kufasiri, pale kunapotokea kwa maneno mapya labda ya simo au msimu, Rejesta, istilahi na menginevyo hii ni taratibu mojawapo ya kutafsiri.

Kutafsiri kunatakiwa kutumia maneno ya karibu na maana sawa na lugha chansi kwa maneno ambayo hayapo katika lugha Lengwa. kwa mfano kiswahili kina misamiati michache ukilinganisha na misamiati ya kiingereza. Hivyo kama kuna msamiati mgumu, mfasiri anatakiwa kutafsiri neno lililo karibu maana na neno la lugha Chansi.

Kutafsiri kunatakiwa maana kamili ya lugha chansi hata kama haipo sawa na ~~mag~~ mapendekezo yako. mfano: Wachaga ni wachafu kwenda kwa kiingereza unatakiwa kutafsiri maana hata kama siokweli kuwa wachaga ni wachafu. Hii ni moja ya umuhimu ~~wa~~ wa taratibu za kutafsiri.

Kwa ujumla ~~mfso~~ kutafsiri ni taratibu ambazo zinaendana kwa kiasi kikubwa na taratibu na sifa za mfasiri, kuwa ni lazima awe na kamusi za lugha zote mbili yaani Lugha chansi na lugha Lengwa na pia usawa uwe katika kwa karibu na wajuzi.

Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye alishindwa kufafanua mambo sita ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri.

Watahiniwa wachache, asilimia 34.8 walijibu vizuri swali hili na kupata alama 12 hadi 20 kutokana na kumudu kueleza *maana ya tafsiri* na kufafanua mambo muhimu sita ya kuzingatia wakati wa kufanya zoezi la tafsiri kama vile *maandalizi, uchambuzi, uhawilishaji, rasimu ya I, II na III.* Kielelezo 10.2 kinaonesha

jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri.

**Kielelezo 10.2**

10. Tafsiri ni kitendo cha kuhawilisha mawazo au taarifa kutoka Lugha chanzi kwenda Lugha Lengwa kwa njia ya maandishi. Tafsiri ni taaluma inayotumia Lugha ambapo mtu anayefanya kazi hii ya tafsiri anapaswa awe ni mjuzi wa Lugha mbili au zaidi ya mbili tofautitofauti ili aweze kukamilisha taaluma yake. Katika Tafsiri kitu au wazo ambalo linatafsiriwa linaitwa matini ambapo matini hayo yanatolewa kutoka Lugha chanzi kwenda Lugha lengo. Lugha chanzi ni ile Lugha ya kuanza ambayo haijafanyiwa mchakato wowote wa Tafsiri na Lugha Lengwa ni ile ambayo imefanyiwa mchakato wa tafsiri. Ili ukamilishe mchakato wa Tafsiri ni lazima ufuate hatua zake za muhimu ili uweze kukamilisha. Yafuatayo ni mambo muhimu sita ya kuzingatia wakati wa kufanya kazi ya Tafrisi.

Maandalizi, hii ni hatua ya muhimu ya kuzingatia wakati wa kufanya maandalizi. Hii ni kwa sababu mtafsiri anapasa afanye maandalizi ya kujiandaa yeye mwenyewe na kazi hiyo halafu anaanza kuandaa vitu ambavyo atavitumii kama vile anaandaa kamusi, anaandaa kalamu na karatasi. Vifaa hivi vinamsaidia yeye kutunza kumbukumbu na kamusi itamsaidia kutafuta maana ya maneno magumu atakayokutana nayo kwenye matini chanzi. Hivyo basi maandalizi ni jambo la muhimu linalomwezesha mtafsiri kufanya kazi yake kwa ufasaha.

Uhawilishaji wa matini chanzi kwenda matini lengwa, hii ni hatua ya muhimu kwa mfasiri kwani anapokuwa ameshafanya maandalizi yake ya kuweka vifaa vyake tayari anaanza kuhawilisha maana kutoka katika matini chanzi kwenda matini Lengwa. Mfano anatafsiri kazi iliyoandikwa kwa Lugha ya Kiingereza kwenda katika Lugha ya kiswahili ataanza kuhawilisha maana na kama kuna neno gumu ataangalia kwenye kamusi na atapata

10 maana halisi ya neno na ataendelea na mchakato wake kwa kubadilisha maana toka lugha chanzi kwenda lugha lengua. Hili pia ni jambo la muhimu sana la kuzingatia wakati wa kufanya kazi ya tafsiri.

Uandaaji wa rasimu ya kwanza, hili pia ni jambo la muhimu katika kufanyakazi ya tafsiri. Hatua hii mfasiri anakuwa amesha fanya uhawilishaji na kama kuna neno gumu tayari anakuwa ameshalitafutia maana yake ndipo anaandaa rasimu yake ya kwanza kwa kuiandika kwa makini bila kukosea. Hatua hii ya usowili wa rasimu ya kwanza mfasiri anakuwa amekaa mwenyewe ndipo anafanya kazi hii bila ya kumshirikisha mtu mwingine yoyote. Hii ni hatua ya muhimu ya kuzingatia wakati wa kufanya kazi ya tafsiri kwani mfasiri yoyote hawezi akakurupuka na kufanya tafsiri bila ya kufanya maandalizi na kufanya au kutengeneza rasimu ya kwanza.

Udurusu wa rasimu ya kwanza, hii ni pia taratibu ya muhimu katika kufanya kazi ya tafsiri. Kwasababu mfasiri yoyote ni lazima aandae rasimu ya kwanza na akiishamaliza kuiandaa rasimu hiyo anatakiwa aidurusu rasimu hiyo kwa kuisoma upya na kuifanyima marekebisho mahali ambapo anakuwa alikosea wakati anaandaa rasimu ya kwanza. Hivyo basi udurusu wa rasimu ya kwanza ni jambo la muhimu la kuzingatia wakati wa kufanya kazi ya tafsiri ili kufanya kazi ya mfasiri aliyoifasha kwenye rasimu yake ya kwanza iwe nzuri kwani anakuwa ameihakiki rasimu yake na kuirekebisha rasimu hiyo.

Uaandaaji wa rasimu ya pili, hii pia ni hatua ya muhimu kwa mfasiri kwani anakuwa ameshafanya michakato yote ya kutengeneza rasimu yake

10 ili ibae vizuri sasa anaandika upya rasimu yake ya pili kwa usahihi na kwa umakini wote kwani anakuwa tayari alishafanya masahihisho kwenye hatua iliyopita ya udurusu wa rasimu ya kwanza. Hivyo basi uandaaji wa rasimu ya pili ni hatua ya muhimu kwani mfasiri anakuwa alishafanya hatua zote na anakuwa ameshahakiki kazi yake hivyo kazi hiyo inakuwa ipo tayari.

Anampa mtu mwingine aisome rasimu ya pili, hii ni hatua ya mwisho ya kuzingatia wakati wa kufanya kazi ya tafsiri. Unamtafuta mtu ambaye ni mjuzi wa taaluma uliyoifanyia tafsiri na yeye pia ni mtafsiri na anajua kanuni zote za tafsiri. Ndipo kazi ya tafsiri inakuwa imeshakamilika.

Hivyo basi tafsiri ni taaluma ya muhimu kwani inafaida kubwa kwa watu na miongoni mwa faida za tafsiri ni inarahisisha mawasiliano, inaongeza kipato cha mtu na inamfanya mtu anakuwa mmahili wa lugha zaidi ya moja.

Kielelezo 10.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeelezea mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri kwa usahihi.

Hata hivyo, asilimia 11.4 ya watahiniwa wengine waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani 7 hadi 11.5 kwa kuwa walitoa majibu yasiyojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika majibu yake aliandika ‘‘*mfasiri lazima asome matini chanzi kwa uangalifu ili kuelewa lengo la matini hiyo, kubaini mada iliyoandikwa kwenye matini chanzi*’’ hoja ambazo zilitakiwa ziwe ‘*Mfasiri afahamu maudhui ya matini chanzi kama vile malengo, utamaduni na hadhira lengwa*’ majibu ambayo ni sahihi. Aidha, mtahiniwa huyo aliweza kueleza maana ya tafsiri na kutaja baadhi ya mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri kwa usahihi. Kielelezo 10.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa majibu yaliyokuwa na mapungufu kwa baadhi ya hoja.

**Kielelezo 10.3**

10 Tafsiri, ni zoezi la uhawilishaji wa habari au ujumbe ulio katika maandishi kutoka lugha moja yaani lugha chanzi kwenda lugha nyingine yaani lugha lengwa, kwa mfano kutoka katika lugha Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili, hivyo chanzi habari au ujumbe unatafsiriwa uwe katika maandishi na si vinginevyo. Kuna baadhi ya mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri, mambo hayo ni kama yafuatayo:


10. Kusoma matini chanzi kwa makini na kwa uangalifu, lengo la kusoma matini chanzi kutaka kuelewa nini hasa habari husika inazungumzia hivyo mfasiri ni lazima asome kwa nzo matini chanzi kwa uangalifu ili kuelewa lengo la matini hiyo.

Kubaini ~~mada~~ aina ya utindo wa matini chanzi, Mulimu mfasiri kujua mtindo ulio tumika na mwandishi wa matini chanzi ili aweze kutoa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa matini chanzi bila kubadili cha hivyo kufanya kazi yake kwa ufasaha mkubwa.

Kubaini mada iliyoandikwa katika matini chanzi, mada inaweza kuwa inahusu mambo mbalimbali mfano masuala ya kiuchumi, kiutamaduni kisiasa na kijamii hivyo ni vizuri kwa mfasiri kujua mada ya matini hiyo

Kuandika rasimu ya kwanza, hii ni tafsiri ya kwanza au hatua ambayo mfasiri huandika tafsiri yake kwa lengo la kufanya marekebisho ya mwisho yaani ~~yo~~ yanapohitajika hii huwa ni kama kioo cha tafsiri inayokuja.

Udurusu wa rasimu ya kwanza, kudurusu ni kurudia kuandika matini chanzi ambayo imefanyiwa marekebisho madogo madogo na kuchunguzwa kwa makini na mfasiri wa matini hiyo kwani hii ndicho kipimo cha matini lengwa.


10. Kuendika matini lengwa, hii ni kazi ya mwisho kabisa katika zoezi la tafsiri ambapo kazi hii huwa ime mahitaji yote yanayohitajika katika tafsiri na huwa imefanyiwa marekebisho ya kutosha na mfasiri au wafasiri.
Mwisho, ubora wa matini lengwa ni sharti iwe na uwezo wa kufasiriwa upya kutoka lugha lengwa kwenda lugha chanzi na majibu yakija vile vile tafsiri hii itakuwa ni ya ubora wa hali ya juu sana, licha ya kuwepo kwa changamoto kama vile ~~ukosefu wa~~ upungufu unao jitokeza katika tafsiri.

Kielelezo 10.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa baadhi ya hoja sahihi na nyingine zisizojitosheleza katika maelezo yake na hivyo kupata alama za wastani.

# 3.0 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI

## 3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI


## 3.2 SEHEMU A: FASIHI KWA UJUMLA

### 3.2.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na lilimtaka mtahiniwa kwa kutumia mifano kuelezea tofauti nne kati ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Watahiniwa wachache, asilimia 20.8 pekee ndio waliojibu swali hili kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili lilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha kufaulu kwa watahiniwa ikilinganishwa na maswali mengine katika mtihani huu. Chati

Namba 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 1**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Idadi kubwa ya watahiniwa, asilimia 83.8 walipata alama za chini (dhaifu) 0 hadi 6.5 kutokana na kushindwa kuelezea tofauti nne kati ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, zaidi ya nusu ya watahiniwa hao (47.9%) walipata alama 0 kwa kuwa walikosa maarifa kuhusu dhana ya fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, watahiniwa walio wengi walifananisha dhana ya fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa lugha ya Kiswahili na ile inayohusu fasihi andishi na fasihi simulizi na hivyo kutoa hoja zilizoegemea katika kutofautisha fasihi andishi na fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile '*uwasilishwaji, marekebisho, umiliki na umri/ukongwe*' ili kutofautisha fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa lugha ya Kiswahili kinyume na matakwa ya swali. Mtahiniwa huyo alitakiwa kutoa hoja kama vile *mazingira/mandhari, utamaduni, lugha* na *uhalisia* ambazo ndizo hoja sahihi zinazotofautisha fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa lugha ya Kiswahili. Kielelezo 1.1 ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja za kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 1.1**

1\. Fasihi ya kiswahili, ni fasihi inayotumia lugha ya kiswahili katika uwasilishwaji wake kutumia njia ya ki mdomo ili kuweza kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa lakini fasihi kwa lugha ya kiswahili ni fasihi inayoa-ndikwa kwa kutumia lugha ya kiswahili yaani fasihi ya maandishi ambapo hadhira huweza kubaini lengo kwa kusoma kazi ya fasihi husika. kazi hizi huweza kuwa na tofauti katika kufikia hadhira.

Zifuatazo ni tofauti kati ya fasihi ya kiswahili na fasihi kwa lugha ya kiswahili;

Uwasilishwaji; fasihi ya kiswahili ni fasihi ya jamii nzima hivyo huweza kuwasilishwa kwa njia ya mdomo na hadhira ukawasilikiza lakini fasihi kwa lugha ya kiswahili huweza kuwasilishwa kwa njia ya maandishi ambapo kitabu chake hutuwa ni kusikiliza. kwa mfano fasihi ya kiswahili ni hadithi, ngonjera lakini fasihi kwa lugha ya kiswahili ni riwaya tamthiliya;

Marekebisho; fasihi ya kiswahili huweza kufanyiwa mareke-bisho ya papo hapo kutokana na hadhira na fanani kuweza kukutana katika mandhari fulani lakini fasihi kwa lugha ya kiswahili si rahisi ......


kufanyiwa marekebisho kwa sababu
ni fasihi inayotumia lugha ya kiswahili
1 katika hali ya maandishi marekebisho
yake huweza kuwa mpaka toleo la pili
kwa mfano; kazi za fasihi zinazo
andikwa kwa kiswahili ni tamthiliya
"Kwenye ukingo wa Thim" ya Ebrahim
Hussein.
Umiliki; kazi ya fasihi ya
kiswahili huweza kumilikiwa na
jamii nzima kutokana imetokana na
mazingira yanayowazunguka, lakini
fasihi kwa lugha ya kiswahili si
mali ya jamii yote kwa sababu ime-
-tumia tu ya kiswahili ili kuweza
kufikia hadhira, lengwa mara nyingi
huwa ni mali ya aliyeitunga na
kuandikwa katika lugha husika.
Tanzu na umri; fasihi ya
kiswahili ina tanzu nyingi kuliko kazi
nyingine na pia ni kongwe katika
maisha ya mwanadamu kwani ili
anza kutumika pindi mwanadamu
alipoanza kuyaita vitu mbalimbali lakini
fasihi kwa lugha ya kiswahili ina
tanzu chache kama riwaya, tamthiliya
ushairi pia ilianza kutumika pindi
lugha ya kiswahili ilipokuwa na kuenea
yani kugundulika kwa maandishi
Hivyo, fasihi ya kiswahili na
fasihi kwa lugha ya kiswahili pia
huweza kufanana katika vipengele-
vingi.

Kielelezo 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetumia hoja za kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi ili kuelezea tofauti kati ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili kama vile *uwasilishwaji, umiliki, marekebisho na umri* kinyume na matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa wachache sana asilimia 16.2 pekee ndio walioweza kujibu swali hili na kupata alama za wastani na zaidi. Asilimia 2.9 pekee ya watahiniwa hao walijibu vizuri swali hili na kupata alama 12 hadi 17 kwa kuwa waliweza kuelezea tofauti nne kati ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili na kutoa mifano dhahiri kama vile *mazingira/mandhari*, *utamaduni*, *lugha* na *uhalisia*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kujibu vizuri kwa kutoa majibu yaliyokidhi mahitaji ya swali na yaliyodhihirisha uwezo mkubwa wa mtahiniwa huyo

katika mada ya Fasihi kwa Ujumla. Vile vile aliweza kutoa utangulizi mzuri na hitimisho zuri lililoendana na swali. Kielelezo 1.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri na kutoa mifano maridhawa.

**Kielelezo 1.2**


1. Fasihi ni kazi ya sanaa ambayo hutumia
lugha kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa
jamii iliyokusudiwa. Kuna aina mbili za
Fasihi yaani Fasihi andishi na Fasihi
Simulizi. Moja huwasilishwa kwa njia ya

1. yamdomo na nyingine huwasilishwa kwa maan-
dishi.
Zifuatazo ni tofauti kati ya Fasihi ya
Kiswahili na Fasihi Fasihi kwa lugha ya
Kiswahili.
Fasihi ya kiswahili ni fasihi inayohusu
maisha ya Waswahili wakati Fasihi kwa ki-
swahili ni kazi ya fasihi ambayo huandikwa
kwa kutumia lugha ya kiswahili. Fasihi ya
kiswahili huwa inachambua na kuibua yale
ambayo yanawahusu waswahili na maisha yao
wakati fasihi ya lugha ya kiswahili huweza kuya-
dili mambo yasiyohusiana na waswahili
Fasihi ya kiswahili huendana na utamaduni
wa Waswahili wakati fasihi kwa lugha kiswahili
huweza kuendana na tamaduni za watu
wengine nje ya waswahili. Hii ni kutokana
na kuwa Fasihi kwa lugha ya kiswahili huusi-
sha matumizi ya lugha ya kiswahili na sio
uswahili wenyewe kama ilivyo katika
Fasihi ya kiswahili. Kwa mfano "Spared" fasihi ya kiswahili
Fasihi ya kiswahili huweza kutumia lugha
yoyote wakati Fasihi kwa lugha ya kiswahili
inabanwa kufanya hivyo. Mfano katika fasihi
ya kiswahili mwandishi au mtunzi huweza
kutunga kazi yake kwa kutumia lugha ya
Kiingereza au Kikabila lakini akabeba
maudhui na ujumbe uliopo katika maadha-
ri ya waswahili. Jambo ambalo ni tofauti
katika Fasihi kwa lugha ya kiswahili kwani
humpasa msanii atumie lugha ya kiswahili
na maudhui hayabanwi. Kwa mfano "I will marry when I want"
fasihi ya kiswahili

Kielelezo 1.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuelezea tofauti nne kati ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili na kutoa mifano mahususi.


Hata hivyo, asilimia 13.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kulingana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizojitosheleza kuhusu tofauti kati ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, mtahiniwa huyo alitoa utangulizi unaohusisha fasihi andishi na fasihi simulizi badala ya fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa lugha ya Kiswahili. Kielelezo 1.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 1.3**

1. Fasihi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Kuna aina mbili za fasihi ambazo ni fasihi simulizi na fasihi andishi. Fasihi simulizi ni aina ya fasihi inayowasilishwa kwa njia ya mdomo mfano, hadithi, majigambo na ngonjera. Fasihi andishi ni aina ya fasihi inayowasilishwa katika maandishi mfano, tamthiliya, ushairi na riwaya. Fasihi ni chombo cha ukombozi wa jamii kwani huweka wazi uovu uliopo katika jamii na kuupiga vita.
Zifuatazo ni tofauti kati ya Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili.

Fasihi ya Kiswahili ni fasihi iliyopo katika jamii ya Kiswahili ambayo hutumika kwa watu wote lakini fasihi kwa lugha ya Kiswahili ni fasihi iliyopo katika lugha ya Kiswahili yaani uandishi wake upo kwa lugha ya Kiswahili.

Fasihi ya Kiswahili ni zao la jamii inayotumia Kiswahili katika mazungumzo yao ambapo hutumia Kiswahili baina yao lakini fasihi katika lugha ya Kiswahili inaweza isiyo zao la katika jamii inayotumia Kiswahili kwani maandishi yake yanaweza kuwa yametafsiriwa kutoka lugha nyingine na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili.


1. Fasihi ya Kiswahili inaendana na chimbuko la lugha ya Kiswahili kwani ilianza kuandikwa na kutumika kama vile lugha ya Kiswahili ilivyoanza kutumika lakini fasihi kwa lugha ya Kiswahili haiendani na chimbuko la kiswahili kwani inaweza kuwa imetokana na lugha nyingine hadi kubamizishwa katika lugha ya Kiswahili.

Fasihi ya Kiswahili inaweza andikwa kwa kuchanganywa na lugha nyingine mfano kiingereza katika uandishi wake ili kuboresha kazi ya fasihi lakini fasihi kwa lugha ya kiswahili haichanganywi na lugha yoyote inapokuwa Kiswahili peke yake kwani ni fasihi kwa lugha ya Kiswahili.

Hivyo, Fasihi ya Kiswahili na Fasihi kwa lugha ya Kiswahili zinatofautiana sana ingawa pia kuna uhusiano wa karibu kwani zote zinahusisha lugha ya Kiswahili.


Fasihi ni muhimu katika jamii kwani inarasimisha kuelimisha jamii, kutunza na kurithisha amali za jamii, kuburudisha jamii na kukosoa jamii. Pia fasihi inadumisha na kuendeleza lugha hivyo inabidi kutunza fasihi ya Kiswahili kwa maendeleo ya lugha ya Kiswahili.

Kielelezo 1.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa majibu kama vile *fasihi ya Kiswahili huendana na chimbuko…, fasihi ya Kiswahili ni zao la jamii…*, majibu ambayo hayakidhi haja ya swali hili.

### 3.2.2 Swali la 2: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na lilihusu mada ndogo ya Fasihi Simulizi na lilimtaka mtahiniwa kuelezea dhima tatu za hadhira katika utanzu wa hadithi na dhima mbili za hadhira katika utanzu wa vitendawili. Swali lililenga kupima maarifa na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 76.1 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Asilimia 56.3 ya watahiniwa hao walifaulu kwa kiwango cha wastani na kizuri. Chati Namba 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 2**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Miongoni mwao, asilimia 20.8 walijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 19, kwa kuwa waliweza kuelezea dhima tatu za hadhira katika utanzu wa hadithi na dhima mbili za hadhira katika utanzu wa vitendawili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa utangulizi mzuri na kuhitimisha vizuri. Vile vile aliweza kuelezea nafasi ya hadhira katika utanzu wa vitendawili kama vile *kuwa waitikaji, kutoa vichocheo, kupiga makofi na kuwa wahusika* na katika kipengele cha hadithi kama *mwitikaji katika utambaji wa hadithi*, *kuitikia kibwagizo cha wimbo*, *kuwa wahusika* na kupata alama nzuri. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 2.1**


2. Fasihi simulizi ni aina ya fasihi au kazi ya sanaa inayowasilishwa kwa njia ya mdomo au masimulizi. Hadithi ni masimulizi yanayotolewa na mtu kwa wakati fulani yenye kusimuliwa na kuandikwa. Hadhira ni washiriki katika masimulizi. Lengo la hadhira ni kupa uhai kazi ya fasihi simulizi. Ziyafuatazo ni dhima za hadhira katika utanzu wa hadithi na dhima za hadhira katika utanzu wa vitendawili. Kwa kuanza na dhima za hadhira katika utanzu wa hadithi.

Kuuliza maswali kwa fanani pale ambapo hawaelewi na kujibu na fanani, hivyo kazi ya hadhira ni kuuliza maswali yeyote kwa fanani endapo hawaelewi kitu au kutaka kujua jambo fulani kuhusu hadithi hiyo.

Kuitikia vile anavyotaka fanani wafanye, hadhira katika masimulizi wana kazi ya kujanja au kuitikia vile wanavyoambiwa na fanani mfano fanani akisema paukwa!" hadhira wanatakiwa kuitikia pakawa!" na miguno ya kuitikia kama mfano mmh'ili fanani ahakikishe anaendelea kwa makini.

Kushangilia kama vile kuimba, kupiga makofi na fanani, hii hutokea pale hadhira wanapo furahishwa na simulizi au kunapokuwa na wimbo wa kuimba katika hadithi hiyo fanani na hadhira huimba. Zifuatazo ni dhima za hadhira katika utanzu wa "vitendawili."

Kuitikia fanani anapoanza kuuliza swali mfano fanani anaposema kitendawili? hadhira wana kazi ya kujibu tega! hivyo hadhira ana dhima ya kuitikia fanani anapoanza kusema kitendawili



2. Kujibu maswali yanayoulizwa na fanani hadhira wakati wa kitendawili ana dhima ya kujibu maswali yanayoulizwa ambayo ni vitendawili mfano kuku wangu ametagia mibani hadhira hujibu nanasi.


Kupiga makofi au kupongeza aliyejibu kitendawili ... hadhira wakati ya kushangilia na kupiga makofi kwa yule aliyejibu vizuri au jawabu mwenzako.

Hivyo basi vitendawili na hadithi katika utendaji wa hadhira hautofautiani sana kwani zote ni kazi za fasihi simulizi na hupamba utendaji.

Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuelezea dhima tatu za hadhira katika utanzu wa hadithi na dhima mbili za hadhira katika utanzu wa vitendawili.

Hata hivyo, watahiniwa wengine asilimia 35.5 walipata alama za wastani yaani 7 hadi 11.5 kwa kutoa majibu yasiyojitosheleza kulingana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi lakini zisizo na ufafanuzi unaotosheleza. Aidha, mtahiniwa huyo hakutoa mifano dhahiri ili kuelezea dhima za hadhira katika tanzu za hadithi na vitendawili. Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa maelezo yasiyojitosheleza kwa baadhi ya hoja za swali hili.

**Kielelezo 2.2**


2 Hadhira, hawa ni watu ambao wanashiriki katika kazi ya fasihi huwa binadamu. Hadithi, utanzu unaotumia lugha ya nathari kufikisha ujumbe, wakati vitendawili, ni semi fupi ambazo hulenga kupima teleg rocia za watu. Kwa kuanza na hadithi hadhira huwa na dhima zifuatazo

Kuipa utendaji hadithi kwa kushiriki katika kuuliza maswali kupiga makofi

Huipa hadithi uchangamfu wa mahukio kwa kuimba mfano pale ambapo mtambaji husimulia na hivyo hadhira huamua kushiriki kwa kuimba

Kuleta dhana ya ushirikishwaji hadhira hushiriki katika hadithi kwa kujibu maswali yanayoulizwa na mtambaji vilevile kwa kuuliza hii huleta ushirikishaji baina ya hadhira na fanani au mtambaji

Vilevile vitendawili hadhira huwa na dhima zifuatazo.

Hukamilisha maana ya vitendawili, hadhira hufanya kazi ya kukamilisha maana kwani kitendawili huwa ni swali ambalo hutegwaji kukamilishwa mfano Nyumba yangu haina mlango hadhira hukamilisha kwa kusema yai


2 Hukamilisha wazo au hukuza na kutanua bongo au akili zao kwa kukamilisha wazo la kitendawili mfano kuku wangu atagia mibani maana yake nanasi hii hutanua akili ya hadhira hasa watoto.

Hata hivyo hadithi na vitendawili hutumia hadhira ili kulifikia lengo kwa kufikia hadhira inayokusudiwa.

Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kushindwa kutoa maelezo yenye kutosheleza baadhi ya hoja zinazohusu dhima ya hadhira katika hadithi na vitendawili.

Baadhi ya watahiniwa, asilimia 43.7 walipata alama hafifu kutokana na kujibu kinyume na matakwa ya swali. Watahiniwa wengine, asilimia 7.3 walishindwa kabisa kubaini dhima ya hadhira katika tanzu za hadithi na vitendawili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza dhima za fasihi kama vile; *kujifunza, kuonya jamii*, *kukuza lugha*, *kuburudisha jamii na kujenga jamii* badala ya kuelezea dhima za hadhira katika tanzu za hadithi na vitendawili kama vile *mwitikaji katika utambaji wa hadithi, kuitikia kibwagizo cha wimbo, kuwa wahusika* (hadithi) na *kuwa mwikaji, kutoa vichocheo, kupiga makofi na kuwa wahusika* (vitendawili). Kielelezo 2.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kabisa kubaini dhima ya hadhira katika tanzu za hadithi na vitendawili.

**Kielelezo 2.3**




2. Hadhira ni watu wote wanaoweza kusikiliza na kuungana na fanani wakati wa kutoa kazi yake ama simulizi, hadithi na maigizo hii huweza kutolewa katika sehemu mbali-mbali na lazima kuwe na, eneo, fanani mwenyewe na hadhira, dhamira na vitu vingine.

Katika utanzu wa hadithi hadhira huwa na dhima nyingi na muhimu sana katika jamii kama.

Kujifunza, Hadhira hupata mafunzo kutokana na hadithi ambayo anaipokea kutoka kwa fanani na kuweka dhamira hiyo katika hali halisi ya maisha ambayo huweza kujifunza na mambo mengine na kujifunza jamii pia

Kuonya jamii, hii pia ni dhima ambayo huweza kupatikana kwa hadhira wakati apokeapo hadithi na kupeleka kuonya jamii kulingana na shughuli ama mambo yaliyopo.

Kukuza lugha, Hadhira pia anaweza kukuza na kuweza lugha kutoka kwa fanani anaetoa hadithi kwani inaweza kuwa ni kwa Kiswahili ama lugha nyingine ambazo huweza kuzalisha maneno mengine na kujikuta wanakuza lugha hiyo.



2. Pia katika utunzi wa vitendawili
unaweza kupata dhima nyingine
kama ifuatavyo
Kuburudisha jamii, suala
la vitendawili katika jamii husika
hutumika kama kiliwazo na
kiburudisho cha jamii pale
wanapofundishana mambo mbalimbali
katika maisha ya binadamu.
Kujenga jamii pamoja
na kupatanisha. Katika tunzi
ya vitendawili mara nyingi huweza
kukutanisha jamii zetu na
kuzimeka katika hali ya wafika
kupitia vitendawili
Maisha, kupitia tunzi mbalimbali
jamii pia imeweza kupata maendeleo
kama vile mengizo, ngonjera, na
tamthilia hivyo Serikali inaonekana
kuwapa kipaumbele zaidi wale
wote wanaohusika na michezo hiyo
kuwa ni moja ya pato la taifa.

Kielelezo 2.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili kwa kuelezea dhima za fasihi kinyume na matakwa ya swali.


## 3.3 SEHEMU B: USHAIRI

### 3.3.1 Swali la 3: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*. Swali hili lilihusu vitabu teule vya Ushairi na lililenga kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze jinsi uongozi mbovu ulivyo kikwazo kwa maendeleo ya jamii katika kujipatia maisha bora kwa kutoa mifano minne kwa kila diwani. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali lilijibiwa na asilimia 55.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi na idadi kubwa ya watahiniwa ambapo asilimia 98.5

walifanya vizuri na kufaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 3 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 3**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Watahiniwa wengi, asilimia 79.1 walijibu swali hili vizuri kwa kupata alama 12 hadi 19. Watahiniwa hao waliweza kuelezea jinsi uongozi mbovu unavyokuwa kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora kwa kutoa mifano minne kwa kila diwani kama ilivyotakiwa. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 21.8 walijibu swali hili vizuri zaidi na kupata alama 16 hadi 19. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa utangulizi mzuri, na aliweza kuelezea hoja zinazokidhi matakwa ya swali kikamilifu na kutaja mashairi yenye nukuu sahihi katika kuelezea jinsi uongozi mbovu unavyokuwa kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu zuri la mtahiniwa aliyeelezea *'dhuluma, uongozi mbovu, wizi, rushwa, umaskini na kutokuwajibika* kama vikwazo kwa jamii kujipatia maisha bora.

**Kielelezo 3.1**

3 Uongozi mbovu, huu ni Uongozi ambao hujali maslahi ya wachache ambao ni tabaka tawala na kuacha tabaka tawaliwa likiteseka. Ni kweli kuwa uongozi mbovu huwa kikwazo kwa jamii kupata maisha bora kwa kutumia Diwani ya Fungate ya Uhuru iliyoandikwa na Mohamed S Khatibu na Kimbunga iliyoandikwa na Haji Gora Haji. Kwa kuanza na Fungate ya Uhuru Uongozi mbaya umekuwa kikwazo kwa kufanya yafuatayo

Usaliti, kitendo cha kwenda kinyume na makubaliano viongozi wa Afrika mara baada tu ya kupata uhuru waligeuka na kuwasaliti wenzao au tabaka tawaliwa kwa kuendeleza funggate ya uhuru hii kuwafanya watu waishi maisha magumu katika shairi la "Fungate" mwandishi anasema

"Fungate ya uhuru inaendeleya
Harusi wana nuru, wazuri wapa-
utiya
Wengi inawadhuru natena waoumiya" Kwahiyo hii inaonesha jinsi gani watu wanaishi maisha duni kwaajili ya uongozi mbovu

Dhuluma, hiki ni kitendo cha kumnyima mtu haki yake. Katika maisha ya uanajamii wengi uame-


3 kuwa wakidhulumiwa haki zao kutokana na viongozi mbovu na viongozi kuwadhulumu raia haki zao kwa kuwaibia mali za uma mwandishi anaeleza haya katika shairi la "Wizi" anasema

"Wizi Umo
Ikuluni
Kasrini
Na bomani
Wanywang'anywao ni fukarani."

kutokana na hali hii wanajamii huyikuta hawapati haki zao hivyo kuishi maisha duni

Unyanyasaji, Viongozi wameku wanyanyasaji na kuzishikilia tabasamu na wanajamii wengi kwani wao ndio wanaoamua wanajamii wapate kitu fulani au wasipate hii inawafanya watu wa tabaka la chini kubaki wanyonge kwani wao tu hawana nguvu mbele ya tabaka kiongozi katika shairi la "Waja Wa Mungu" mwandishi anasema

"Duniani wanyonge kupata haki
Tabaka la juu kupenda
Abadani si waja wa mungu"


Vilevile katika Diwani ya Kimbunga, Uongozi umekua kikwazo kwa kufanya yafuatayo:
Rushua, tunaona viongozi wakitoa na kuchukua rushwa hii kufanya wachache kupata haki wakati wengi wao wakiwa katika hali ngumu katika shairi la "Rushua" mwandishi anasema
"Rushua kajenga kambi, na kuondoka hataki
Afanya kila vitimbi, mkaidi hashindiki", Hii inaonesha jinsi viongozi waliyojikita katika rushua na hivyo kufanya jamii kutokuwa na maisha bora.
Unyonyaji - kitendo cha kuchukua mali ya mtu au kuweza kuongeza bei ya kitu viongozi wamekua wakiwanyonya raia kwa kuongeza bei ya vitu hii inawafanya washindwe kupata kwa wakati hii imeonekana
3 katika shairi la "Wenye navyo Watubana ambapo bidhaa zimepandishwa bei hii kuwafanya watu kupata tabu.
Kutumia mabavu katika utawala, hii inaonesha jinsi viongozi wanavyowatawala kwa mabavu raia wao hii kufanya washindwe kupata haki na kufahamu kujitawala baada wakati wa ukoloni viongozi walitawala kwa mabavu na kufanya watu wakose haki na maisha bora katika shairi la "Kujitawala" mwandishi anasema.
"Kujitawala ni kwema kuliko kutawaliwa
Kujitawala ni umma kila yao kuamua" hii inaonesha jinsi wanajamii wanavyopata tabu pale wanapokuwa hawako huru hii kuwafanya kutaka kujitawala ili kuwa na maisha bora

Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuelezea jinsi uongozi mbovu ulivyokuwa kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora na kutoa mifano maridhawa.

Aidha, watahiniwa wengine (19.4%) walipata alama za wastani ambazo ni 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kuelezea dhamira kama vile *rushwa, matabaka, ukoloni mamboleo na kufanya kazi kwa bidii* bila kuhusisha na jinsi uongozi mbovu ulivyokuwa kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora kupitia dhamira hizo.

**Kielelezo 3.2**

3. Kiongozi ni mtu anayechaguliwa na watu toka miongoni mwao ili aweze kusimamia shughuli zote za maendeleo katika jamii husika. Lakini "Uongozi mbovu ni kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora.


Kwa kutumia vitabu viwili ambavyo ni "Kimbunga" ikiyoandikwa na Haji Gora na "Chungu Tamu" yake Theobald A. Mvungi kuthibitisha kauli ya kuwa uongozi ~~bora~~ mbovu ni kwazo cha maisha bora katika jamii.

Kwa kuanza na kitabu cha Kimbunga, Mwandishi ameonisha ukweli huu.

Rushwa; Rushwa ni kitendo cha kutoa na kupokea kitu chochote kwa muhusika ili atoe upendeleo kwa yule aliyetoa ilihali hana sifa ya kupata kile anachokitaka. Hili kauli inapatikana katika shairi la rushwa, hivyo jamii itashindwa kufikia malengo au maendeleo kutokana na rushwa.

Matabaka, ni ile hali ya utofauti -

5. iliyopo katika jamii, mfano tabaka tawala (viongozi) na tabaka tawaliwa.
Hayi Gora anaonesha matabaka kupitia shairi la Manzese mpaka Ostabei, pale ambapo hali hii inasababisha tabaka la chini kutopata maisha bora.
Ukoloni mamboleo ni hali inayo tokea katika nchi zetu, ambapo viongozi wapo madarakani kufuata wakiwakilisha matakwa ya wakoloni. Mwandishi anaone-sha hilo katika shairi la Chatu na kuku.
Umuhimu wa kupinga dhuluma, ni ile hali ya viongozi kutowatendea haki wananchi wao ambazo waliahidi wakati wakiomba kuchaguliwa, kwahiyo umuhimu wa kupinga dhuluma inapatikana katika shairi la Chanzo ni wenye kauli.
Pia kwa kutumia kifaka cha Chungu Tamu, mwandishi anaonesha hali hii.
Unyonyaji ni ile hali ya watu wenye nafasi kutotumia madaraka kama ipasavyo kwa jamii. Msanii anaonesha hali hii ya unyonyaji kupitia shairi la Chatu na kuku.
Uongozi mbaya, ni hali ya viongozi wabio madarakani kutotenda haki kwa wananchi wake, hali hii ya uongozi mbaya inapatikana katika shairi la Kademokrasi katoweka.
Kufanya kazi kwa bidii, kutoka shairi la Daktari Ashari, uongozi mbovu hautaweza kusimamia utendaji, -


3 wa kazi nzuri hivyo kuwa kikwazo kwa
jamii kufikia au kujipatia maisha bora.
Matabaka ni hali inayokuwepo ya
utofauti wa kimaisha miongoni mwa jamii,
hali hii inapatikana katika shairi la
Manzese mpaka Oslabei, pale ambapo
viongozi huwa na maisha ya juu zaidi
kuliko wananchi waliowachagua.
Hivyo ili jamii yoyote iweze kujipa-
tia maisha bora lazima kuwe na
uongozi mzuri utakaopeleka mbele
mahitaji ya wananchi waliowachagua.

Kielelezo 3.2 ni sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa baadhi ya hoja zisizo na ufafanuzi wa mashairi kulingana na matakwa ya swali.

Hata hivyo, watahiniwa wachache sana (1.5%) kati ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walipata alama za chini yaani 0 hadi 6.5 kwa kuwa walishindwa kuelezea jinsi uongozi mbovu ulivyo kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora. Baadhi ya watahiniwa walitoa hoja chache zisizojitosheleza na hata maelezo yao hayaoneshi bayana jinsi uongozi mbovu ulivyo kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora. Kielelezo 3.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kutokuwa na ufafanuzi na mpangilio mzuri wa hoja alizotoa.

**Kielelezo 3.3**

3. Uongozi mbovu ni kikwazo kwa jamii katika kupata maisha bora. Hili hudhihirika waziwazi kupitia diwani mbili zifuatazo, diwani ya kimbunga na pia diwani ya mapenzi bora. Jamii nyingi baada ya kupata uhuru na kuanza kujitawala watu wengi walidhania kuwa wangelikuwa huru na kufanya kile roho inapenda lakini mambo yalikuwa kinyume na matarajio yao, hii ilitokana na baadhi ya viongozi waliowaami kuwaongoza ila hatimaye kuwasaliti watu wao. Katika diwani ya kimbunga mshairi anazungumzi mambo mengi yanayokumba jamii kwa ujumla kwa mfano, anazungumzia suala zima la uongozi ambapo kuna aina tofauti za uongozi ukiwemo ule uongozi mbaya. Anaiasa jamii kufanya kazi katika shairi lake la kazi anawaambia vijana wengi kujishughulisha na ufanyaji kazi na kuinua kipato cha maisha mema ya kwao kuliko kutegemea viongozi waliojali jamii yao na waliowachagua.


Anasema kuwa viongozi wengi hawana maadili mema katika jamii nzima mama wao hujilimbikizia kila kitu kwa kutumia vyeo vyao. Mshairi katika shairi la viongozi, anawaasa viongozi kujua na pia kutambua uwepo na umuhimu wao katika jamii husika kwa ujumla na kutumikia watu kwa njia inayofaa na kuepuka majungu

na fikra potovu. Mshairi katika diwani ya kimbunga haswa kwenye shairi lake la kimbunga ameonyesha ni jinsi gani viongozi na uongozi wao mbaya huipoteza jamii husika kwa madai ya kutotimiza jukumu na wajibu wao katika jamii. Anaendelea kwa kusema kuwa wapiga kura ndio wanaoumia baada na hata kabla ya uchaguzi kwa ujumla.

Katika diwani ya mapenzi bora, mshairi anaongelea mambo mbalimbali yakiwemo ya uongozi mbovu, siasa ambapo siasa imechukuliwa kama mchezo wa paka na panya yaani viongozi wengi wanagwana na hivyo basi hata swala zima la uongozi wao hukabidhiana wao kwa wao.

Mshairi katika diwani ya ~~nduzo~~ mapenzi bora ameonyesha pia kwa kuna aina tofauti ya mapenzi, kuna mapenzi ya ukweli na kuna mapenzi ya uongo au ya udanganyifu. Mshairi anasema kuwa mapenzi ni ile hali ya kuipenda jamii yako, kuipenda nchi yako, kupenda familia yako na taifa lako kwa ujumla.

Kupitia mapenzi ya uongo, viongozi wengi hutumia fursa ya kuongoza watu ili kutumia nafasi hiyo kujinufaisha wao wenyewe na familia zao tu. Viongozi wanafiki hujifanya kuwa na mapenzi bora kwa jamii zao ila baada ya kupata kile wakitakacho, hubadilika na kuwa mbogo. Mapenzi ya uongo ni yale mapenzi ya kusaliti jamii yako na



nchi yako kwa ujumla. Vijana wengi hawana kazi wala makazi kwasababu, waliwachagua viongozi wanafiki waliokuwa na ahadi hata kupita uwezo wao wa kimaisha. Vijana wengi pia hawana kazi kwa kupitia uzembe na imani potovu kuwa wanachagua kazi kitu ambacho kinyafaya maisha yake duni sana duniani. Mshairi pia anaonyesha jinsi uongozi mbovu ni kikwazo kwa jamii kupitia hali ya watu iliyopo ya maisha magumu katika jamii nyingi. Hivyo basi uongozi mbovu ni kikwazo kwa jamii katika kujipatia maisha bora.

Kielelezo 3.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali vibaya na kupata alama hafifu.

### 3.3.2 Swali la 4: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*. Swali lilihusu vitabu teule vya Ushairi na lililenga kupima matumizi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha usemi kuwa ‘‘Ushairi ni msingi wa maneno yenye hekima kwa jamii ya leo,’’ kwa kutoa hoja nne kwa kila diwani na kutumia mifano kutoka katika diwani mbili alizosoma. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili limejibiwa na asilimia 44.2 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Miongoni mwao, asilimia 98.9 walijibu swali hili vizuri na kufaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kwa kupata alama 7 hadi 19.5. Chati Namba 4 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 4**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Idadi kubwa ya watahiniwa, asilimia 80.3 walijibu swali hili vizuri na kupata alama 12 hadi 19.5. Miongoni mwao, asilimia 31.8 walijibu vizuri zaidi na kupata alama 15 hadi 19.5 kwa kuwa waliweza kuthibitisha usemi kuwa ushairi ni msingi wa maneno yenye hekima kwa jamii ya leo. Watahiniwa waliweza kufafanua mambo mbalimbali ambayo ni hekima na busara zilizoko katika diwani teule kama vile; kupinga uonevu na dhuluma, matabaka, vita, uwepo wa uongozi bora, umuhimu wa elimu na hoja nyinginezo kupitia diwani teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya FUNGATE YA UHURU alitoa hoja kama vile ; *kuwa na utawala bora*, *kupiga vita suala la wizi, kupiga vita umasikini na kuwa na umoja na mshikamano*. Katika diwani ya CHUNGU TAMU alitoa hoja kama vile; *kupiga vita matabaka, kuepuka vita, kuwa na mapenzi ya dhati na kupiga vita ukoloni mamboleo* hoja ambazo ni sahihi. Aidha, mtahiniwa huyo alitoa mfano wa mashairi yanayoakisi dhana hiyo katika diwani husika. Hata hivyo, mtahiniwa huyo alikuwa na mapungufu katika utangulizi kwa sababu hakufafanua dhana ya ushairi kama msingi wa maneno yenye hekima. Kielelezo 4.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja zilizokidhi matakwa ya swali.

**Kielelezo.4.1**


4. Ushairi ni kazi ya fasihi ambayo hutumia lugha kufikisha Mafunzo na Ujumbe ndani ya jamii. Kwa kutumia Diwani mbili ambazo ni FUNGATE YA UHURU iliyo andikwa na ~~Hiyo andikwa na~~ Mohammedi S. Khatib pamoja na diwani ya CHUNGU TAMU iliyo andikwa na T. A. Mvungi. Waandishi wa diwani hizi wametumia kazi zao kwa hekima na busara ili kuweza kuasa jamii juu ya ujenzi wa jamii Mpya.

Ifuatayo ni namna Mwandishi wa FUNGATE anavyo tumia hekima ya kazi yake kufikisha somo ~~na~~ kwa jamii.

Kukuwa na utawala bora. Huu ni Mfunzo ambao huweza pigga vita Mambo yote ambayo yenye kukwepesha Maendeleo. Mfano Mwandishi katika Shairi la VIONGOZI WA AFRIKA anawaasa Viongozi wasiwe wenye kutawala kwa Mabavu wafuate Misingi ya Kidemokrasi, katika shairi la NAODHA MTWESHI ~~na~~ anausia.

Kupiga vita suala la wizi, hili ni suala linalo husisha unyang'anyi na uporaji Mali. Mwandishi ana waasa viongozi wa dini na serikali wasiwe wenye kuiba Mali za watu. Mfano katika Shairi la WIZI mwandishi anaeleza,

Kupiga vita Umaskini. hii ni hali ambayo watu kupambana vikali juu ya hali ngumu ya Maisha. Mwandishi katika Shairi la NAONA, SAMAKI DEMANI, VIONGOZI WA AFRIKA


anaonesha ni kwa namna gani umaskini una
4 vyoathiri Maisha ya Watu na pia
wanashawishi watu kupiga vita ili waweze
kujikomboa.
Kuwa na Umoja na Mshikamano.
hii ni hali ambayo watu kuungana na
kuwa kitu kimoja, Mwandishi wa diwani
hii anaonesha ni kwa namna gani watu
wanapaswa kuungana ili waweze kujenga
jamii Mpya. Mfano katika shairi la
TUUNGANE, KA GORILA, NIKIZIPATA
BUNDUKI Mwandishi anahimiza jamii ya
kuwa na Umoja na Mshikamano.
Zifuatazo ni kasoro katika diwani
ya CHUNGU TAMU.
Kupiga Vita Matabaka hii
hii ni namna watu wanavyo tofautiana
kiuchumi, jamii na kisiasa. Mwandishi
wa diwani hii anaonesha kwa namna gani
Matabaka ni kikwazo. Mfano katika shairi
la MANZESE MPAKA OSTABEI
ambapo Matabaka huweka kwa wazi kitabaka.
Kuepuka Vita. hii ni hali
ya jamii kuingia katika Migogoro inayo
sababisha Mapigano. Mwandishi ametumia
shairi la DAKTARI ASKARI kuonesha
athari za Vita ambapo huweza kupelekea
Vifo, uharibifu wa Mali za Umma
n.k. Mwandishi kupitia kazi yake
anapasa jamii isiwe na Migogoro
itakayo weza kusababisha kutokea
kwa Vita.

Kielelezo 4.1 sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyelezea jinsi washairi wanavyotumia maneno yenye hekima kwa jamii ili kuwasilisha ujumbe wao kuhusu masuala mbalimbali ijapokuwa utangulizi wake haukujitosheleza.

Hata hivyo, asilimia 18.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani 7 hadi 11.5 na watahiniwa wachache sana asilimia 1.1% pekee ndio waliopata alama dhaifu. Kwa jumla, watahiniwa hawa walitoa hoja zisizojitosheleza hususan zisizo na mifano madhubuti ili kuthibitisha jinsi ushairi ulivyo maneno yenye hekima kwa jamii ya leo katika diwani husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika majibu yake alitoa utangulizi na hitimisho dhaifu na hivyo kukosa alama eneo hilo. Aidha, Mtahiniwa huyo alitoa hoja kama; *kuwa na uongozi bora*, *kuwa na umoja na mshikamano* na mengineyo lakini hakufafanua vyema mifano ya mashairi aliyotumia katika kuthibitisha jinsi washairi wanavyotumia maneno yenye hekima kwa jamii. Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 4.2.**


4. Mikwali kwamba "Ushairi ni msingi wa Maneno yenye hekima kwa jamii ya leo" kwa kutumia diwani Mbili FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na MOHAMED S. KHATIBU pamoja na KIMBUNGA kilicho andikwa na HAJI GORA tunaweza kuona vile Ushairi kwa ni Msingi wa Maneno yenye hekima kwa jamii ya leo kama ifuatavyo.

Kwa kuanza na kitabu cha FUNGATE YA UHURU kilicho andikwa na MOHAMED KHATIBU tunaweza kuona vile ushairi ni msingi wa Maneno yenye hekima.

Kuwa na Uongozi bora; Kutokana uongozi mbaya uliopo katika jamii ya sasa - Mwandishi ameijadili kutumia Mashairi Mbali Mbali kama vile "Wizi" Mwandishi anatuonesha jinsi wizi unavyokuwa nichanzo cha kuendesha Maendeleo nyuma pia katika Shairi la "Viongozi wa Afrika" Mwandishi anatuonesha jinsi Uongozi Mbaya unavyokuwa Chanzo Cha kuendesha Maendeleo nyuma.

Kwa na Umoja na Mshikamano; Mwandishi anaonesha ni jinsi gani umoja - ambao unaleta Maendeleo Mbalimbali Mfano katika Shairi la "Tuungane" tunaona jinsi gani ambavyo wana Amasisha umoja pia katika Shairi la "Umoja" tunaweza kuona vile linavyo Amasisha watu kuungana

Kupinga Rushwa; Tunaweza kuona vile mashairi yanavyo hamasisha upingaji wa Mambo Mabaya ikiwamo Rushwa. Mwandishi anatumia Shairi la "Hongera na Bunduki"


4 Shairi hilo linaonesha kutumia Bunduki ili kupinga Mambo Mabaya yote yanayojitokeza katika jamii zetu Ikiwemo Unyonyaji, Rushwa Vitu hivi hutudisha Maendeleo Nyuma.

Kuwa Wazalendo; pia katika Shairi la "Nchi yangu" linaonesha kwa jinsi gani tunatakiwa kuwa na Mapenzi ya dhati na nchi yetu na kuwa wazalendo ili kutetea nchi yetu Kupitia Shairi hilo tunaweza kuona ni jinsi gani Mshairi - Jalogo na Manaro yanye hekima katika Jamii ya leo.

Kuwakuthibitisha hilo kwa kutumia kitabu Cha KIMBUNGA kilichoandikwa na HAJI GORA Mwandishi anaonesha ulio ushairi wake na hekima, katika Jamii ya yao.

Kuwaasa Vijana kuwa na tabia Nzuri; Mwandishi anatumia Shairi la "Vijana wa Zanzibar" kuonesha ni jinsi gani Sasa hivi Vijana wamekua na tabia Zaidi yaani tabia Mbaya hivyo basi kwa kupitia Shairi hilo Mwandishi anawaonya vijana ili kuwa na Adabu kwa walimwengu wote kwani vijana ni nguvu kazi ya Taifa

Kuwaasa Vijana Kuthamini wazazi; Mwandishi anatuonesha Jinsi Maadili yalivyo Shuka hivyo anatumia Shairi la "Wazazi" Ili kuwaasa vijana kuwaheshimu na kuwatii wazazi wao. Na hata katika Shairi la "Vijana wa Zanzibar" Mwandishi anawaonya Vijana kuwa na tabia nzuri

Kielelezo 4.2 sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kuelezea baadhi ya hoja bila ukamilifu wake.


## 3.4 SEHEMU C: RIWAYA

### 3.4.1 Swali la 5: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi,* kuhusu vitabu teule vya Riwaya na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mitazamo ya wandishi kutoka

katika riwaya mbili alizosoma kwa kutoa hoja nne kwa kila riwaya. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache sana yaani asilimia 12.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Licha ya swali hili kujibiwa na watahiniwa wachache, asilimia 95.9 ya watahiniwa hao walipata alama nzuri na kufaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 5 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 5**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 83.9 ya watahiniwa walijibu vizuri swali hili na kupata alama 12 hadi 19.5. Miongoni mwao, asilimia 32.6 walijibu vizuri zaidi na kupata alama 16 hadi 19.5. Watahiniwa hao waliweza kubainisha mitazamo ya waandishi wawili kutoka katika riwaya mbili ambayo ni ya kiyakinifu zaidi (mazingira halisi kama vile uwajibikaji, kupiga vita umaskini kujitoa muhanga na nyinginezo) kuliko mitazamo ya kidhanifu (kuutazama ulimwengu kwa uwezo wa kimungu). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu vizuri kwa kutumia riwaya ya *Vuta N'kuvute* kama vile; *Ubaguzi wa rangi ni sumu katika maendeleo au ujenzi wa jamii mpya*, *juhudi katika kazi ndio suluhisho la umasikini*, *kujitoa muhanga* na nyinginezo zinazodhirisha mtazamo wa kiyakinifu kwa mwandishi wa riwaya hiyo. Kwa upande wa riwaya ya *Mfadhili*, mtahiniwa alitoa hoja kama vile; *mapenzi na kazi ni vitu viwili ambavyo lazima kuvitenganisha*, *tenda wema uende zako, ulevi sio*

*suluhisho* na nyinginezo ambazo kwazo, mtazamo wa mwandishi umedhihirika.

**Kielelezo 5.1**

5 Mitazamo; ni namna mwandishi
anavyowaza au kufikiria katika kuandika
kazi yake ya fasihi au ni mawazo inayompa-
nya Mwandishi kutunga kazi yake ya kifasihi
ni kweli kabisa kuwa mitazamo ya wandishi
hutofautiana kila mwandishi ana mtazamo wake
au dira yake wakati anapoandika kazi ya
sanaa. Kwa kutumia riwaya mbili ambazo
ni "MFADHILI" iliyoandikwa na Husein Tuwa
pamoja na "VUTA N'KUVUTE" iliyoandikwa na
"Shafi Adam Shafi" inadhibitishwa kuwa kila
msanii ana mtazamo wake katika jamii
Kwa kuanza na kitabu cha
"VUTA N'KUVUTE" kilichoandikwa na "Shafi
Adam Shafi" kinaonyesha mtazamo wa
Mwandishi "Shafi Adam Shafi" kama ifuatavyo.
Ubaguzi wa rangi ni sumu katika
maendeleo au ujenzi wa jamii mpya; Shafi
Adam Shafi anaamini kuwa ubaguzi lazima
upingwe vikali na ndio maana kaandika
riwaya hii ya Vuta n'kuvute. Kwa mfano
katika riwaya hii Shafi Adam Shafi "ameonyesha
ubaguzi wa rangi kati ya weusi na weupe
ambao ni wahindi ambapo mwandishi
amefetea umoja na mshikamano kwa kumt-
umia mhusika "yasmin" ambaye ampambana
vikali na ubaguzi wa rangi.
Juhudi katika kazi ndio suluh-
isho la umasikini Mwandishi Shafi Adam Sh-
afi anaamini kuwa mtu ukiwa na juhudi
lazima utafanikiwa na utaepuka umasikini
Kwa mfano anamtumia mhusika Bwana Raza

5 ambayo ana juhudi ya kutafuta pesa na kufanya kazi anavyofanikiwa na kuendelea kimaisha. akijali Mbinu hii anajaribu njia nyingine na ndivyo inavyotakiwa katika maisha.

Kujitoa muhanga ni Mbinu nzuri sana au inayofaa kuleta Mabadiliko; Shafi Adam Shafi amemtumia mhusika Denge pamoja na kikundi chake chote cha akina Mambo, Sukutua kuleta Mapinduzi kwa kujitoa muhanga kupambana na utawala wa Kimabavu hivyo Mwandishi Shafi Adam Shafi anaamini kuwa kujitoa muhanga ni silaha tosha na mbinu kuntu ya kuleta Mabadiliko.

Suala la mapenzi waachiwe wawili wanaopendana, Shafi Adam Shafi anaamini kuwa mapenzi ni kwa watu wawili wanaopendana na haipaswi kuingilia mapenzi ya mtu kwa Mfano anapingana moja kwa moja na suala la kuchaguliwa Mchumba ambao ipo kwa jamii pia hivyo anaihasa jamii kuacha tamaduni hiyo mara moja kwani siyo nzuri na haina faida yeyote. kwani suala la mapenzi ni kwa watu wawili wanaopendana.

Sio katika "VUTA N'KUVUTE" tu bali hata katika riwaya ya "MFADHILI" kilicho andikwa na "HUSEIN TUWA". Mwandishi ana mitazamo yake anavyoiona jamii kama-


Mapenzi na kazi na vitu viwili ambavyo lazima kuzitenganisha; hii inamaana kuwa kama mtu utachanganya mapenzi na kazi hakuna mafanikio na utaharibu tu Husein Tuwa anamtumia mhusika Gaddibula

5 aliyechanganya mapenzi na kazi hatimaye kazi ikaharibika. vile vile mapenzi yamemwaribia kazi Dania kushuka kwa uwajibikaji kutokana na mapenzi hivyo jamii lazima iweke tahadhari. kwani mapenzi na kazi haviwiani kabisa.

Tenda wema nenda zako, hii pia ni mtazamo wa Husein Tuwa ambapo anaamini kuwa usingoje malipo ukitenda mema kwani binadamu hawana shukrani kwa mfano Husein Tuwa anamtumia Gaddibula aliyemjadhili Dania "Ini" japokuwa anajua alichomfanyia na anajua kuwa yeye ndiye aliyemsaliti Husein Tuwa amemjenga Gaddibula ili kuonyesha dhana ya kuwa ukitaka kutenda wema usiangalie ulichotendewa.

Ulevi sio suluhisho la matatizo; "Husein Tuwa" anaamini kuwa ulevi hauwezi kuwa suluhisho la matatizo. ameonyesha mtazamo huu kwa kumwangalia au kumsuka mhusika "Dania" ambaye amekuwa mlevi wa kupindukia kisa ya usaliti wa mapenzi ambapo Terry alimsaliti. akaanza kunywa pombe kali ambazo zilimletea madhara na kuugua ini. pia Gaddibula alikua mlevi wa sigara akidhani ya kuwa ni suluhisho la tatizo lake lakini kumbe sio. hivyo ni muhimu jamii kutambua kuwa ulevi sio suluhisho la matatizo. kwani kuna watu katika jamii wanadhanya pombe ndio suluhisho

Usaliti katika uhusiano inaleta utendaji mbovu katika kazi, pia ni mtazamo wa "Husein Tuwa" ambapo mwandishi huyu ameionyesha suala la usaliti kuwa ni chanzo cha utendaji kazi mbovu kwa kumtumia



5. Mhusika Gaddhibula ambaye amesalitiwa na Nyamluja. ilimpelekea Gaddhibula kutowajibika kazini na kuwa mzembe hadi kunyang'anywa wadhifa wake na kuamishwa kwenda kituo kilichopo Dar es Saalam. ambayo pia ilikua ni fadhila na huruma za Mama Mlole. hivyo Mwandishi anaamini hivyo.

Kwa kumalizia kila Mwandishi wa kazi yo jasili huiangalia jamii yake ni kipi chema au kibaya ili aweze kuandika kazi yake kwa kuangalia namna ya kuielimisha, kuikosoa, kuirekebisha jamii yake ili kuleta mabadiliko chanya katika Maisha ya kila siku hivyo Msanii ni kioo cha jamii ambaye anamulika kila kitu katika jamii kama kizuri hukiliamasisha na kukitunza kama kibaya hukikemea na kuelimisha.

Kielelezo 5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyebainisha kwa usahihi mitazamo ya waandishi wa Riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mfadhili*.

Hata hivyo, asilimia 12.0 walipata alama za wastani yaani 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa baadhi ya hoja ambazo si sahihi. Baadhi ya watahiniwa walitoa hoja sahihi ambazo hubainisha mitazamo ya kiyakinifu ya waandishi wa riwaya teule kama vile *kufanya kazi kwa bidii, uongozi bora, umuhimu wa tiba za asili na umuhimu wa elimu* (kutoka riwaya ya *Kufikirika*). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipata alama za wastani kutokana na kutoa utangulizi usioridhisha na baadhi ya hoja zilizotolewa zilikuwa sahihi bali maelezo yake hayakukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 5.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 5.2**

Mitazamo ni hali ya mwandishi kuwa na msimamo fulani ambao yeye anaona kuwa mtazamo wake ukifuatwa katika jamii utasababisha mapinduzi au maendelo ya jamii katika nyanja zote yaani kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Ni kweli kuwa mitazamo ya waandishi wa kazi za fasihi hutofautiana kati ya mwandishi mmoja na mwingine, kwa kutumia Riwaya ya VUTA N' KUVUTE iliyo-andikwa na shafi Adamu shafi pamoja na Riwaya ya MFADHILI iliyo andikwa na Hussein Tuwa. Kwa kuanza na riwaya ya vuta n' kuvuta mwand Mwandishi shafi Adamu shafi ana mtazamo tofauti na Hussein Tuwa.

Mwandishi shafi Adamu shafi ana mtazamo wa kimapinduzi kwani ameweza kueleza mambo yote yanayosababisha mivutano katika mwaya yake mambo hayo ni kama vile,

Mila na destruri zilizopitwa na wakati, kwa kumtumia mhusika yasmini ambaye ndiye mhanga wa mila na destun zilizopitwa na wakati. mfano Yasmini alilazimishwa na wazazi wake kuolewa na Bwana Raza hali ya kuwa bwana Raza ni mzee pia yasmini baada ya kuondoka kwa Bwana Raza aliolewa tena na Shihabi naye akamuweka utawani hali ambayo mwandishi ana sema lazima jamii ikombolewe.

Suala la mapenzi na ndoa Mwandishi pia ameweza kuwa na mtazamo wa kimapinduzi katika suala la mapenzi na ndoa kwa kutoa suluhi kwa suala la mapenzi na ndoa waachwe wawili waliopendana na siyo kuchaguliwa mchumba kulazimishwa kuolewa kama alivyofanyiwa.

5 Yasmini na wazazi wake.

Suala la matabaka, Pia mwandishi shafi-Adam shafi ana mtazamo wa kimapinduzi kwa sababu kaonyesha suala la matabaka linavyosababisha kukwamisha maendeleo ya jamii mfano katika riwaya hii kulikuwa na matabaka kati ya wakoloni na waafrika, hivyo Dengo na kundi lake waliamua kuungana kupambana na wakoloni ili kuondoa matabaka katika jamii.

Suala la Rushwa, pia mwandishi ana mtazamo wa kimapinduzi kwani ameonyesha suala la rushwa lilivyo shamiri katika jamii na jinsi watu wanavyotumia madaraka yao. mfano Yasmini alitaka kutumiwa na kopulo matata ili awezi kumpeleleza Dengo habari zake ili aweze kumkamata lakini yasmini hakukubaliana naye hivyo mwandishi ana msimamo wa kimapinduzi.

Vile katika riwaya ya mfadhili Mwandishi Hussein Tuwa ana msimamo wa kidhanifu kwani ameweza kueleza mambo yote yanayo kwamisha ujenzi wa jamii mpya lakini hakutoa suluhisho nini kifanyike ili kuondoa matatizo hayo.

Suala la usaliti katika mapenzi Mwandishi ana msimamo wa kidhanifu kwani yeye anadhani unaweza ~~kuisha~~ usaliti katika mapenzi unaweza kuisha endapo jamii itakombolewa mf. Usaliti alio fanyiwa Dania ~~kwa~~ ~~f~~ na jerry wakati wanaishi na baada ya kundi kumuomba msamaha tena Dania na kusameheana alimsaliti baada ya kuugua na kutekwa jerry aliwa mzamini wake wa ini. Hivyo Mwandishi hajatoa suluhisho nini kifanyike ili jamii ijikomboe na usaliti unaoendelea kutokea.


Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyebainisha mitizamo ya kiyakinifu na ya kidhanifu ya waandishi wa riwaya mbili teule na kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wachache asilimia 4.1 walipata alama hafifu yaani 0 hadi 6.5 kwa kushindwa kubainisha mitazamo ya waandishi kutoka katika riwaya mbili walizosoma. Baadhi ya watahiniwa, asilimia 1.2 walipata 0 kutokana na kukosa maarifa kuhusu mitizamo ya waandishi wa kazi fasihi. Watahiniwa wengine

walielezea mbinu mbalimbali za kiutunzi kama vile barua, masimulizi, dayalojia, hadithi na mbinu nyingine zilizotumiwa na waandishi wa riwaya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa utangulizi usiokidhi matakwa ya swali na kubainisha mitazamo ya waandishi isiyo sahihi katika riwaya teule *Mfadhili* na *Vuta N'kuvute* kwa kuandika, *mwandishi alitumia barua, masimulizi, majibizano, nafsi, matumizi ya barua, matumizi ya nyimbo, dayolojia au majibizano na hadithi au masimulizi* hoja ambazo si sahihi. Kielelezo 5.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha mitazamo ya waandishi (kiyakinifu) kutoka katika riwaya mbili alizosoma.

**Kielelezo 5.3**

5. Mwandishi: Ni mtu atumiae muda
wake mwingi katika kuandika na kuzungumza
na jamii kwa njia ya maandishi.
Mwandishi huandika mambo hayo kwa
lengo la kuelimisha jamii na kuipa
mwanga ili iweze kupata maendeleo.
Kwa kutumia vitabu viwili ambavyo ni
Mfadhili na vuta ni kuvute.
Kwa kuanza na kitabu cha
MFADHILI Mwandishi ametumia ujuzi wake
katika kuandika riwaya yake kama ifuatavyo;
~~Muundo Mwandishi ametumia~~
~~muundo~~ Mwandishi ametumia barua;
Mwandishi ametumia mtindo wa barua
katika kujenga kazi yake ili kuweza
kuwavutia wasomaji na kuwafanya wadeue
Kwa mfano wa barua iliyo andikwa
na Nyambuja kwa Gaddi bwabi.
Mwandishi ametumia masimulizi;
Mwandishi amejenga kazi yake kwa
kutumia masimulizi au hadithi ambayo
imeweza kuwavutia wengi na kuwafanya
wapende kazi yake kwa mfano. Mwanzo
wa hadithi hadi mwisho.
Mwandishi ametumia Majibizano;
Majibizano katika riwaya hii ya
Mfadhili yameonekana pale Nunu na
Baaz pamoja na Bi hanuni walipokua
wakivutana ili kumfanya akubali
kile walicho kuwa wakitaka, PIA
na sehemu nyingi Majibizano yametokea


5' Mwandishi ametumia nafsi zote
tatu, mtindo wa mwandishi umeonyesha
nafsi zote zinazotumika katika uandishi
kwa mfano nafsi ya kwanza na ya pili,
hadi ya tatu zote zimeonyeshwa katika
kitabu.
Pia katika kitabu cha vuta
ni kuvute. Mwandishi ametumia mtindo
ambao unatofautisha kazi yake na kazi
zingine za fasihi kama ifuatavyo:
Matumizi ya barua; katika
kujenga kazi yake mwandishi
ametumia barua ambazo zilikuwa
zikiandikwa na wahusika kwa
mfano Yasimini aliandika barua
kwa shihabu, mtindo huu humfanya
kazi yake iwe bora zaidi.
Matumizi ya nyimbo;
Mwandishi ametumia nyimbo katika
kufanya kazi yake iwe nzuri na
yenye kupendeza kwa mfano
Yasimini na mwajuma walikuwa
wakiimba nyimbo.
Mwandishi ametumia dayolojia
au Majibizano. Mwandishi amejipamba
kazi yake kwa kutumia majibizano
baina ya wahusika kwa mfano
Majibizano ya Yasimini na mwajuma
Mwandishi ametumia hadithi
au Masimulizi; Mwandishi ametumia
masimulizi ili kumfanya msomaji
asicho katika kusoma kazi yake


Kielelezo 5.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea mitazamo ya waandishi kutoka katika riwaya za *Mfadhili* na *Vuta N'kuvute*. Hata hivyo, mtahiniwa alikuwa na tatizo la kitahajia kama vile kutumia neno *asicho*…badala ya *asichoke*.

### 3.4.2 Swali la 6: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*. Swali lilihusu vitabu teule vya Riwaya na lililenga kupima tathmini. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20 na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha usemi kuwa ''Dunia ni tambara bovu'' kwa kutoa

hoja nne na mifano kwa kila riwaya kutoka katika riwaya mbili alizosoma.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wengi katika sehemu hii ambapo asilimia 87.5 walilichagua. Aidha, swali hili lilijibiwa vizuri na watahiniwa wengi ambapo asilimia 99.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na nzuri zaidi. Chati Namba 6 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 6**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 94.3 ya watahiniwa hao walijibu vizuri na kufaulu kwa kiwango cha juu kwa kupata alama 12 hadi 19.5. Miongoni mwao, asilimia 21.7 walifanya vizuri zaidi na kupata alama 16 hadi 19.5 kwa kuwa walithibitisha kwa usahihi usemi usemao, ‘‘Dunia ni tambara bovu’’ kwa kutoa hoja nne kwa kila riwaya. Aidha, walionesha jinsi maisha ya wahusika mbalimbali yanavyoakisi usemi huo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile, ‘‘*Dharau, ulevi, usaliti na mapenzi ya uongo*’’ kupitia *Mfadhili* na kwa upande wa *Vuta N'kuvute* akatoa hoja kama vile ‘‘ *Matabaka, mapenzi ya pesa, usaliti na mila na desturi potofu* ili kuthibitisha usemi huo. Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 6.1**

6. Ni kweli kabisa "Dunia ni tambara bovu" maana ni kweli ndani ya dunia kuna mambo mengi mabaya yanaendelea kila siku katika jamii zetu, na mambo haya hufanya kuonesha kuwa dunia imebeba mambo yote ya maovu au mambo yote mabaya yanayoendelea au yanayotokea katika jamii zetu.

Kwa kutumia vitabu viwili vya riwaya "MFADHILI kilichoandikwa na Hussein Tuwa na VUTA N' KUVUTE kilichoandikwa na Shafi Adam Shafi. ~~Kwa~~ vitabu hivi vinaonesha mambo yote mabaya yanayofanya dunia kuonekana kama tambara bovu. Kutokana na maovu au mambo mabaya yanayojitokeza ktk jamii nzima.

Kwa kuanza na kitabu cha MFADHILI kilichoandikwa na ~~Shafi~~ Hussein Tuwa kinaonesha maovu au mambo mabaya yanayofanya dunia kuonekana kama tambara bovu yani limebeba matatizo ~~maov~~ mambo mabaya. Yafuatayo ni mambo ~~mamb~~ mabaya yanayofanya dunia kuonekana kama tambara bovu.

Dharau. Katika jamii nyingi watu wanashindwa kuheshimiana kulingana na utofauti wao, wapo watu ambao humdharau watu wengine kwa utofauti wa mambo ~~mbl~~ mbalimbali mwandishi anatuonesha Dania anavyoonesha dharau kwa Gaddi bullah alipomtukana ofisini kwake na kumbeza jina kisha Dania kumdharau na kumtaja kuwa "wewe sio Gaddi bullah bali wewe ni gaidi bullah" hivyo Dania alionesha dharau kwa kumdharau Gaddi bullah, hivyo kuonekana kwa dharau katika jamii hupelekea Dunia kuonekana kama tambara mbovu limeshindwa kuondoa taka hii.

Ulevi. Dunia inaonekana ni tambara mbovu kutokana na kuwepo kwa ulevi uliokithiri katika jamii

6 ambapo ulevi huo humua na athari katika ujenzi wa taifa maana watu hulewa na kupelekea kushindwa kufanya kazi kwa bidii, suala hili la ulevi ni moja ya matatizo yaliyo katika jamii. Mwandishi anaweka wazi kwa kumwonesha Dama kukithiri kwa ulevi Dama alianza kutumia vilevi baada ya kukimbiwa na Jerry, iliamueza kutoa mawazo lakini ulevi huo ulipelekea kuharibu ufanisi wa kazi, Hivyo tumbe tuna ona kuwa ulevi nao ni moja, ya matatizo bara maovu yaliyo katika Dunia.

Usaliti, suala hili la usaliti nalolinaonekana kuwa ni tatizo ambalo lipo katika jamii nzima hivyo usaliti unaonekana kuwa ni tatizo kubwa ambalo nalo limebebwa kwenye jamii, Mwandishi anamwonesha Dama kama msaliti ambapo Dama alimsaliti Baddi kwa kutoandaa taarifa ambayo ilitakiwa kusomwa kwenye mkutano, Dama alimuliwa na Baddi bullah kuandaa taarifa lakini Dama hakuweza kuiandaa na walikubaliana hivyo Dama alimsaliti Baddi bullah, Hili tatizo lipo katika jamii yetu ambayo suala hili linafanya Dunia kuoneka ni tambara Mbovu.

Mapenzi ya Uongo, Dunia mebeba mapenzi ya udanganyifu mpaka inaoneka kama dunia ni tambara bovu maana limebeba maovu mengi, kimemo hili la mapenzi ya uongo, mapenzi ya uongo yanaonekana kwa Jerry kwa Dama, Jerry hakuwa na mapenzi ya dhati kwa Dama maana alimkaanbia siku ya ndoa hakumdi ahlama maekani vilevile Jerry hakuwa za kumpa ini kama alivyokuwa amemwahidi Dama hivyo basi mapenzi ya uongo ni moja ya tambara bovu uliopo katika jamii.

Kwa kuendelea na kitabu cha VUTA N' KUVUTE

6. Kilichoandikwa na Shafi Adam Shafi kinaonesha mambo ambayo yanapelekea Dunia kuonekana ni tambara bovu kwa kuonesha mambo mabaya au ya kiovu yanayoendelea katika jamii.

Matabaka, Dunia inaonekana kama tambara bovu kutokana na kuwepo kwa matabaka mbalimbali katika jamii, kuna tabaka la watawala na tabaka la watawaliwa, wakoloni walifanya utabaka kuwepo kwa kuwanyonya na kuwaonea raia ambapo inapelekea Denge na kundi lake kupambana kutafuta ukombozi vilevile kuna matabaka ya wenyepesa na masikini pia tabaka la rangi familia au wazazi wa Yasmini hawakutaka Yasmini kuolewa na watu wengine tofauti na asili ya kihindi. Hivyo kuna matabaka mengi ktk jamii yanayopelekea Dunia kuwa tambara bovu.

Mapenzi ya pesa, katika jamii watu wanatanguliza sana mapenzi ya pesa. Kitendo hiki utu ambapo hufanya Dunia kuonekana imebeba tambara bovu ktk jamii la mapenzi ya pesa. Mwajuma anaonekana anapenda pesa, husa mapenzi na watu wenye pesa anamshawishi Yasmini kumwacha mpenzi wake Denge ampate Shihabu mtu mwenye pesa. Hivyo mapenzi ya pesa ni ni moja ya tambara bovu katika Dunia.

Usaliti ni moja ya jambo bovu linalofanya Dunia kubeba tambara bovu maana watu husalitiana sana katika jamii hapa Yasmini alimsaliti mpenzi wake Shihabu kwa kwenda kwa ~~A~~ ~~Ad~~ Denge kuku ~~ya~~ Yasmini alimwaga na kwenda kusalimia mjumbani.

Mila na desturi potofu, Dunia imebeba tambara bovu la mila potofu zinazoendeshwa na watu katika jamii, ~~H~~ Mwandishi anamwonesha Shihabu anamfanya Yasmini utawani yani~~katto~~ lana

Kielelezo 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyethibitisha usemi ‘‘Dunia ni tambara bovu’’ kwa usahihi kwa kutoa hoja zinazoonesha maisha ya wahusika mbalimbali yalivyokuwa na mahangaiko ya kila aina.

Aidha, Asilimia 5.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani 7 hadi 11.5. Watahiniwa wachache sana (0.4%) pekee ndio waliopata alama za chini 0 hadi 6.5. Hii inatokana na kutoa baadhi ya hoja na maelezo yasiyojitosheleza katika kuthibitisha usemi usemao ‘‘Dunia ni tambara bovu.’’ Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja nzuri lakini alishindwa kutoa ufafanuzi unaojitosheleza. Mathalan, katika utangulizi wake, hoja zilizotolewa na maelezo ya hoja havina uhusiano wa moja kwa moja katika kuthibitisha


usemi husika. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 6.2**

6 Ndiyo "Dunia ni tambara bovu" kwa maana ya kwamba Dunia imejaa uozo mwingi na uovu na uchafu mwingi ambao una athari mbaya katika jamii. Kwa kutumia riwaya ya "MFADHILI" iliyoandikwa na "HUSSEIN TUWA" pamoja na riwaya ya "VUTA N'KUVUTE" iliyo andikwa na "SHAFI A. SHAFI" kwa kuanza na riwaya ya "MFADHILI" iliyo andikwa na "HUSSEIN TUWA" anaeleza jinsi Dunia ilivyojaa na uchafu na uovu mwingi kama ifuatavyo

Unafiki, hii ni tabia ya kujifanya ni mwema kwa mtu lakini kumbe ndiye adui na nyoka mbaya hii katika tamthiliya Mwandishi anatumia rafiki yake wa Gaddi Bullah kama rafiki ambaye ni mnafiki kwa Gaddi kwani alijifanya kuwa ni mwema kumbe ndiye aliye kuwa akimwibia mke wake Gaddi Bullah, na baadae kupelekea ndoa ya Gaddi Bullah na Nyambura kuvunjika, hii ni tabia iliyooza na haifai kabisa.

Ulaghai wa mapenzi, huu ni uongo wa mapenzi na katika riwaya hii mwandishi ameonyesha jinsi ulaghai wa mapenzi ulivyo kuwa ni kikwazo cha shida na matatizo katika jamii kwani Jerry alimlaghai Dania kimapenzi na wakazaa mtoto, pia Jerry alimwahidi Dania ya kuwa akirudi safarini kutoka Ulaya atakuja kumuoa lakini hakurudi na hii ilimuingiza Dania katika uongo



6 Mkali wa Mahazo ambapo kumpelekea
mpaka kutumia pombe kali.
Usaliti, pia Mwandishi anaonyesha
usaliti kama ndicho chanzo cha shida
na matatizo kwani anamtumia mhusika
Daniza kama mtu ambaye alikuwa ni
msaliti na ambaye hakuwa mwaminifu
ambapo Daniza alimsaliti Gaddi Bullah
na kuondoka na Jerry ambaye tena kwa
mara ya pili alimsaliti Daniza tena na
hii kupelekea athari kwa Gaddi Bullah na
kwa Daniza pia.
Ulevi, huu ni Utumiaji na Unywaji wa
pombe kupita kiasi, na katika ~~[illegible]~~ ya
hii riwaya Mwandishi anaeleza kuonyesha
jinsi Ulevi ulivyo na athari mbaya kwa
afya ya mwanadamu, na hii ni Daniza
mpaka ini kuharibika ni kwa sababu ya
pombe kali kutumia kupita kiasi hivyo basi
Ulevi sio mzuri kwani hupelekea hali
nguvu na afya kuharibika kama Daniza
Pia Mwandishi wa riwaya ya "VUTA
N'KUVUTE" anaeleza jinsi gani dunia ilivyo
haribika kama ifuatavyo.
Ndoa za kulazimisha, hizi ni ndoa za
kale, zinapitwa na wakati hii ni pale
ambapo wazazi wake na Yasmini walivyo
mlazimisha Yasmini kuolewa na mtu
mzee ambaye sio chaguo lake la moyoni
na hii ni mila ambayo haifai kwani
mtu anatakiwa kuchagua mwenzi
ambaye anamhitaji na kumpendana


Kielelezo 6.2 ni sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyethibitisha usemi ‘‘Dunia ni tambara bovu’’ kwa kutoa hoja na maelezo yasiyojitosheleza hivyo kupata alama za wastani.

## 3.5 SEHEMU D: TAMTHILIYA

### 3.5.1 Swali la 7: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*, kuhusu vitabu teule vya tamthiliya na lilimtaka mtahiniwa achambue dhana ya *mapenzi ya kweli* ilivyokuwa jawabu la migogoro iliyopo katika jamii kupitia tamthiliya mbili alizosoma. Swali lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 64.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Miongoni mwao, asilimia 62.0 walijibu swali vizuri kwa kuwa walielewa matakwa ya swali ipasavyo na kufaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 7 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 7**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Watahiniwa wachache, asilimia 28.8 pekee ndio waliojibu vizuri na kupata alama 12 hadi 19.5 kwani waliweza kufafanua dhana ya mapenzi ya kweli yalivyo jawabu la migogoro iliyopo katika jamii kupitia tamthiliya mbili walizosoma. Baadhi ya watahiniwa walifafanua jinsi mapenzi ya kweli yalivyo jawabu la migogoro iliyopo katika jamii kupitia tamthiliya ya 'MORANI' kwa kutoa hoja kama vile *uzalendo, kujitoa muhanga, kupambana na wahujumu uchumi* ambazo ni jawabu la mgogoro wa kiuchumi katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa utangulizi mzuri na kufafanua jinsi mapenzi ya kweli ya Bi. Pili kwa mumewe yalivyokuwa dawa

ya kuilinda ndoa yao (kutoka tamthiliya ya NGUZO MAMA). Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefafanua dhana ya mapenzi ya kweli yalivyo jawabu la migogoro iliyopo katika jamii.

**Kielelezo 7.1**


07. Mapenzi ya kweli, haya ni mapenzi halisi amba-
yo huweza kujitokeza kati ya Mtu na Mtu, Mtu na nchi
yake. Kwa kutumia ~~A~~ "Kivuli kinaishi" kitabu kilicho
andikwa na Said Mohamed na "Nguzo Mama" kitabu
kilichoandikwa na "Penina Muhando" Mapenzi ya kweli
ni jawabu la migogoro mingi katika jamii. Kwa kuanza
na "Kivuli Kinaishi"

Mapenzi ya kweli ya Mtolewa kwenye nchi yake yaliweza ku-
saidia kuwaelimisha watu ili waweze kupambana
na uongozi wa Bi Kilembwe Mtawala wa Giningi. Kwani
aliweza kupandikiza mawazo ya kimapinduzi kwa vizazi
vipya.

Mapenzi ya kweli ya Bibi Kizee kwa watoto
alipowasimulia kisa cha Giningi yaliweza kuwasaidia wa-
toto hao kuweza kupinga utawala wa Bi kilembwe
na kusaidia kuondoa migongano mingi mno jamii.

Mapenzi ya kweli kati ya wati na nchi yao
ya Giningi waliweza kujitoa muhanga ili kuondoa
au kupinga utawala wa Bi Kilembwe ambao uliku-
wa na madhara kwa jamii ile hivyo hata katika
jamii zetu tunapaswa kuwa na Mapenzi ya kweli
kwenye jamii ili kuweza kupinga utawala ~~wa~~ mbovu.

Mapenzi ya kweli ~~kwa~~ ya wazee kwenye
nchi yao ~~~~ ya Giningi ambayo walikuwa tayari kufa
nya au kutoa mawazo mazuri kuweza kuiokoa
Giningi na mwisho wake waliuwa hiyo longo ilikua




07. kuondoa migogoro katika jamii yao ya lingi.
Pia katika "Nguzo Mama" iliyoandikwa na
Penina Muhando tunaona Mapenzi ya kweli
yafuatayo:
Bi tano kwa mume wake, huyu alikuwa
na mapenzi ya dhati kwa mumewake na alipoona
Bi sita (kahaba) anamfuata mume wake aliweza
kupambana nae ili kuondoa migogoro katika ndoa
yake.
Bi pili kwenye familia yake, Huyu alikuwa
na mapenzi ya kweli kwa watoto wake na ndio
maana tunamuona yeye anafanya kazi kuweza kupata
fedha za kulelea watoto wake ili kuondokana na
migogoro kwani mumewe hatapata pesa kwaajili ya
familia yake na kusababisha yeye kuhukura
pesa ya mkewe.
Binane kwenye nchi yake, huyu alikuwa
na mapenzi ya dhati kwenye nchi yake kwani
alikuwa akiwasisitizo watu kutengeneza umoja wa
walimu ili kuweza kujikwamua na matatizo mbali-
mbali na kuepusha migogoro kwenye jamii hasa
katika suala la pesa za ~~kuende~~ kujikomboa wanawake.
Bi saba kwa watoto wake alikuwa na
mapenzi ya dhati hata baada ya kifo cha mume
wake tunaona alinyang'anywa kila kitu ila aliendelea
kuwapenda watoto wake na aliweza kuondo migogoro
kati yake na ndugu wa mume waliokuwa ~~na~~ wamemdhu-
lumu mali za mume wake.
Hayo ni baadhi ya mapenzi ya dhati au
ya kweli yaliyojitokeza hivyo tunapaswa kuwa na
mapenzi ya kweli katika jamii zetu ili kuweza
kuondoa migogoro mbalimbali.

Kielelezo 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua vizuri dhana ya mapenzi ya kweli yalivyokuwa jawabu la migogoro iliyopo katika jamii kupitia tamthiliya za NGUZO MAMA na KIVULI KINAISHI.

Hata hivyo, asilimia 33.2 ya watahiniwa walipata alama za wastani kati ya 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa baadhi ya hoja ambazo hazikujitosheleza. Baadhi ya watahiniwa hao, waliweza kufafanua jinsi mapenzi ya kweli yalivyokuwa jawabu la migogoro mingi katika jamii na kutoa mifano sahihi.

Watahiniwa wengine walieleza katika baadhi ya hoja zao jinsi mapenzi ya kweli yanavyosababisha migogoro katika jamii kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 7.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 7.2**




07. Mapenzi ya kweli ni kitendo cha kuwa na Imani na kitu au mtu bila ~~kuenda~~ kwenda kinyume nao. mapenzi ya kweli yanaweza yakawa ni kati ya mtu na mtu au kati ya mtu na nchi yake. Ni kweli mapenzi ya kweli ni jawabu la migogoro mingi katika jamii, migogoro hiyo inaweza ikawa ya mtu na mtu, mtu na Serikali au mtu na nafsi yake. Waandishi wengi wa vitabu wameweza kuonesha hali hii kwa njia mbalimbali, kwa kutumia tamthiliya mbili ambazo ni "MORANI" iliyoandikwa na Emanuel Mbogo na "KIVULI KINAISHI" iliyoandikwa na Said Mohammed. Wote wamelijadili hili.

Kwa kuanza na "MORANI" mwandishi amebainisha hili ~~kwa~~ kama ifuatavyo;

07. Mgogoro kati ya Nungunungu na Jalia; vilevile mapenzi ya kweli aliyokuwa nayo Jalia na nchi yake yamesababisha mgogoro kali yake na Nungunungu ambaye alikuwa akiiba mali za nchi kwa ajili ya kujinufaisha mwenyewe. Kwa mfano katika tamthiliya tunaoneshwa ni kwa jinsi gani Jalia anampiga Nungunungu kwenye baa bila kujali Nungunungu ana wadhifa gani eneo hilo. Hivyo msanii anaonesha mapenzi ya kweli ni kitu kinacho sababisha mgogoro katika jamii. Katika jamii zetu wapo watu ambao wana mapenzi ya dhati na kuwa chachu ya maendeleo ya jamii fulani.

Mgogoro kati ya Nungunungu na ~~Mwenda~~ Dongo; mapenzi ya kweli aliyonayo Dongo kwa nchi yake yamekuwa chanzo cha mgogoro huu ambapo Dongo anasimamia suala hili licha ya upinzani kutoka kwa Nungunungu na rafiki zake akina Yusufu na kutetea kusimamia ipasavyo na kufanikiwa kukamatwa kwa Nungu Nungu. Hivyo mwandishi ameonyesha ni kwa jinsi gani mapenzi ya kweli yalivyo chanzo cha maendeleo katika jamii. Katika jamii zetu mapenzi ya kweli yamesababisha watu wengi kuishia jela na muda mwingine yamesababisha kuwa na uongozi mzuri na kupata maendeleo hasa nchini Tanzania ambapo viongozi wameonesha mapenzi ya kweli kwa nchi yao.


Vilevile katika tamthiliya ya "KIVULI KINAISHI" mwandishi ameonesha migogoro mbalimbali iliyosababishwa na mapenzi ya kweli kama ifuatavyo:

Mgogoro kati ya Mtolewa na Bi Kirembwe; Bi kirembwe kama kiongozi wa jamii ameingia kwenye mgogoro na kijana Mtolewa ambae ana mapenzi ya kweli na jamii yake. Katika kitabu inaonesha Mtolewa anavyopigana dhidi ya uongozi mbovu wa Bi kirembwe, mapenzi ya dhati hayo hatimaye yanasababisha anakufa kwa kupigania haki yake. Hivyo msanii anashauri hatuna budi kuwa na mapenzi ya kweli hata kama yanaweza kusababisha hatari. Katika jamii vilevile wapo watu ambao wana mapenzi ya kweli na nchi yao.

Kielelezo 7.2 ni sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kufafanua baadhi ya hoja jinsi mapenzi ya kweli yanavyosababisha migogoro katika jamii kinyume na matakwa ya swali.

Asilimia 38.0 ya watahiniwa walijibu vibaya swali hili na kupata alama 0 hadi 6.5 kwa kushindwa kufafanua jinsi dhana ya mapenzi ya kweli yalivyokuwa jawabu la migogoro katika jamii kupitia tamthiliya mbili alizosoma. Asilimia 14.6 walipata alama 0 – 1 kwa kuainisha migogoro mbalimbali katika tamthiliya teule bila ufafanuzi wowote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu swali hili vibaya kwa kubainisha migogoro iliyojitokeza katika tamthiliya ya *Kwenye Ukingo wa Thim* kama vile, *mgogoro wa Hebert na George, Hebert na Martha na mingineyo* bila kufafanua ni kwa jinsi gani mapenzi ya kweli yangezuia migogoro hiyo. Hali kadhalika, katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* alibainisha migogoro kama vile, *mgogoro kati ya Chizi na shangazi yake, Bi Saba na shemeji zake, Sudi na mkewe, Bi Tano na Bi sita* bila ufafanuzi wowote. Kielelezo 7.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyebainisha migogoro katika tamthiliya teule bila kufafanua ni jinsi gani mapenzi ya kweli yalivyo jawabu la migogoro hiyo.

**Kielelezo 7.3**


7. Kwa kutumia Tamthiliya mbili kati
ya nne, k Nakiango na Tamthiliya ya "Kwenye
Ukingo wa Thim iliyoandikwa na Mwandishi E-
brahim Hussein" na Ile ya Nguzo Mama iliyo
andikwa na Mwandishi "Penina Muhando" nath
bitisha ukweli huu kwa kufafanua hoja hoja nne
Kutoka Katika Kila kitabu. Katika Tamthiliya ya
Kwenye Ukingo wa Thim mwandishi ameonesha Mig
ogoro Kama ifuatavyo:

Mgogoro kati ya Hebert pamoja
George: Katika Tamthiliya hii ya Kwenye Ukin
go wa Thim Mwandishi ameonesha Mgogoro kati
ya Hebert na George ambapo chanzo cha Mgogo-
ro uko ni baada ya Hebert kutokwenda Haru-
sini Kijijini kwao jambo ambalo lilimuuthi bwa
na George.

Mgogoro kati ya Hebert na Martha
Mwandishi pia ametuonesha Mgogoro uliojitokeza
Katika Tamthiliya hii ya Kwenye Ukingo wa Thim
kupitia Hebert na Martha. Chanzo cha Mgogoro
huu ni kuzulumiwa kwa mali za Martha baada ya
Mme wake kufariki (George). Hivyo mwandishi
ameonesha kutokuwepo kwa Mapenzi ya kweli
kati ya Hebert na Martha.

~~Mgogoro kati ya Chizi na Shang-
aze yake. Mwandishi pia ameonesha kuwepo kwa
Mgogoro kati ya Chizi na Shangazi yake. Chanzo
cha Mgogoro huu ni pale ambapo Shangazi yake
Chizi h~~

Mgogoro kati ya Chris na Martha
Katika Tamthiliya hii Mwandishi pia ametuonesha
uwepo wa Mgogoro kati Chris na Martha. Chanzo


7. Chanzo cha Mgogoro wa K. Chris na Martha ni baada ya Martha kutomuweka wazi Chris kuwa George hakuwa baba yake Mzazi. Hivyo hapakuwa na Mapenzi ya kweli kati ya Martha na Mumewe Chris.
Mgogoro mwingine ni kati ya Ukale na Usasa, Katika Tamthiliya hii Mwandishi ameonesha jinsi gani watu wanavyotofautiana juu ya Usasa Ukale na Usasa, kwa mfano, wapo watu wanaungana na Tamaduni na Mila za Kizamani wakati huo huo wapo watu wanaoungana na Mila na Tamaduni na Sasa na kupinga zile za Kale. Hivyo hakuna mapenzi ya kweli kati ya Makundi hayo mawili yanayopingana.
Katika Tamthiliya ya Nguzo Mama iliyoandikwa na 'Penina Muhando' Mwandishi ameonesha Migogoro kama ifuatavyo:
Mgogoro kati ya Chizi na Shangazi yake. Mgogoro huu umeoneshwa ambapo chanzo chake ni Shangazi yake Chizi hakumpenda Chizi kufikia hata wakati mwingine kumfukuza Nyumbani. Chanzo au Sababu za Shangazi yake Chizi kutompenda Chizi hazikuelezwa. Hivyo hapakuna na Mapenzi ya kweli kati ya Shangazi Chizi na Chizi mwenyewe.
Mgogoro kati ya Bi Saba na Shemeji zake. Chanzo cha Mgogoro huu ni pale ambapo Bi Saba alizulumiwa mali zake na Shemeji zake. Kwa mfano Bi Saba anasema "Hata Kitanda! Hata Sufuria ndio! he! nitalala wapi? na nitapikia wapi?" Hivyo hapakuna na Mapenzi ya kweli kati ya yao.


Kielelezo 7.3 ni sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali kwa kubainisha migogoro katika tamthiliya teule badala ya kufafanua jinsi *mapenzi ya kweli* yalivyo jawabu la migogoro hiyo katika jamii.

### 3.5.2 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi*. Swali lilihusu vitabu teule vya tamthiliya na lilimtaka mtahiniwa kufafanua namna kipengele cha majibizano kinavyosaidia kujenga na

kupendezesha kazi ya tamthiliya. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 34.4 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Miongoni mwao, asilimia 94.0 walijibu vizuri swali hili na kufaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 8 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 8**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia


Watahiniwa wengi, asilimia 75.3 walijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 19.5. Baadhi yao, asilimia 13.1 walipata alama za juu 16 hadi 19.5 kwa kuwa waliweza kuonesha jinsi majibizano ya wahusika yanavyosaidia kujenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya. Watahiniwa hao walielezea pia jinsi mazungumzo ya wahusika yanavyobeba mawazo ya mwandishi wa tamthiliya. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika tamthiliya ya *Morani* alionesha jinsi majibizano kati ya *Aisha na Nungunungu yanavyojenga wazo la mapenzi na uzulufu (hali ya uzee na kupungukiwa akili).* Katika tamthiliya ya '*Kivuli Kinaishi*' mtahiniwa alionesha wahusika kama vile, *Mtolewa na Bi Kirembwe* wanavyojibizana katika kuwakilisha wazo zima la kujitoa muhanga. Kielelezo 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufuata matakwa ya swali.

**Kielelezo 8.1**.

8\. Majibizano ni hali au tendo la pande mbili au zaidi zinazojibizana katika kutoa wazo au kauli juu ya suala fulani; Majibizano ni kipengele muhimu katika kuumba na kubeba wazo la mwandishi; Katika tamthilia ya ya MORANI aliyoandikwa na EMMANUEL MBOGO na tamthiliya ya KIVULI KINAISHI aliyoandikwa na SAID MOHAMED waandishi wameonesha jinsi majibizano yalivyotumiwa kujenga wazo. Kianza na tamthiliya ya MORANI aliyoandikwa na EMANUEL MBOGO anaeleza majibizano yafuatayo.

Majibizano kati ya Aisha na Nungunungu, katika tamthiliya ya MORANI mwandishi amejenga wazo la mapenzi na uzurufu, katika majibizano ya Aisha na Nungunungu, wakati Aisha alipofukuzwa shule aliende kwa Nungunungu na kumweleza kuwa amefukuzwa shule nungunungu alimjibu ovyo, wakati katika [illegible] mapenzi walikua wote na-

8 Kipindi Aisha hajaenda shule alikuwa -
anashinda kwa Nungunungu hivyo -
majibizano yao yaliweza kutoa wazo
kuu na kuumba dhamira kuu.
Majibizano kati ya Jalia na akina -
Yusuph na Mlemeta; Jalia alikuwa kama-
zi mwanamke jasiri asiyeogopa kitu aliwe-
za kuwakemea Mlemeta na Yusuph
juu ya suala la kutomuweka katika
orodha ya wahujumu uchumi Bwana Nungu-
nungu, na aliwaambia akina Yusuph na -
Mlemeta, kama wamemuulia na Nungu-
nungu ala siyo yeye Jalia, aliweza kupa-
mbana na wahujumu uchumi kwa-
hali na mali na kuweza na kufanikiwa-
majibizano hayo kumeba wazo kuu la -
kupiga vita wahujumu uchumi na kupi-
nga unafiki na usaliti.
Majibizano kati ya Jalia na -
Nungunungu, katika tamthiliya ya Nguzo...
Mwandishi ameeleza juu ya majibizano
ya Jalia na Nungunungu, wakati huo Jalia
alimfuata Nungunungu nyumbani kwake -
pia aliweza kupita getini na alikuwa -
na bunduki, katika majibizano hayo Jalia
ameonekana kuwa jasiri mtu asiyeziona
wahujumu uchumi na mwenye msimamo
na malengo, vivyo hivyo pia Nikosanga-
katika tamthiliya Kivuli Kinaishi -
kilichoandikwa na SAID MOHAMED mwa-
ndishi anaeleza majibizano yafuatayo.
Majibizano kati ya Mtolewa na -


8 Bi.Kirembwe; Katika tamthiliya ya Kivuli-
Kinaishi; Mwandishi anaelezea majibizano
yaliyotokea Kati ya Mtolewa na Bi.Kiremb-
we, pale Giningi. Mtolewa aliweza kujibi-
zana na Bi.Kirembe na Kuweza Kupatiwa
Umaarufu na kutoa wazo la Kujitoa-
Mhanga, Mtolewa hakuogopa Kitu chochote
lazima na sisi tunajamii tuweze Kujitoa-
Mhanga
Majibizano Kati ya Bawabu II na Mto-
lewa Katika tamthiliya ya Kivuli KINAISHI
Mwandishi anaonesha majibizano yaliyo-
Kuwepo Kati ya Mtolewa na Bawabu II wak-
ati wa Kuingia Giningi, Mtolewa aliweza
Kujibizana na Bawabu II na Kumuweze-
sha Kuingia Giningi Mtolewa alitoa rush-
wa na ndipo aliruhusu Kuingia Giningi:
hivyo Suala la rushwa limetoka na-
Kuzuana Kubeba wazo Kuu.
Majibizano Kati ya Bawabu wa-
I na II na Wake au yule Mfanyabiashara na-
Mwalimu pia na Mkulima, Katika tam-
thiliya ya Kivuli KINAISHI, Mwandishi-
ameelezea jinsi majibizano yalivyobeba
na Kutoa wazo Kuu la Mwandishi.
Bawabu wa I na II walijibizana na Mwalimu
Mkulima na mfanyabiashara, ambapo Maba-
wabu waliwambia Ukitaka Kuingia-
Giningi lazima utoe chochote ambayo-
ni rushwa, Mfanyabiashara alitoa rushwa
ya ~~shilingi~~ shilingi elfu 5000 ndipo-
akaruhusiwa Kuingia Giningi na.

Kielelezo 8.1 ni jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua majibizano katika tamthiliya ya *Morani* na *Kivuli Kinaishi* na kuonesha ni kwa jinsi gani yalivyoweza kusaidia kujenga na kupendezesha kazi za tamthiliya hizo.

Aidha, Asilimia 18.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani yaani 7 hadi 11.5. Kwa ujumla, watahiniwa hao walishindwa kufafanua baadhi ya hoja, ijapokuwa waliweza kutaja majibizano ya wahusika na majina yao sahihi, lakini walishindwa kuelezea umuhimu wa

majibizano hayo katika kujenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa *utangulizi* na *hitimisho* lisilowiana na matakwa ya swali na kupata alama za wastani. Kielelezo 8.2 ni sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyetaja majibizano mbalimbali kwa usahihi bila kuonesha jinsi yalivyojenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 8.2**

Pia kuna majibizano kati ya wanaopinga kuhujumu uchumi na wahujumu uchumi. Mfano mwandishi anaonesha majibizano kwa Jalia na wale wanaohujumu uchumi akina Nguruno Hungurungu. Mfano Jalia anasema hatuwezi "kuacha mapapa tukavua kelege". Majibizano haya ni ya muhimu sana kwani yanapiga vita uhujumu uchumi. Hata jamii ya sasa suala kuhujumu uchumi bado ni changamoto.

Pia kuna majibizano kati ya wale wanaopiga vita suala kuhujumu uchumi na wale wanaojifanya kuwa ni wanamapinduzi kumbe ni wasaliti. Mfano hakina Mapito, Jalia na Malongo wakijibizana na hakina Mlemeta na wenzake kwa kuwasaliti wakati wa kupambana na wale wanaohujumu uchumi.

Katika ~~riwaya ya~~ Tamthiliya ya "Nguzo mama" majibizano yamejitokeza kama ifuatavyo.


Kwanza kuna majibizano kati ya Bi nane na Mwenyekiti haya ni majibizano kwa Bi nane na mwenyekiti kale ~~M~~ walimu wanapomchukulia maneno ya uchonganishi kwa Bi nne ~~na ya na~~ yanayomhusu Binane na Bi nne kuyachukua kwa mwenyekiti na kusababisha migongano kati ya Bi nne na Mwenyekiti.

Pia kuna majibizano kati Bi Saba na shemeji zake yanatokea baada ya Bi Saba kufiwa na mme wake na ndipo shemeji zake wanaanza kumnyanganya mali zote alizoziacha mme wake na Bi Saba. Ndipo Bi Saba anaanza kujibizana na shemeji zake.

Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli majibu ya mtahiniwa aliyetaja majibizano mbalimbali na kutoa ufafanuzi usiojitosheleza.

Watahiniwa wachache sana, asilimia 6.0 walipata alama hafifu yaani 0 hadi 6.5. Watahiniwa hao kwa kiasi kikubwa walikosa maarifa ya kutosha katika kufafanua jinsi majibizano yanavyosaidia kujenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya. Baadhi ya watahiniwa hao, walitaja wahusika ambao si wa tamthiliya hizo kama vile *shinda na bapa*. Aidha, walishindwa kuonesha jinsi majibizano katika tamthiliya teule yanavyopendezesha kazi ya tamthiliya. Kielelezo 8.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejikita katika kuwatumia wahusika *shinda* na *bapa* wasiohusika katika tamthiliya teule alizopewa.

**Kielelezo 8.3**


SEHEMU D:-


8) Majibizano ni njia mojawapo inayoyepush-
elewa kutumiwa na waandishi wengi wa
tamthiliya katika kufikisha ujumbe kwa
jamii. Majibizano ni kipengele muhimu katika kuumba
na kubeba wazo la mwandishi. Thibitisha hili kwa
kutumia tamthiliya mbili ya "Mosarini" kutoka kwa
Emmanuel Mbogo na "Nguzo Mama" kutoka kwa
Penina Muhando. Kwa kuanza na kitabu cha Mosarini
kutoka kwa Emmanuel Mbogo.

Majibizano yaliyotolewa katika hiki
kitabu yamejenga na kupendezesha kazi za
waandishi kwa kujenga mandhari nzuri ya Night

club ambako kumeibua wazo la uzuvutu baina ya Nungunungu na Aisha kupitia majibizano yao ambayo Aisha alikuwa akimweleza Nungunungu kuwa Amefukuzwa shule na baba yake kapelekewa barua kuhusu utoro wa mwanae na hivyo kufukuzwa kutokana na kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi na mtumimo Nungunungu.

Pia majibizano kati ya Nungunungu pamoja na jalia yamesaidia kujenga na kupendezesha kazi za mwandishi kwa kuonesha tabia ya wahusika wawili pamoja na asitia yao ambako Nungunungu anaoneshwa kama mhujumu uchumi na jalia ni mhusika anaeyepigana ili kuondoa uhujumu uchumi hivyo pia kujenga wazo la uhujumu uchumi kupitia zile mungu baina ya jalia na Nungunungu ambako jalia anampiga na kumkamata Nungunungu bila hata ya kuogopa vitisho vyake na kusita.

Mwandishi kupitia majibizano wanajenga na kupendezesha kazi zao kwa kujenga utofauti kati ya wahusika mbalimbali ambao kuna wahusika duara ambaye ni jalia mwenye msimamo na asiyebadilika na wahusika shinda wanaobadilika kwa kuyumbishwa na kushawishiwa na wahusika duara na bapa mfano ni mhusika yusufu pamoja na wanlemeta ambako kupitia majibizano yao kunajitokeza wazo la uditi ambao unafanywa na mlemeta na yusufu kwa jalia na wanandi wote kwa kutetea ya kuwashika wahujumu uchumi ambaye ni Nungunungu. Katika kitabu cha "Ngozi Mama" pia linaonesha jinsi


majibizano yanayojenga na kupendezesha kazi za waandishi
Kupitia majibizano kati ya bi.5 na bi.6 mwandishi kazi yake inapendezeshwa kwa kutumia uteuzi mzuri wa lugha ambayo ni lugha ya matusi ndiyo iliyotumiwa katika majibizano kati yao. hivyo mwandishi kufanikisha kuonesha ni jinsi gani lugha ya matusi inavyotumika na kupitia haya majibizano pia kunazuka kwa wazo la Umalaya kwa bi.6 kutembea na mashika mume wa bi.5.
— Mwandishi kupitia majibizano amependezesha kazi yake kwa kuonesha wahusika ambao ni bapa wasiopenda kubadilika kubaki katika msimamo wao kwa kumtumia bi.8 ambaye amesimama na kusisitiza kuinuliwa kwa nguzo mama na bi.4 anaye- penda madaraka na ubinafsi kwa kutaka kubaki kung'ang'ania kuwenye uongozi, hivyo kupitia haya majibizano kunazuka kwa wazo la uchu wa mad- araka.
Pia katika majibizano kati ya bi.8 na mwenyekiti, mwandishi amependezesha kazi yake na kujenga wazo kuu kupitia majibizano ambapo pia amemchora mhusika Mwenyekiti wa kijiji cha patata kama mhusika shinda asiyeyumba na msimamo juu ya maamuzi yake na kukubali kuendeshwa na wahusika wengine kama mhusika bi.4 Nahata pia kunaujengaji wa taswira mbalimbali kama vile Nguzo Mama ambayo imetumika kuashiria ujumbe katika jamii kuwa ni muhimu wanaume, wanawake pamoja na watoto wote kuungana ili kuweza kuleta maendeleo kwa akina mama na jamii kwa ujumla.


Kielelezo 8.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejadili hoja ya kupendezesha kazi ya tamthiliya kwa kutumia wahusika ‘‘shinda’’ na ‘‘bapa’’ ambao si wahusika wa tamthiliya zilizoorodheshwa.

## 3.6 SEHEMU E: USANIFU WA MAANDISHI

### 3.6.1 Swali la 9: Usanifu wa Maandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Usanifu wa Maandishi* na lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari na kisha kubainisha vipengele vya fani vilivyotumika. Swali lililenga kupima majazi ya utambuzi katika ngazi ya uchambuzi na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la lazima. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 87.2 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Namba 9 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 9**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 36.9 walijibu vizuri na kupata alama 12 hadi 20. Watahiniwa hao waliweza kueleza mbinu za kifani zilizotumika katika habari waliyopewa kama vile, muundo (*muundo wa moja kwa moja*), mtindo (*mtindo wa masimulizi*), matumizi ya nafsi mbalimbali anaposema (*anapokaa.., akashuka..*), matumizi ya lugha ya kutohoa kiingereza (*bladiful..*), wahusika *kondakta wa basi, Buricheka, dereva wa basi, mama mgonjwa, mama msafiri na Jaluo.* Aidha, watahiniwa wengi walitaja na kutoa mifano ya mandhari ya tukio kwa usahihi. Kielelezo 9.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kueleza mbinu

mbalimbali za kifani zilizotumika katika habari waliyopewa kwa usahihi.

**Kielelezo 9.1**.

9. (a) MUUNDO

mwandishi ametumia muundo wa moja kwa moja kwa kuwa ameeleza kuanzia mwanzo wa hadithi hadi mwisho.

(b) MTINDO

mwandishi ametumia mitindo mbalimbali kama ifuatavyo

(i) mtindo wa masimulizi

- hii ni kwasababu kuna msimuliaji anayesimulia tukio jinsi ilivyokuwa.

(ii) matumizi ya nafsi

mfano nafsi ya tatu umoja hasa anaposema "anapokaa....", "akashuka...."

(iii) matumizi ya lugha ya kiingereza

mwandishi ametumia baadhi ya maneno ya kiingereza kama vile "Bladiful!".

(c) WAHUSIKA

mwandishi ametumia wahusika mbali mbali kama vile

(i) Kondakta wa basi

(ii) Buricheka

(iii) dereva wa basi

(iv) mama mgonjwa

(v) mama msafiri

(vi) Jaluo

(d) MANDHARI

mwandishi ametumia mandhari ya kubuni ambayo siyo ~~halisi~~ halisi na pia

9. ametumia mandhari ya barabarani kwa kuwa ameelezea mambo yanayotokea barabarani. wakati wa kusafiri.

(e) MATUMIZI YA LUGHA

- Lugha iliyotumika kwa ujumla inaeleweka kwa kuwa msanii ametumia msamiati unaoeleweka na kufahamika kwa wengi. pia mwandishi ametumia tamathali za semi na mbinu nyingine za lugha kama ifuatavyo:-

(i) matumizi ya takriri, huu ni urudiaji wa maneno yanayofanana hasa kwa kuyafuatanisha maneno hayo. mfano "pisha... pisha.... pisha!"

(ii) matumizi ya mdokezo, ~~huu ni~~
- hii ni mbinu ya kisanaa ambapo baadhi ya maneno au silabi huachwa kuandikwa kumuacha msomaji amalizie. mfano "Hakufua ....", "pisha...", "akashangaa..."

(iii) matumizi ya tashbiha, hii ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha vitu viwili tofauti kwa kutumia viunganishi. mfano (a) kijana mmoja alionekana ~~kama~~ amenyoa nywele kama ugitugiti wajogoo"
(b) kila mtu alizonga rafiki mithili ya mbuzi wanaogwagwa...

(iv) matumizi ya tashihisi, hii ni tamathali ya semi ya kupa ~~sifa~~ vitu sifa

9. za binadamu. mfano
(a) --gari lile lililokuwa likilamba lami ---

(v) Matumizi ya misemo
mfano
(a) Simba akizidiwa hula majani
(b) Asiyekujua hakuthamini
(c) Zimwi likujualo hadi mwisho halikusui.

(vi) matumizi ya vifupisho vya maneno. mfano UDA.

(vii) matumizi ya mubalagha, hii ni mbinu ~~mfano~~ ya kuongeza chuku. mfano
(a) baiskeli kule! miguu juu!

Kielelezo 9.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri kwa kutaja na kufafanua mbinu mbalimbali za kifani zilizotumika katika habari aliyopewa.


Aidha, watahiniwa wengi (50.3%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza katika kubaini mbinu mbalimbali za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari. Baadhi ya watahiniwa hao waliweza kuzichambua baadhi ya mbinu za kifani kama vile, *wahusika, muundo, mtindo, mandhari na matumizi ya lugha.* Kielelezo 9.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye aliweza kubainisha baadhi tu ya mbinu za kifani na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 9.2**

9 Vipengele Vya Fani, Fani ni
Umbo la nje la kazi ya Fasihi, Vipe
ngele vya fani, Ni Vipengele amba
Vyo humtofautisha Msanii mmoja
na Mwingine, Vipengele hivi Ndivyo
huwa Vinaonesha Upekee wa Mwa
ndishi mmoja na Mwingine. Vifuatavyo
ni Vipengele Vya Fani Vilivyotumika
Katika Matini hayo ni:-
Wahusika, Ni watu au
Vitu ambavyo hutumiwa na Mwandishi
Katika kazi ya Fasihi, Katika Matini
hii Msanii ametumia wahusika
ambaoni binadamu, wahusika hao
ni pamoja na Buncheba, Kondakta
Mama, Kijana mmoja amenyoa Nywele
kama ugiligili wa jogoo na pia
Jaluo ambao huwa wahusika
wanesaidia Katika kukamilisha Visa,
Ujumbe katika Matini hii
Muundo, Mpangilio wa
Visa na Matukio katika Matini
hii ni Moja kwa Moja kwani
tunaona tukio la kwanza kabla
Gari halija wasili kulitokea ajali,
Gari lilipofika kulitokea Mgogoro
na hata baada ya Gari kuondoka
huyo kutokana na Mpangilio
huu unampa msomaji urahisi wa
kujua Visa na Matukio vilivyo
katika Matini hii,

9. Mtindo, Ni ile Namna au jinsi ya Mwandishi kulieleza jambo katika Matini hii Mwandishi ametumia Mtindo wa Masimulizi ambapo Msani amesimulia Visa na Matukio kutoka Mwanzo mpaka Mwisho Lakini kwa Kiasi ki dogo Mwandishi wa Matini hii ametumia Mtindo wa Majibizano Kwamfano Kijana mmoja alisema "Oya we Mama toa Makalio Yako njiani tunashuka" na yule Mama Akamjibu "Shuka Zenyewe ziko wapi? peleka ~~Ki~~ Fito zako huko,

Mandhari, Ni eneo au Sehemu ambayo kazi ya Fasihi hufanyika, Mandhari katika Matini hii ni Mandhari Halisi kwani tunaona Maeneo kama Mwanza, Buiru na Kituo Cha basi ambayo Vyote hivi Vinapatikana katika Mandhari halisi, Mwanza na Buiru Vinaonesha Matini hii ni Mandhari halisi katika Nchi ya Tanzania kwani inamkoa wa Mwanza na kuna eneo linaloitwa Buiru, Mandhari nyingine ni Ndani ya Basi na Mandhari ya Barabarani, Kuenye Lami ambapo ajali ya Baiskeli Ilitokea.



9. Matumizi ya Lugha,
Katika Matini hii Mwandishi ametumia Lugha rahisi na Inayoeleweka
kakini Lugha hii Imejaa Misemo,
Methali na Nahau Mbali mbali
kama vile: Simba akienda kula
Majani, Dunia tambara bovu, Asiye
kujua hakuthamini.
Pia katika Matumizi
Ya lugha kuna Matumizi ya
Kingereza kwa mfano: Bladi ful"
'Stupid' ambayo imetokana na
Utumizi wake hivi Mwandishi
anaonekana kutofauta kifani
Matumizi ya Tamathali
Za Semi, Kwamfano Takriri iliyo
jitokeza ni "Nimepatwa, Nimepatwa,
na Pisha, Pisha, Pisha, Pia tamathali
ya Semi nyingine ni Tashihisi,
mfano neno Pyaaaa!
Matumizi ya Viswahili
badaya ya Kiswahili, Kwamfano
"Musa ona kuisa kanyaga mimi?
Dunia Musma Inasaidika amani wewe
inakanyagana? "Siku mingine tafyeka
koromeo lako"
Matumizi ya lugha za
Matusi, Pia Mwandishi wa
Matini hii ametumia lugha za
Matusi kwamfano: Mwanaharamu
we! na "Oya we mama toa Makalio
Yako njiani tunashuka.

Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa ambaye aliweza kubainisha baadhi ya mbinu kama *muundo, mtindo, mandhari na matumizi ya lugha*; ijapokuwa hakufafanua vizuri kipengele cha matumizi ya lugha.

Watahiniwa wachache asilimia 12.8 waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 6.5 kwa kuwa walishindwa kueleza mbinu mbalimbali za kifani zilizotumika katika kifungu cha habari kama vile, *wahusika*, *mandhari na matumizi ya lugha*.

Aidha, watahiniwa hao waliweza kutaja baadhi ya mbinu kama vile *muundo, matumizi ya tashihisi* na *takriri* lakini hawakufafanua jinsi mbinu hizo zilivyotumika katika kifungu cha habari. Kielelezo 9.3 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubaini na kufafanua mbinu anuwai za kifani zilizotumika katika matini husika.

**Kielelezo 9.3**


9. Fani ni ufundi au ustadi alioutumia mwandishi katika kazi yake. Vifuatavyo vi ni vipengele vya fani vilivyotumika katika habari au matini hii.

Mtindo, msanii ametumia mtindo wa daiolojia, ambapo ametumia utiririko wa ~~wosi~~ matukio katika kazi yake kuanzia mwanzo mpaka mwisho na lugha iliyosheheni msamiati wa kutosha.

Muundo, mwandishi katika matini hii ametumia muundo wa ki mapokeo kwani kwa kupanga kazi yake katika aya. Ambapo tunaona aya tatu katika matini hii.

Matumizi ya tashihisi, Mwandishi ametumia lugha ya picha na Mfano, Mungu juu, Endoa injini Kiuno we!

Pia katumia takriri kama vile Mkikimkiki" ni mfano wa maneno yanayoandikwa kwa kujirudia rudia

Mchanganyiko wa lugha ya kiswahili na kiingereza kama vile Stupid!

Kielelezo 9.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyebainisha *mtindo* na *lugha mchanganyiko* kama mbinu pekee za kifani zilizotumika katika matini aliyopewa na kupata alama za chini.

## 4.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

Uchambuzi wa kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili unaonesha kuwa, watahiniwa walifanya vizuri katika mada ya *Utungaji* (98.9%), *Ufahamu na Ufupisho* (96.1%), *Usanifu wa Maandishi* (87.2%) na *Matumizi ya Sarufi* (85.6%). Hata hivyo, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo kwa mwaka 2017 kilikuwa ni cha juu zaidi ikilinganishwa na mwaka 2016 ambapo kiwango cha kufaulu kilikuwa: *Utungaji* (96.1%), *Ufahamu na Ufupisho* (95.7%), *Usanifu wa Maandishi* (81.9%) na *Matumizi ya Sarufi* (68.7%) ambavyo ni viwango vya chini zaidi vya kufaulu. Hata hivyo, mada ya Ushairi ilikuwa na kiwango sawa cha kufaulu kwa watahiniwa yaani (98.7%) kwa mwaka 2016 na 2017.

Aidha, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada ya *Riwaya* (96.3%), *Maendeleo ya Kiswahili* (82.6%), *Tamthiliya* (78.0%), *Utumizi wa Lugha* (75.5%), *Tafsiri na Ukalimani* (42.2%) na *Fasihi kwa Ujumla* (36.3%) kilikuwa ni cha chini zaidi ya mwaka 2016 ambapo mada hizo yaani *Riwaya* (98.5%), *Maendeleo ya Kiswahili* (95.6%), *Tamthiliya* (97.7), *Utumizi wa Lugha* (98.1%), *Tafsiri na Ukalimani* (66.2%) na *Fasihi kwa Ujumla* (92.4%) zilikuwa na kiwango cha juu zaidi cha kufaulu ikilinganishwa na mwaka 2017.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada mbalimbali kwa mwaka 2017 kilikuwa kizuri ambapo asilimia 79.8 walipata alama zaidi ya 35. Hata hivyo, kiwango hiki ni cha chini zaidi ikilinganishwa na kiwango kizuri zaidi cha kufaulu cha watahiniwa kwa mwaka 2016 ambapo asilimia 89.7 walipata alama zaidi ya 35. Pamoja na muachano huo, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa miaka miwili mfululizo kinadhihirisha kwamba watahiniwa wengi wana uelewa katika ujifunzaji hivyo kupata umahiri wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa.

## 5.0 HITIMISHO

Kwa jumla, kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2017 kilikuwa kizuri ambapo asilimia **99.88** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata alama 35 au zaidi. Kiwango kizuri cha kufaulu kimetokana na watahiniwa kuwa na ujuzi na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa. Kiwango hiki cha kufaulu kwa watahiniwa kimekuwa na upungufu wa asilimia 0.6 ikilinganishwa na kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2016 ambapo wastani wa kiwango cha kufaulu kilikuwa **99.94.**

Aidha, wastani wa kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2017 katika mada zote ni asilimia 79.8, kiwango ambacho ni cha chini zaidi ikilinganishwa na asilimia 89.7 ya ufaulu wa mada kwa mwaka 2016.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kufanya vizuri kama vile; uelewa mdogo wa matakwa ya swali, mtiririko usiokidhi vigezo vya uandishi, uelewa mdogo wa mada mbalimbali na uwezo mdogo katika kujibu maswali. Kadhalika, watahiniwa hao walishindwa kutoa mifano sahihi na ya kutosha katika kujenga hoja za kujibu swali na kutokufuata maelekezo ya swali.

Uchambuzi wa kufaulu kwa mtihani huu unaonesha kuwa watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani katika mada zote. Ufaulu mzuri wa mwaka 2017 umetokana na watahiniwa kuwa na ujuzi na weledi wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa.

Mwisho, taarifa hii iwe changamoto katika kuwasaidia walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutokujibu vizuri maswali hususani katika mada za *Tafsiri na Ukalimani* na *Fasihi kwa Ujumla*. Aidha, taarifa hii itakuwa na tija kwa walimu katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani, na hivyo kuinua kiwango zaidi cha kufaulu kwa watahiniwa katika somo hili. Pia taarifa hii itatoa hamasa kwa wanafunzi na hasa ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa ambapo kila mtahiniwa anapaswa kujieleza vizuri bila kikwazo chochote huku akijiamini na kujivunia kuwa lugha hii ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania.

## 6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi inapendekezwa kuwa :

(a) Kuboresha kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika mada za Tafsiri na Ukalimani na Fasihi kwa Ujumla, mada ambazo zilikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu, inasisitizwa kuwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa mada hizo mbinu shirikishi itumike.

(b) Katika mada ya *Tafsiri na Ukalimani*, watahiniwa wapewe mazoezi ya kutosha katika kutafsiri matini mbalimbali ili wajue mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kufanya tafsiri kama vile kujua maudhui ya matini chanzi, kuchunguza misamiati ya matini chanzi na kupitia rasimu (maandiko) mbalimbali ili kufanikisha tafsiri ya matini husika. Aidha, walimu wa lugha ya Kiswahili waandae warsha katika mikoa yao ili kujengeana uwezo wa namna ya kufundisha mada hii kwa kuwa ufaulu wake si wa kuridhisha.

(c) Kwa upande wa *Fasihi kwa Ujumla*, watahiniwa washiriki katika kutunga na kuwasilisha kazi za fasihi ili kubaini tofauti kati ya kazi za fasihi za Kiswahili na zile zinazotumia lugha ya Kiswahili. Aidha, watahiniwa washiriki pia katika kutunga kazi mbalimbali za fasihi simulizi kupitia tanzu zake ili kubaini kazi mbalimbali za wahusika kama vile *hadhira* na *fanani*.

(d) Kipengele cha fani katika uchambuzi wa vitabu teule vya fasihi kipewe kipaumbele zaidi hasa katika kuvisoma na kuweza kujua mbinu za kifani zilizotumika kufikisha ujumbe.

(e) Wizara ya TAMISEMI kitengo kinachoshughulikia elimu kiandae semina elekezi kwa waalimu wa Kiswahili ili kuongeza ujuzi zaidi kwenye baadhi ya mada kama vile *Tafsiri na Ukalimani* na *Fasihi kwa Ujumla.*

**Kiambatisho A**

## ULINGANIFU WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2016 na 2017

| Na. | Mada | 2016 | | | 2017 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Maswali | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 35 au Zaidi | Maoni | Idadi ya Maswali | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 35 au Zaidi | Maoni |
| 1 | Utungaji | 1 | 96.1 | Vizuri | 1 | 98.9 | Vizuri |
| 2. | Ushairi | 2 | 98.7 | Vizuri | 2 | 98.7 | Vizuri |
| 3. | Riwaya | 2 | 98.5 | Vizuri | 2 | 96.3 | Vizuri |
| 4. | Ufahamu na Ufupisho | 2 | 95.7 | Vizuri | 2 | 96.1 | Vizuri |
| 5. | Usanifu wa Maandishi | 2 | 81.9 | Vizuri | 1 | 87.2 | Vizuri |
| 6. | Matumizi ya Sarufi | 2 | 68.7 | Vizuri | 3 | 85.6 | Vizuri |
| 7 | Maendeleo ya Kiswahili | 2 | 95.6 | Vizuri | 2 | 82.6 | Vizuri |
| 8. | Tamthiliya | 2 | 97.7 | Vizuri | 2 | 78.0 | Vizuri |
| 9. | Utumizi wa Lugha | 2 | 98.1 | Vizuri | 1 | 75.5 | Vizuri |
| 10. | Tafsiri na Ukalimani | 1 | 66.2 | Vizuri | 1 | 42.2 | Wastani |
| 11. | Fasihi kwa Ujumla | 2 | 92.4 | Vizuri | 2 | 36.3 | Wastani |

**Kiambatisho B**

## UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

## 121 – KISWAHILI – 2017

